**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA SABA**

**Kikao cha Nne – Tarehe 13 Aprili, 2007**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Samuel J. Sitta) Alisoma Dua*

**MASWALI NA MAJIBU**

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nimebaini kwamba tunashindwa kumaliza maswali yale 15 au 16 tunayoweka kwenye *Order Paper* kila siku kwa sababu kiasi kikubwa cha maswali yenu na ya nyongeza yanakuwa marefu sana na pia majibu kutoka Serikalini mara nyingine yanakuwa marefu mno. Kwa hiyo, nawasihi hebu tujaribu leo tulenge katika kiini cha swali na swali la nyongeza lilenge pale pale kwenye swali la msingi ili maswali na majibu yaweze kutosheleza bila kuwa na hadithi ndefu mno. Swali la kwanza, linaelekezwa kama kawaida Ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, linaulizwa na Mheshimiwa Mgana Msindai, Mbunge wa Iramba Mashariki, CCM.

Na. 40

**Bima ya Maisha kwa Wabunge**

**MHE. MGANA I. MSINDAI** aliuliza:-

Kwa kuwa, Waheshimiwa Wabunge hawana bima yoyote ya kuwalinda hasa wanapofanya kazi zao vijijini, porini na wanaposafiri Nje na Ndani ya Nchi:-

Je, Serikali inasemaje juu ya kuwapatia Waheshimiwa Wabunge Bima ya maisha?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. DR. LUKA J. SIYAME)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mgana Msindai, Mbunge wa Iramba Mashariki, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa hakuna utaratibu rasmi wa bima uliowekwa na Serikali kwa ajili ya safari za Mbunge Vijijini, porini, nje na ndani ya nchi isipokuwa tu kama atatumia usafiri wa ndege ya Serikali. Hii ni kwa mujibu wa masharti ya kazi ya Mbunge yaliyotolewa na Serikali kupitia Waraka wa Ofisi ya Rais wenye Kumb.Na. CAB. III/338/01/13 wa tarehe 21 Oktoba, 2005. Sera ya Bima nchini inalenga katika kulinda watu wa mali dhidi ya uharibifu, ajali na madhara yanayotokea kwa bahati mbaya kutokana na hitilafu mbalimbali na kuweza kufidiwa sehemu ya thamani kama zilivyosajiliwa. Zipo aina nyingi za huduma za bima hapa nchini ambazo zinatolewa ili kupunguza makali ya athari za ajali na majanga yasiyotabirika. Huduma hizo ni pamoja na za mali, vyombo vya usafiri, watu binafsi na watu wanaokuwemo ndani ya vyombo na mali wakati inapotokea ajali.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa masharti ya kazi ya Mbunge, huduma ya bima ya maisha siyo moja ya maslahi aliyoainishwa. Hivyo basi, wito wa Serikali kwa Waheshimiwa Wabunge ni kuwahimiza wajiwekee bima ya maisha na kuhakikisha mali zao ikiwemo nyumba au gari binfasi la Mbunge vinawekewa bima ya majanga makubwa *(comprehensive insurance*) ili ajali inapotokea bima hiyo itumike kufidia madhara kwa mali yake na kwake yeye mwenyewe binafsi.

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza. Kwa kuwa matatizo mengi yanatokea sasa hivi kwa mfano, kuna ajali ya ndege ilitokea Mbeya ambayo Mheshimiwa Mbunge na Waziri alifariki, na juzi juzi hapa Waheshimiwa Wabunge walipigwa kule Kilwa na kuumizwa vibaya; na kwa kuwa sasa hivi Bunge ni *pillar* ya tatu. Je, ni lini sasa Serikali itaachia ili Bunge lijitegemee liweze kuanzisha bima zake lenyewe? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. DR. LUKA J. SIYAME):** Mheshimiwa Spika, Serikali inakiri kweli kwamba kuna ajali nyingi zinazotokea siku hizi, lakini pia Serikali inaweka wazi kwamba jambo hili ni vyema likapelekwa kwenye Tume ya Huduma za Bunge likajadiliwa na kutolewa mapendekezo ili liweze hapo baadaye na kuletwa hapa Bungeni na kupitishwa kwa utaratibu uliopo.

Na. 41

**Mawasiliano ya Barabara**

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE** aliuliza:-

Kwa kuwa, mawasiliano ya barabara ni muhimu sana kwa maendeleo ya nchi na Serikali kwa kulitambua hilo imetoa Shs. 10 bilioni kwa ajili ya matengenezo ya barabara zilizoharibiwa na mvua; na kwa kuwa, Mkoa wa Dodoma umepewa Shs. 508,500,000/= kwa ajili ya matengenezo ya barabara zilizoharibiwa na mvua katika Mkoa huo:-

(a) Je, katika mgao wa fedha hizo, Wilaya ya Mpwapwa imepewa kiasi gani?

(b) Je, Serikali inafahamu kwamba, barabara za Wilaya ya Mpwawa hasa ile ya kutoka Mbande-Mlali, Kongwa-Mpwapwa, Gulwe-Mima-Seruka; na ile ya kutoka Mpwapwa-Kimagai-Godegode – Pwaga hadi Mbuga zimeharibika sana na kusababisha kero kwa wananchi wanaozitumia barabara hizo?

(c) Je, Serikali itakubaliana nami kwamba, fedha hizo zitumike pia kujenga daraja la Godegode ambalo ni kiungo kikubwa kati ya Jimbo la Mpwapwa na Kibakwe?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa George Malima Lubeleje, Mbunge wa Mpwapwa, kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali imetenga shilingi bilioni 10 kwa mwaka wa fedha 2006/2007 kwa ajili ya matengenezo ya barabara zilizoharibiwa na mvua nchini kote na kati ya fedha hizo Mkoa wa Dodoma umetengwa shilingi milioni . 508,500,000. Fedha hizi zitahudumia barabara za Mkoa ambazo ziko chini ya Wakala wa Barabara *(TANROADS).*

Mheshimiwa Spika, fedha hizi zitagawanywa Kiwilaya. Hata hivyo, katika barabara zitakazotengenezwa katika Wilaya ya Mpwapwa ni barabara ya Ngambi - Mpwapwa – Mlali hadi Pandambili ambazo zimetengewa shilingi milioni 90 na barabara ya Mpwapwa hadi Gulwe ambayo imetengewa shilingi milioni 4. Hivyo kati ya fedha hizo shilingi milioni 508,500,000 ni shilingi milioni 94 tu ambazo zitatumika kwa ajili ya ukarabati wa barabara Wilayani Mpwapwa ambazo ziko chini ya Mkoa.

(b) Mheshimiwa Spika, kwa barabara zile zinazohudumiwa na Halmashauri, Serikali iliziagiza Halmashauri zote nchini mnamo mwezi Januari, 2007 zifanye ukaguzi wa barabara zilizoharibika sana kutokana na mvua na kuandaa makisio ya matengenezo ya barabara hizo na Halmashauri ya Mpwapwa ni mojawapo. Katika matengenezo ya Barabara ya Gulwe- Mima – Seruka (km 64) jumla shilingi milioni 269,286,000/= zinahitajika. Kwa barabara ya Mpwapwa - Kimagai – Godegode – Pwaga- Mbuga (km 90) kiasi cha shilingi milioni 318,632,000/= zitahitajika, hii ikijumuisha ujenzi wa daraja jipya la Godegode.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa gharama hizi za matengenezo ni kubwa na hazikuwepo katika Bajeti ya mwaka wa fedha 2006/2007 Serikali inashauri Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa kutumia fedha za Mfuko wa Barabara katika kufanya matengenezo ya maeneo korofi tu ili kufungua mawasiliano katika barabara hizo kwa kuzingatia vipaumbele. Aidha, kutokana na umuhimu wa barabara hizo

Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa imeziingiza kwenye mpango wa Bajeti yake kwa mwaka wa fedha 2007/2008 ili kuziimarisha zaidi katika maeneo korofi.

Mheshimiwa Spika, Serikali inakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba ujenzi wa daraja la Godegode ni muhimu sana kwani ni kiungo kikubwa cha Majimbo ya Mpwapwa na Kibakwe na linaunganisha pia Bonde la Kilimo cha umwagiliaji huko Lumuna.

Kwa kutambua umuhimu huo Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa imeweka ujenzi wa daraja hili katika Mpango wa Miradi ya Maendeleo kwa mwaka 2007/2008 kwa kutenga kiasi cha shilingi 95,000,000 ambazo zitatumika kujenga daraja hilo.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE :** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu –TAMISEMIi. Kwa kuwa hivi karibu Mheshimiwa Naibu Waziri, hivi karibuni alitembelea Wilaya ya Mpwapwa na alipata shida sana kupita katika barabara hizo hasa maeneo ya Ihondo, Mima na yeye mwenyewe anakiri hilo. Kuendelea kutenga milioni 25 kutengeneza barabara za Wilaya katika Wilaya zetu kufuatana na huo Mfuko wa Barabara unaotengwa kila mwaka. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri atakubaliana nami kwamba fedha hizo hazitoshi, sasa fedha ziongezwe kama tulivyoomba kwamba angalau asilimia 40 ya fedha za barabara ziweze kutengwa kwa ajili ya Halmashauri zetu badala ya hiyo asilimia 30 ambayo tunapewa sasa. Hilo swali la kwanza.

La pili, kwa kuwa, hivi karibuni daraja la barabara ya kutoka hospitali ya Wilaya ya Mpwapwa, Hazina kwenda Ving'hawe karibu na eneo la *TANESCO* Mpwapwa limebomoka na magari hayapiti sasa, gari zote zinapita barabara ya kutoka Mpwapwa, Majengo hadi Ving'hawe. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa sababu hii ni dharura Serikali itakuwa tayari kutenga fedha ili waweze kujenga daraja hilo hata kutupatia *bail bridge?*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, kuhusu swali la kwanza ni kwamba sera hizi tumejiwekea sisi wenyewe na utaratibu huu tumejiwekea sisi wenyewe wa asilimia 30 na asilimia 70. Asilimia 30 kwa ajili ya Halmashauri na asilimia 70 zinaenda kwa ajili ya barabara za Kitaifa na barabara za Mikoa. Sasa kwa utaratibu huo tutaendelea kutenga hizo asilimia 70 na asilimia 30 mpaka utaratibu utakapobadilika. Hilo naomba tulichukue ili tulifanyie kazi. Siwezi nikatoa jibu la haraka haraka.

Mheshimiwa Spika, kuhusu fedha za dharura kwa ajili ya daraja hilo. Naomba Mheshimiwa Mbunge hilo aliombe kama dharura katika Ofisi yetu. *(Makofi)*

**MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini kwa kuwa msingi wa fedha hizi bilioni 10 ni kukutana

na ile dharura ya uharibifu mkubwa wa barabara na hasa uliotokea vijijini kutokana na mvua zilizonyesha; na kwa kuwa mvua hizo pia zimesababisha wananchi wamepata mazao mengi kule vijijini. Mimi ningedhani na pengine kushauri kwamba fedha hizi zingeelekezwa vijijini zaidi kuliko kutengeneza barabara za Mikoa ambazo zimekuwa zikitengenezwa mara kwa mara. Kwa msingi huo nataka kujua je, Serikali haioni umuhimu wa busara hii? *(Makofi)*

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa George Simbachawene, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli hizo mvua zilizonyesha na zinazoendelea kunyesha katika sehemu mbalimbali za nchi yetu zimeleta madhara makubwa sana katika barabara zetu na hapo hapo zimeleta neema kwa maana ya kupata mazao mengi zaidi.

Lakini kama Serikali ilivyosema humu Bungeni zile shilingi bilioni 10, zililenga katika barabara ambazo zinaunganisha Mikoa yetu na lengo lake lilikuwa ni kuhakikisha kwamba angalau mawasiliano kati ya Mkoa mmoja na mwingine yanakuwepo pamoja na kwamba ni wa shida ile *possibility.* Naelewa kabisa kama alivyojibu Mheshimiwa Naibu Waziri wa TAMISEMI. Katika maeneo ya vijijini ambapo ndiyo hayo mazao yapo tungeliweza sana kuyafikia huko. Lakini kwa hali ya fedha na Bajeti ya Serikali tunavyoifahamu wote hatutaweza kufanya hivyo mpaka yale ambayo yamesemwa na Mheshimiwa George Lubeleje na wengine tunayatekeleza.

Mheshimiwa Spika, fedha za matengenezo kwa barabara zetu Bajeti yake kama tunataka kuzitengeneza barabara zote ni shilingi bilioni 221. Sasa hivi Mfuko wa barabara peke yake unaweza kutupatia bilioni 78 huo ndiyo ukweli. Kwa hiyo, nakisi hiyo ni kubwa sana. Sasa muendelee kutushauri ni namna gani tunaweza tukatunisha mfuko huu wa barabara ili tuweze kuzifikia na barabara za vijijini.

Na. 42

**Tatizo la Maji Lulindi**

**MHE. SULEIMAN O. KUMCHAYA** aliuliza:-

Kwa kuwa tatizo la maji ni la nchi nzima; na kwa kuwa, Serikali iko mbioni kulitatua tatizo hilo kadri hali ya uchumi wa nchi itakavyoruhusu; na kwa kuwa, tatizo hilo lipo pia katika Jimbo la Lulindi; na kwa kuwa katika vijiji vya Chiwambo, Mkululu na maeneo mengine kuna vyanzo vya maji ambavyo vinaweza kabisa kupunguza tatizo la maji Jimboni humo pamoja na Wilaya ya Masasi:-

(a) Je, Serikali ina mkakati gani wa kuboresha upatikanaji wa maji katika maeneo hayo ili kupunguza kero hiyo ya maji?

(b) Ili kuthibitisha hayo yaliyosemwa. Je, Serikali iko tayari kufanya ziara katika maeneo hayo?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Suleiman Omari Kumchaya, Mbunge wa Lulindi, lenye vipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Vijiji vya Chiwambo na Mkululu, kama vilivyo vijiji vingi vilivyo katika ukanda wa juu wa Makonde, vinategemea maji kutoka kwenye chemchem nyingi zilizo katika ukanda huo. Kijiji cha Chiwambo kinapata maji kutoka chemchem ya Lulindi - Nanganga ambayo inahudumia zaidi ya vijiji 20 vikiwemo Lulindi, Ndwika, Mkaseka, Luagala, Nanganga, Mvita, Luatala, Mkumbululu, Ng'uni/Ulungu, Namombwe, Mwitika, Mirewe, Ndibwa, Mbuyuni, Mitonji, Chiungutwa, Mitesa, Msanga, Mpilipili, Chiwambo na Namalenga. Kijiji cha Mkululu kinapata maji kutoka chemchem ya Mkululu ambayo inahudumia vijiji vinne vya Mkululu, Miba, Mbugo na Mpopo.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu katika Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji ya mwaka 2006 -2025 imetenga fedha kwa ajili ya vijiji mbalimbali vikiwemo vijiji vilivyotajwa vya Jimbo la Lulindi kama ifuatavyo:- Chiwambo Mradi wa Mtiririko wa Maji ambao utafanyiwa ukarabati umetengewa jumla ya shilingi milioni 168,290,000. Mkululu ambapo mradi wa maji ya bomba umetengwa jumla ya shilingi milioni 120,703,000. Hali kadhalika kuna Mradi wa Lupaso ambapo watajimbiwa kisima kirefu cha ukarabati ambacho ni shilingi milioni 19,500,000.

(b) Mheshimiwa Spika, pamoja na ufuatiliaji wa karibu unaofanywa na Afisa wa Maji wa Bonde la Mto Ruvuma wa utekelezaji wa Mkakati kwa Kitaifa wa Hifadhi ya Ardhi na Vyanzo vya Maji, Serikali itafanya ziara katika maeneo hayo na kusaidiana na Mheshimiwa Mbunge kuhamasisha wananchi kutunza vyanzo vya maji na pia kuhakikisha miradi iliyoombewa fedha inatekelezwa.

**MHE. SULEIMAN O. KUMCHAYA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja dogo la nyongeza. Kwanza, namshukuru Naibu Waziri kwa majibu mazuri. Kwa kuwa tatizo hili la maji katika eneo hili ni la muda mrefu na ameishatamka kwamba fedha zimetengwa. Je, fedha hizo ni kwa mwaka wa fedha ujao?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, fedha hizo ni fedha zinatokana na *Quick Win* ya kipindi cha mwaka huu 2006/2007.

**MHE. RAYNALD A. MROPE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuuliza swali moja la nyongeza.

Pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri ningeomba kufahamu kwamba Serikali ilikuwa na Mpango Kabambe wa kuleta maji Mji wa Masasi kutokana na chanzo cha chemchem Mbwinji. Mwaka uliopita ingawaje upembuzi yakinifu ulishakamilika, lakini maendeleo yake yamekuwa ya kusuasua mno na hatuelewi ni lini mpango huu utaanza. Sasa nataka kuiuliza Serikali. Je, mpango wa kuleta maji ya uhakika Masasi utaanza lini kwa uhakika na utakamilika lini?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba kuna mradi wa Mbwinji. Mradi huo ambao utahudumia Miji miwili, Mji wa Nachingwea ambao uko kilomita 35 kutokea kwenye mradi huo na pia Mji wa Masasi ambao uko kilomita 40 kutokea kwenye mradi huo Lakini mpaka hivi sasa usanifu umefanywa na jumla shilingi bilioni 34.5 ndizo zitatumika kwa ajili ya kutengeneza mradi huo. Fedha kwa ajili ya mradi huo tumeziomba kutoka Shirika la Maendeleo la Waarabu linaloitwa *BADEA* na sasa tunasubiri majibu kutoka huko.

Hali kadhalika pia wakati tukisubiri kama Mheshimiwa Mbunge alivyosema kwamba anataka mambo ya uhakika ni kwamba tuna uhakika na huko, lakini kama itashindikana bado tuna imani kwamba kwa mipango yetu ya baadaye pole pole tutapanga fedha kwa ajili ya mradi huo.

Na. 43

**Ulinzi wa Wavuvi na Mali Zao**

**MHE. MOHAMED H. MNYAA** aliuliza:-

Kwa kuwa Jeshi la Polisi ndilo lenye dhamana ya kulinda usalama wa raia wa Tanzania na mali zao; na kwa kuwa juhudi za Jeshi hilo zinaonekana katika kulinda usalama wa raia wa nchi kavu hadi kwenye vyombo kama magari, kushauri kuweka *'speed governor'* ili kuepuka ajali:-

(a) Je, ni juhudi gani zimechukuliwa na Serikali kulinda usalama wa raia na mali zao hasa wavuvi na wale wanaosafiri kupitia baharini katika mwambao wa Tanga, Bagamoyo, Visiwa vya Unguja , Visiwa vya Pemba, Lindi, Mafia, Mtwara, Ziwa Victoria na kadhalika?

(b) Je, ni ajali ngapi za baharini zimeripotiwa, wangapi waliookolewa na wangapi waliofariki katika kipindi cha mwaka 2001 hadi Mei, 2006?

(c) Je, ni vyombo gani vilivyowekwa na Serikali kuangalia usalama wa baharini na kuokoa wale wanaofikwa na dhoruba au ajali nyingine?

**NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Usalama wa Raia, napenda kumjibu Mheshimiwa Mohamed Habib Mnyaa, Mbunge wa Mkanyageni, swali lake lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, jukumu la msingi la Serikali pamoja na mambo mengine ni kulinda usalama wa raia na mali zao popote walipo. Katika kutekeleza jukumu hilo, kwa upande wa watumiaji wa vyombo vya majini hasa wavuvi Jeshi la Polisi kwa kushirikiana na vyombo vingine vya dola limekuwa likifanya doria na misako ya mara kwa mara katika bahari na maziwa kwa lengo la kudhibiti uhalifu majini.

Jeshi la Polisi kwa kushirikiana na Taasisi nyingine za Serikalil hushiriki katika kuokoa maisha ya wananchi inapotokea maafa katika vyombo vya majini. Aidha, wananchi wanaoishi katika maeneo ya mwambao hupewa elimu ya kufanya shughuli zao katika maeneo salama pamoja na kuhamasisha kutoa taarifa za watu wnaaoshiriki vitendo viovu vinavyohatarisha usalama wao na mali zao.

(b) Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha kuanzia mwaka 2001 hadi Mei, 2006, jumla ya ajali za Baharini na katika Maziwa zilizoripotiwa ni 360 ambapo watu 541 walipoteza maisha na wengine 472 waliokolewa.

(c) Mheshimiwa Spika, vyombo vilivyowekwa na Serikali kuangalia usalama wa majini katika bahari na maziwa kwa ajili ya kuokoa wale wanaofikwa na dhoruba au ajali nyingine ni pamoja na Kikosi cha Wanamaji cha Jeshi la Polisi, Kikosi cha Wanamaji cha Jeshi la Wananchi wa Tanzania (*Navy*), Kikosi cha KMKM, Mamlaka ya udhibiti wa usafiri wa Nchi kavu na majini (SUMATRA), Kikosi cha Zimamoto na Uokoaji *(Fire and Rescue Services*) na Kikosi cha Uokoaji cha Mamlaka ya Bandari. Vyombo hivyo nilivyovitajwa hapo juu vina vitendea kazi mbalimbali zikiwemo boti za doria na vifaa vya uokoaji na kadhalika.

**MHE. MOHAMED H. MNYAA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza. Kwa kuwa taarifa zinapotolewa kwa *Police Marine* au Polisi kuhusu ajali zinazotokea huchukua muda mrefu mno kufuatilia; na kwa kuwa katika Vikosi vyetu vya Ulinzi hasa JWTZ, KMKM, JKU, JKT vinaonyesha ushirikiano mkubwa mno wa kazi, navipongeza.

Lakini kwa kuwa katika bandari zetu mara nyingi Zanzibar, Unguja na Pemba boti hizo za KMKM zinakaa bandarini kwa muda mrefu mara nyingi kusubiri taarifa za magendo ya karafuu. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri atakubaliana na mimi sasa kwa kuonyesha ushirikiano huo huo boti hizo zitumike na *Police Marine* zifanye Kikosi cha *Coast Guard* ili kulinda usalama wa wavuvi ambao wengi wanapotea baharini?

La pili, kwa kuwa sina uhakika *radar* hii iliyonunuliwa kwa mabilioni mengi ya fedha kwamba ina uwezo wa kufanya doria au ulinzi wa meli zinazomwaga uchafu pamoja na wavuvi wanaopata ajali. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri atakubaliana nami

kwamba Serikali imefika muda sasa hivi kununua *radar* maalum au helikopita ya kufanya ulinzi huo kama *radar* hiyo haiwezi kufanya kazi hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA:** Mheshimiwa Spika, kwanza sikubaliani naye kuhusiana na suala kwamba KMKM boti zake ziko pale kwa ajili ya kufuatilia magendo ya karafuu tu. Bali kikosi kile kinashirikiana vizuri sana na Jeshi la Polisi wakati ambapo zinatokea ajali kuwasaidia wananchi mbalimbali na mifano mingi ipo na Mheshimiwa Mohamed Habib Mnyaa anaijua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, aidha, ni kwamba Jeshi Polisi mara linapopata taarifa hushiriki kikamilifu katika suala la uokoaji. Lipo tatizo la wananchi pia kuchelewa kutoa taarifa kwa vyombo husika kwa wakati, ndiyo wakati mwingine huchukua muda mrefu kushughulikia tatizo lenyewe. Lakini taarifa zinapotolewa mapema nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na wananchi wote kwamba hatua za haraka huchukuliwa katika kusaidia kuokoa maisha ya wananchi.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Rada, Rada iliyopo hivi sasa inatosheleza sana kutoa taarifa mbali mbali na kusaidia kuweza kupata habari za kutosha. Kwa hivyo, kwa wakati huu hakuna umuhimu wa kununua Rada nyingine. Lakini, lipo jambo la muhimu kwamba tutakapopata uwezo wa kuweza kununua Helkopta ambayo itasaidia sana wakati inapotokea majanga ya namna hiyo. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niongezee katika jibu zuri la Mheshimiwa Naibu Waziri wa Usalama wa Raia.

Mheshimiwa Spika, kwanza, ningependa kusahihisha kwamba Rada si kazi yake kulinda doria. Rada kazi yake ni kutufahamisha vyombo vinavyoingia au vinavyokaribia katika nchi yetu, ndio kazi yake. Walinzi ni watu wengine kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini la pili; vile vile si sahihi kusema kwamba Rada iliyonunuliwa kwa mabilioni, nataka Bunge lako lifahamu kwamba vyombo vyote vya Serikali au silaha zote za kijeshi ni aghali sana, hakuna chombo rahisi. Hununui Rada kama vile unaenda kununua pikipiki. Kwa hiyo, suala la gharama tuliweke sawa! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo ningependa kusema kwamba kama alivyojibu Mheshimiwa Naibu Waziri, ningependa kuchukua nafasi hii kuwahakikishia Watanzania kwamba, tunadhibiti ulinzi wa mali zetu katika bahari hii ya kwetu na Bahari Kuu. Vyombo tunavyo, msiwe na wasi wasi. *(Makofi)*

**MHE. LUCY F. OWENYA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa Serikali iliweka sheria ya kudhibiti mabasi yaendayo kwa mwendo wa kasi kwa kuweka *Speed Governor*. Lakini, tumeona mbasi yaendayo mkoani bado yanaenda kwa mwendo wa kasi sana. Swali ambalo nataka

kuelewa ni kwamba, Je, Serikali imefuta utumiaji wa vidhibiti mwendo kwenye mabasi haya?

**SPIKA:** Naona hili ni jipya, halihusiani na swali la msingi?

**MHE. MWANAWETU S. ZARAFI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Ahsante pia kwa maelezo ya Mheshimiwa Waziri. Lakini, mimi bado nina swali dogo la kuuliza kwamba ametutajia kuna Jeshi la Maji la Polisi ambalo liafanya kazi ya doria na kulinda usalama wa raia, wavuvi na kadhalika. Lakini vyombo hivi vinaelekea viko sehemu moja.

Je, katika maeneo ambayo hivi vyombo havifiki mfano Mkoa wa Lindi, Mtwara na sehemu zote za Pwani; ni wakati gani hivi vyombo vitakaa pale au vitafika kwa ajili ya doria au kuweza kusaidia kuokoa maisha ya wananchi? Ni mkakati gani ambao Serikali itaweka kwa ajili ya maeneo haya ambayo yako mbali na maeneo ambayo mmeweka hivyo vyombo vya doria?

**NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema katika swali langu la msingi kwamba Jeshi la Polisi hushirikiana na vyombo vingine vya dola. Pale ambapo Jeshi la Polisi halina chombo katika eneo hilo, basi hushirikiana ama na Jeshi la Wananchi wa Tanzania, ama na Mamlaka ya Bandari au chombo kingine chochote cha dola kilichopo hapo kwa nia ile ile ya kuokoa maisha ya wananchi inapotokea ajali. Na uhusiano huo upo wa karibu sana baina ya vyombo vyote vya dola.

Kwa hiyo, naomba kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge, pale ambapo Jeshi la Polisi halina boti la doria, vyombo vingine vya dola husaidia kufanya kazi hiyo.

Na. 44

**Gari – Kituo cha Polisi Mji Mdogo wa Mlimba**

**MHE. CASTOR R. LIGALLAMA** aliuliza:-

Kwa kuwa Mji Mdogo wa Mlimba katika Wilaya ya Kilombero una vijiji saba ambavyo ni Mlimba A, Mlimba B, Matema (km18), Viwanja Sitini (km 6), Msolwa (km 8), Kalengakero (km 6) na Kamwene (km 4); na kwa kuwa vijiji hivyo vina vitongoji 47 na idadi ya watu wasiopungua 25,000 na Stesheni kubwa ya *TAZARA* iliyoajiri wafanyakazi wengi; na kwa kuwa Jeshi la Polisi katika Mji huo halina gari la kuwawezesha kumudu kazi zao kwa ufanisi:-

Je, Serikali inaweza kuwahakikishia wananchi wa Kata ya Mlimba kuwa watapatiwa gari angalau moja katika kituo hicho, ili kuwaondolea adha ya kufuata matukio ya uhalifu kwa kutumia baiskeli?

**NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kumjibu Mheshimiwa Castor R. Ligallama, Mbunge wa Kilombero, swali lake kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua upungufu wa vitendea kazi uliopo katika maeneo mbalimbali nchini, ukiwamo upungufu wa magari kwa vituo mbalimbali vya Polisi nchini. Aidha, kwa kutambua umuhimu wa Mji Mdogo wa Mlimba kuwa na usafiri wa gari kwa ajili ya kuzuia uhalifu, Jeshi la Polisi limeshatoa gari Na.*STJ.974 Land Rover 110* kwa ajili ya kituo cha Polisi Mlimba. Kutokana na hali ya gari hilo Jeshi la Polisi limelazimika kulifanyia matengenezo ili liweze kutoa huduma katika eno hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kuyafanyia matengenezo magari machakavu yaliyopo wakati ikiendelea kuangalia uwezekano wa kupata vitendea kazi awamu kwa awamu kadri hali ya Bajeti ya Serikali itakavyoruhusu. Aidha, nataka kumhakikishia Mheshimiwa Castor Ligallama, kuwa kituo cha Polisi Mlimba ni moja katika vituo ambavyo vitapewa upendeleo maalum mara tutakapopata magari mapya kwa ajili ya vituo vya Polisi nchini. Aidha, nichukue fursa hii kumshukuru sana Mheshimiwa Rais na Amiri Jeshi Mkuu kwa jitihada zake kubwa anazochukua za kuvisaidia Vikosi vya Ulinzi na Usalama Tanzania. Hivi karibuni tu alitusaidia kupata magari 40 na pikipiki 177 kutoka Ufalme wa Dubai. Namshukuru sana Mheshimiwa Rais na mtoaji wa msaada huo Shekh Rashid Bin Mohamed Makhtum, kwa Msaada huo. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. CASTOR R. LIGALLAMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri, naishukuru Serikali kwa ahadi nzuri. Lakini, Wilaya yangu ya Kilombero inapokea Watanzania wengi, siwezi kuwaita wageni, Watanzania wengi wanakuja kwa shughuli za kilimo; na kwa vile wengi wao hatujui historia zao kule wanakotoka, yametokea matukio mengi ya uhalifu katika maeneo yetu. Je, pamoja na ahadi nzuri aliyotoa, Mheshimiwa Waziri atakuwa tayari kutuahidi kutoa nyenzo kama hizo katika Tarafa za Mang’ula, Kidatu na Mgeta?

**NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA:** Mheshimiwa Spika, kwanza napenda nipokee shukrani za Mheshimiwa Ligallama. Aidha, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Ligallama kwamba Jeshi la Polisi siku zote litakuwa tayari kushirikiana na wananchi wa maeneo hayo kuhakikisha kwamba ulinzi na usalama wa wananchi hao siku zote unadumishwa. Aidha, Jeshi la Polisi litaendelea kuimarisha ulinzi kwa Tanzania nzima ili kuhakikisha kwamba maisha ya wananchi wetu na mali zao yapo salama.

Na. 45

**Uchakavu wa Reli na Treni**

**MHE. LUCAS L. SELELII** aliuliza:-

Kwa kuwa treni ni usafiri pekee unaotumiwa kwa wakazi wa Mikoa ya Magharibi na Kanda ya Ziwa; na kwa kuwa reli na treni vyote vimechakaa:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kutengeneza reli ili iwe ya kisasa?

(b) Kama reli itatengenezwa, Serikali itakuwa tayari kununua injini na mabehewa mapya?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MAUA A. DAFTARI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, niruhusu nimwombe Mwandishi wa Habari, Ndugu Beatrice Bandawe wa Gazeti la Nipashe, awe makini katika kuandika yale ambayo yanazungumzwa na kujadiliwa ndani ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Lucas L. Selelii, Mbunge wa Nzega, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Serikali iko katika huduma za mwisho za kukodisha huduma za uchukuzi na usafiri wa Shirika la Reli Tanzania *(TRC)*. Kwa mpango huu, Mkodishaji kwa kushirikiana na Serikali ataboresha njia ya urefu wa kilomita 648 ifikie uzito wa ratili 120 kwa yadi ili kuongezea uwezo wa kubeba mizigo mizito zaidi na kuongeza kasi ya mwendo wa treni na kupunguza muda wa safari ukilinganisha na hali ilivyo hivi sasa.

Serikali ya Awamu ya Nne inatarajia kuboresha njia nzima ya Reli ya Kati hadi Kigoma na Mwanza ili ifikie uzito wa ratili 120 kwa yadi na kuna mpango wa muda mrefu wa kupanua njia ya Reli kutoka mita moja hadi kufikia kiwango cha *standard gauge* yaani mita 1.435 ifikapo mwaka 2025. Upana huu utawezesha treni ya abiria kwenda mwendo wa kasi hadi kufikia kilomita 200 kwa saa.

(b) Mheshimiwa Spika, ukarabati na utanuzi wa mabehewa na vichwa vya treni utakuwa ni jukumu mojawapo la Mkodishaji kufuatana na mahitaji yatakavyokuwa yanajitokeza.

**MHE. LUCAS L. SELELII:** Mheshimiwa Spika, nina maswali mawili ya nyongeza. La kwanza, katika majibu ya Mheshimiwa Waziri au ya Serikali ambayo hayaonyeshi ni lini Mkodishaji na Serikali wana mpango wa muda mfupi, walichokionyesha hapa ni mpango wa muda mrefu wa 2025. Je, hao wakaazi wa Kanda ya Magharibi, Mikoa ya Magharibi pamoja na Kanda ya Ziwa, wakae wakijua ni lini watakuwa na uhakika wa usafiri wa treni kwa sababu hata barabara sasa hivi hawana? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, usafiri wa treni ni kuanzia Mwanza , Kigoma mpaka Dar es salaam. Lakini kwa sasa wasafirishaji wa mizigo na abiria wanahangaika kushuka hapa Dodoma. Je, ni lini treni na mizigo itafika hadi Dar es salaam?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MAUA A. DAFTARI):** Mheshimiwa Spika, hata hivi sasa hatua zimechukuliwa na tayari tulishaagiza vipuri na vipuri vimefika, mataruma na reli zake kwa ajili ya ukarabati wa njia kuanzia Kitinku hadi Makutopora, Itigi hadi Tura. Na tunategemea tutapata *fish plates* mwezi wa Juni ili kazi ianze. Napenda nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, si nia ya Serikali hata mara moja kuona wananchi wanamalizia safari yao Dar es salaam.

Lakini ni kutokana na uchache wa injini na uchache wa mabehewa ndio uliotufikisha hapa. Lakini, tunategemea shughuli hizi za ukodishwaji zitakapokamilika, Mwekezaji ili afanye biashara na apate faida, atalazimika kufanya shughuli za kuboresha huduma hizo za mabehewa na injini zake.

**MHE. MHONGA S. RUHWANYA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Kila mara Wabunge wa Kanda ya Magharibi tunapouliza swali hili tunaambiwa kwamba Serikali ipo katika hatua ya mwisho. Je, ni lini hiyo hatua ya mwisho itafikiwa? Hatujapewa wakati kamili ni lini hatua ya mwisho itafikiwa! *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MAUA A. DAFTARI):** Mheshimiwa Spika, ni kweli tunajibu, hatujamaliza majadiliano. Majadiliano yatakapomalizika na tutaingia mikataba na shughuli zikaanza, tutakuwa katika *position* nzuri ya kusema sasa tutamaliza masuala haya ya Reli ya Kati.

Na. 46

**Ujenzi wa Barabara ya Kutoka Ng'wigumbi – Maswa**

**MHE. LUCY T. MAYENGA (K.n.y. MHE. FRED M. TUNGU)** aliuliza:-

Kwa kuwa moja ya kichocheo kikubwa cha maendeleo mahali popote duniani ni ubora na uimara wa miundombinu hasa barabara; na kwa kuwa Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2005 kwa kulitambua hilo hasa katika kuchochea maendeleo katika Wilaya ya Kishapu, kiliahidi kujenga barabara ya kutoka Ng'wigumbi hadi Maswa kwa kiwango cha lami; na kwa kuwa, kwa dhamira hiyo hiyo, wakati wa sherehe za Wafanyakazi mwaka 2006, Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete, aliahidi kujenga barabara ya kutoka Kolandoto hadi Meatu kupitia Mhunze – Makao Makuu ya Wilaya ya Kishapu kwa kiwango cha lami:-

Je, Serikali imefikia hatua gani katika utekelezaji wa ahadi hizo?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Fred M. Tungu, Mbunge wa Kishapu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli Ilani ya Uchaguzi ya Chama Tawala (CCM) ya mwaka 2005 kiliagiza kufanyika kwa upembuzi yakinifu na usanifu kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya Maganzo – Maswa – Bariadi – Mkula hadi Lamadi. Katika mwaka huu wa fedha 2006/2007 Wizara yangu itakamilisha upembuzi yakinifu barabara ya Ng'wigumbi – Maswa – Bariadi hadi Sapiwi (Kilomita 171). Kazi hiyo itagharimu jumla ya shilingi milioni 215.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2007/2008 Serikali itaendelea kutenga fedha kwa ajili ya kuifanyia usanifu wa kina na kuandaa makabrasha ya zabuni ya ujenzi wa barabara hiyo kwa kiwango cha lami kadri Bajeti itakavyoruhusu.

Mheshimiwa Spika, ili kuanza kutimiza ahadi za Mheshimiwa Rais, Wizara yangu itajitahidi kutenga fedha kadri Bajeti itakavyoruhusu katika mwaka wa fedha 2007/2008 ili kuifanyia upembuzi yakinifu barabara ya Kolandoto - Mhunze – Lalago Mwanhuzi (Kilomita 117).

**MHE. LUCY T. MAYENGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri, napenda kuuliza swali dogo la nyongeza kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa ahadi hii ya ujenzi wa barabara hizi ambayo ilitolewa na Mheshimiwa Rais wakati wa kipindi cha Kampeni na katika sherehe za Mei Mosi, ninamwomba Mheshimiwa Waziri. Je, Serikali iko tayari sasa kutoa ratiba ya utekelezaji wa ahadi hizi?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA):** Mheshimiwa Spika, kama anaulizia ujumla kwa maana ya ahadi zote za Mheshimiwa Rais, hizi ratiba yake ni miaka mitano kwa maana kwamba Ilani ya Uchaguzi ya miaka mitano kuanzia mwaka 2005 – 2010 na zinategemea Bajeti ya kila mwaka. Kwa hiyo, kila mwaka Serikali itakuwa inaeleza itatekeleza nini katika mwaka huo.

Mheshimiwa Spika, lakini kama ni swali ambalo ameuliza Mheshimiwa Mpendazoe, nimeeleza ratiba nzuri sana ambayo sina sababu ya kuirudia.

Na. 47

**Aina za Lami katika Barabara zetu**

**MHE. RAYNALD A. MROPE** aliuliza:-

Kwa kuwa zipo aina mbali mbali za lami nchini kiasi kwamba haieleweki ni aina gani inayofaa kwa aina gani ya barabara:-

(a) Je, kuna utaratibu gani maalum unaotumika kuweka viwango vya aina ya lami inayowekwa kwenye barabara za Kitaifa/Kimkoa na zile za Halmashauri?

(b) Je, Wakandarasi nao wanapewa utaratibu huo na kupewa adhabu pale inapobainika kwamba hawakufuata uhakiki maalum na matokeo yake ni yapi hasa katika barabara ya Kibiti – Lindi – Mingoyo?

(c) Je, kwa nini kuna matabaka tofauti ya lami kati ya Mingoyo – Kibiti?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Raynald A. Mrope, Mbunge wa Masasi, napenda kutoa maelezo ya jumla kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, lengo kubwa la kujenga barabara kwa kiwango cha lami ni kuwezesha zidumu kwa muda mrefu ikilinganishwa na barabara za changarawe au udongo. Ujenzi huu huhifadhi matabaka ya chini ya barabara *(Pavement Structural Layers)* ili yasidhoofishwe na athari za maji pamoja na kusagika kutokana na magurudumu ya magari.

Aidha barabara za lami huzuia uharibifu wa tabaka la juu *(Wearing Course)* unaosababishwa na magari yanayotumia barabara hizo na hivyo kuzifanya zidumu na kurahisisha usafiri na usafirishaji.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa tabaka la juu la lami umegawanyika katika mafungu makubwa matatu:-

Aina ya kwanza ni *Otta Seal*. Hii ni lami nyepesi ambayo humwagwa juu ya tabaka la changarawe hususan katika barabara zinzaotumiwa na magari machache. Aina ya pili ni *Surface Dressing*. Hii ni lami nyepesi ambayo humwagwa barabarani juu ya tabaka zilizoandaliwa na juu yake kokoto husambazwa na kushindiliwa.

Aina ya tatu ni *Asphalt Concrete*. Katika ujenzi huu lami huchanganywa na kokoto kwenye mtambo maalum *(Asphalt Plant)* na humwagwa barabarani kwa unene maalum na kushindiliwa.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naomba kujibu swali la Mheshimiwa Raynald A. Mrope, Mbunge wa Masasi, kama ifuatavyo :-

(a) Mheshimiwa Spika, utaratibu unaotumika kuamua kiwango na aina ya lami itakayotumika katika barabara mbali mbali unazingatia vigezo vifuatavyo :- Kwanza, ni idadi na uzito wa magari yanayotarajiwa kutumia barabara husika. Pili, ni kiasi cha fedha zilizotengwa kwa ajili ya kugharamia ujenzi wa barabara husika.

(b) Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa kuwa Makandarasi wanapewa michoro ambayo wanalazimika kuifuata wakati wa ujenzi. Michoro hii huwa ni sehemu ya mkataba. Aidha, ni kawaida ujenzi husika kusimamiwa na Mkandarasi Mshauri ambaye jukumu lake kubwa ni kuhakikisha kuwa Mkandarasi anazingatia viwango vilivyoainishwa katika michoro ya mkataba.

Mheshimiwa Spika, pale inapogundulika kuwa Mkandarasi amejenga tofauti na viwango vilivyoainishwa katika mkataba, hatua mbali mbali huchukuliwa dhidi yake. Hatua hizi zimetamkwa bayana katika mkataba husika.

(c) Mheshimiwa Spika, kwa miradi ya barabara inayoendelea sasa kati ya Dar es salaam hadi Mingoyo, ni tabaka la aina moja tu ya lami inayotumika ambayo ni *Surface Dressing*.

**MHE. RAYNALD A. MROPE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kujibu vizuri maswali yangu. Lakini ningetaka kuuliza; kama yeye amepita barabara kati ya Mtwara mpaka Masasi sehemu za Mkwaya – Mingoyo na sehemu ya Chipite – Nanganga. Pale utaona kwamba lami imenyunyiziwa juu juu. Magari yakipita, basi kokoto zote zinaangukia pembeni mwa barabara.

Sasa, mtindo huu ndio mtindo gani uwekaji lami? Anaweza kuniambia kwamba lami ya namna hiyo ndiyo inayostahili katika barabara kuu kama ya Mtwara kwenda Masasi ?

Mheshimiwa Spika, la pili ni kwamba hata Waheshimiwa Wabunge ni mashahidi, utakuta sehemu mbali mbali katika barabara zetu kunakuwa na lami ya ajabu kabisa, unakuta inadidimia yenyewe. Kwa mfano pale Ruvu, lami inadidimia. Na si hivyo tu, kuna sehemu nyingine lami yake ikinyesha mvua tu, basi inateleza au wakati wa joto kali, inateleza. Sasa mtindo huu ni mtindo gani kwa Tanzania hii na inaashiria ulegevu katika usimamizi, uzembe na kadhalika au hatujui namna ya kutengeneza lami ?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA)**: Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba nimetembelea barabara ya kutoka

Mtwara mpaka Masasi. Lakini anachozungumza nadhani ni *repairs* ambazo zinafanyika baada ya ile barabara kuwa imejengwa zamani kwa kiwango cha *surface dressing*.

Kwa hiyo, ni kwamba wakati ambapo kutokana na ufinyu wa Bajeti, ingetakiwa kwa kweli kwa sasa barabara ile tuiondoe yote na tuijenge upya.Lakini kutokana na ukosefu wa fedha tumekuwa tukiifanyia ukarabati maeneo korofi kwa kuweka hiyo *layer* ambayo ni kama ile niliyosema ya *otta seal* na kushindilia kidogo kwa maana ya kuweka changarawe juu na baada ya muda magari yakiishakanyaga kwa muda mrefu, basi huwa inatulia. Lakini, kwa kweli ni kutokana na hali halisi na Bajeti ambayo ipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini kutokana na swali lake la pili hilo alilouliza kwamba maeneo fulani unaona barabara zinaharibika. Kama nilivyosema, kiwango cha barabara cha kutengeneza au aina za barabara ni hizo tatu nilizotaja. Lakini, inategemea sana hali halisi ya eneo husika. Kwa mfano, ukiona barabara ya Nzega – Tinde kwenda Shinyanga, ile kutokana na udongo wa eneo lile ilibidi kwa kweli wale wenzetu Wakandarasi kutoka Afrika Kusini kuondoa udongo wote kutoka chini na ile ilikuwa gharama kubwa.

Mheshimiwa Spika, sasa pale ambapo gharama haitoshelezi kufanya hayo hata kama udongo hauwezi kuhimili aina hiyo ya barabara na fedha ni chache, basi hufanyika utaratibu wa kawaida wa kujenga barabara kama tunavyofanya. Na kwa kweli unakuta baada ya miaka michache, barabara ile inakuwa na athari hizo alizozitaja na wala si kwamba kila wakati ni kutokana na ubovu wa mkandarasi, ila kutokana na hali halisi ya eneo lenyewe na bajeti iliyokuwepo. Kinachotakiwa kufanywa sasa kutokana na hali hiyo ni kila baada ya muda, basi kurekebisha maeneo hayo kwa kuweza kuondoa ile lami na kuweka nyingine kadri fedha zinavyoruhusu.

**MHE. DR. CHRISANT M. MZINDAKAYA:** Mheshimiwa Spika, kutokana na uzoefu ambao tumeuona sisi wote na mwenyewe Waziri amethibitisha kwa majibu yake. Atakubaliana na mimi kwamba usimamizi wa ujenzi wa barabara za lami si makini sana na ndio maana barabara zinapotengenezwa hazizingatii maeneo na ardhi ya mahala ambapo barabara inatengenezwa ?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA):** Mheshimiwa Spika, kwa kweli tatizo kubwa ni uwezo wa kutengeneza barabara kwa kiwango kinacholingana na hali halisi ya eneo lenyewe. Lakini, inawezekana kweli kwamba kuna wakati usimamizi unakuwa mbovu. Lakini nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, wakati tunateua Msimamizi wa kusimamia barabara *(Consultant Engineer)* tunakuwa makini sana na tunachagua *Consultant* ambaye tuna hakika atasimamia vizuri.

Kwa hiyo, hatuamini kwamba tunaweza tukachagua msimamizi ambaye atakuwa mbabaishaji. Lakini inapotokea hivyo na tukawa na taarifa, basi huchukua hatua zinazofaa. Lakini la muhimu ni kwamba maeneo yanatofautiana kutegemea na ardhi husika na kama ingekuwa kwamba basi tuweke fedha za kuhakikisha kwamba kila eneo, kwa mfano kama una *black cotton soil*, basi uondoe ardhi yote ile, gharama zinaweza kuwa kubwa sana tukashindwa kujenga barabara kwa kiwango tunachotegemea.

Na. 48

**Makampuni Yanayoshughulikia Utafiti wa Madini**

**MHE. ESTHER K. NYAWAZWA** aliuliza :-

Kwa kuwa, wawekezaji wa Sekta ya Madini walioko Nyarugusu, *East Africa Mines* na *IAM Gold Mining* ni makampuni yanayoshughulika na utafiti wa madini maeneo hayo; na kwa kuwa makampuni hayo hupewa *Prospecting License* toka Wizarani; na kwa kuwa hufika na kuwanyanyasa wananchi wa maeneo hayo:-

(a) Je, Serikali haioni umuhimu wa kuwaandaa kwanza wananchi kwa kuwapa elimu ya kutosha kabla ya kutoa *Prospecting Licence*?

(b) Je, utafiti huo hufanyika kwa muda gani na masharti yake ni yapi yanayowazuia wawekezaji hao kubadilishana hovyo bila utaratibu?

(c) Je, fidia wakati wa utafiti inalipwa na nani?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Esther K. Nyawazwa, Mbunge wa Viti Maalum, naomba kutoa maelezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, Kampuni ya *East Africa Mines Limited* imekuwa ikifanya utafiti wa madini katika maeneo kadhaa yanayozunguka Ziwa Viktoria yakiwemo maeneo ya Nyarugusu baada ya kupewa leseni za utafutaji madini kwa mujibu wa Sheria ya Madini ya mwaka 1998. Mwezi Machi, 2006, Kampuni hiyo ilibadilisha jina na sasa inaitwa *IAM GOLD Tanzania Limited*.

Mheshimiwa Spika, kampuni yoyote inapopewa leseni ya madini hutakiwa kuendesha shughuli zake kwa kuzingatia sheria zilizopo sambamba na kuheshimu wananchi wanaoishi katika maeneo wanakofanyia shughuli zao.

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa maelezo hayo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Esther K. Nyawazwa, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa elimu ya mambo ya madini kwa wananchi walio katika maeneo yenye madini ni muhimu sana.

Mheshimiwa Spika, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge na Bunge lako tukufu kuwa Wizara yangu hutoa elimu kwa wananchi wa maeneo yenye madini kwa njia ya mafunzo, warsha na semina. Mafunzo hayo hutolewa na wataalam wa Wizara kwa

kushirikiana na taasisi zingine kama vile Shirika la Viwanda Kuhudumia Vidogo Vidogo *(SIDO)*.

Vile vile wataalam walioko katika ofisi za madini zilizoko katika baadhi ya Mikoa na Wilaya wamekuwa wakitoa elimu ya ugani *(extension services)* kwa wananchi wa maeneo yenye madini. Lengo la mafunzo hayo ni kuwawezesha wananchi kuelewa haki, wajibu na mipaka ya leseni katika maeneo yao.

Mheshimiwa Spika, ili kuelimisha Umma wa Watanzania, Wizara yangu imekuwa ikichapisha vijarida na vipeperushi na kuvisambaza kwa wananchi kupitia ofisi zake za Mikoani. Aidha, Wizara yangu iko mbioni kufufua vipindi vya elimu kwa Umma kwa njia ya Redio kama ilivyokuwa katika miaka ya 2003 – 2004 na tuna mpango wa kuanzisha vipindi vya elimu kwa Umma kwa njia ya Televisheni.

(b) Mheshimiwa Spika, leseni za utafutaji mkubwa wa madini kwa mara ya kwanza hutolewa kwa vipindi vya miaka miwili miwili au mitatu kutegemeana na hatua ya utafutaji iliyofikiwa na aina ya madini yanayotafutwa. Leseni ya awa li ya utafutaji wa madini *(Prospecting Licence with Reconnaissance Period)* hutolewa kwa miaka miwili ili kuwezesha mwombaji kufanya utafiti wa awali wa kubaini eneo la kuomba leseni ya utafutaji madini *(Prospecting Licence)*. Leseni ya utafutaji madini wa awali haihuishwi.

Mwombaji wa *prospecting license* halazimiki kuanza na leseni ya utafutaji wa awali bali anaweza kuomba moja kwa moja leseni ya utafutaji madini yaani *prospecting license* ambayo inatolewa kwa kipindi cha awali cha miaka mitatu. Endapo mwekezaji atakuwa hajakamilisha shughuli zake za utafutaji madini, leseni hii huweza kuhuishwa kwa vipindi vingine viwili vya miaka miwili miwili kwa sharti la kupunguza nusu ya eneo alilokuwa akilimiliki kila mara anapohuisha leseni yake.

Mheshimiwa Spika, sheria ya madini inamruhusu mmiliki kuhamisha au kuuza hisa zake zote au baadhi kwa kampuni yoyote au mtu yeyote mwenye sifa kisheria kumilikishwa leseni ya madini.

(c) Mheshimiwa Spika, fidia ya mali yoyote inayoathirika kutokana na shughuli zozote za madini zikiwemo za utafutaji wa madini hutakiwa kulipwa na mmiliki wa leseni.

**MHE. ESTHER K. NYAWAZWA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri, katika jibu lake la msingi amekiri kwamba kampuni hii iko katika Kanda ya Ziwa na imekuwa ikiwanyanyasa wananchi walioko katika Jimbo la Busanda Nyarugusu na wananchi walioko katika Jimbo la Busega kwa Dr. Chegeni wananyanyasika na amekiri kabisa kwamba hii kampuni imemaliza muda wake ikabadilishana na mtu mwingine lakini bado anaendelea kuwanyanyasa wananchi wa eneo lile.

(a) Mheshimiwa Spika, sasa naomba Mheshimiwa Naibu Waziri anieleze je, Serikali, inatoa kauli gani kwa wananchi wanaokutwa katika maeneo yale ambayo

wanafanya utafiti na wananyanyasika pasipo makubaliano yoyote na haya makampuni na wala hawapati fidia yoyote katika maeneo hayo?

(b) Kwa kuwa hii kampuni imeendelea kubadilishana na muda wa utafiti ni wa muda mrefu sana miaka miwili. Je, Mheshimiwa Waziri, unaweza kukubaliana na ombi langu, tukaongozana wewe pamoja na Wabunge wa majimbo hayo mawili tajwa ukawasikiliza wananchi wanavyonyanyaswa na hayo makampuni katika eneo hilo? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kwanza, niseme tu kwamba kuhusu suala la kwanza kama nilivyoeleza kwenye majibu ya msingi ni kwamba si kweli kwamba tumekiri kwamba makampuni haya yamekuwa yakiwanyanyasa. Nadhani kumbukumbu za *Hansard* zinaonyesha sijakiri bali tulikuwa tunaelezea utaratibu umekuwa ukitumika. Pamoja na hayo napenda kusema kwamba taratibu zinaendelea kufuatwa na kila inapojitokeza kwamba kuna mgogoro sisi Serikali kwa kushirikiana na wawekezaji pamoja na mamlaka zingine zinazohusika tunahakikisha kwamba utaratibu unafuatwa na kwenye migogoro tunaingilia kati kwa kweli kuutatua.

Mheshimiwa Spika, kwa hili suala la fidia naomba kumuarifu Mheshimiwa Mbunge na Bunge lako tukufu kwamba tunaendelea kulifanyia kazi inapoonekana kwamba kuna mgogoro ambao kwa kweli upande mmojawapo wa wahusika unanyanyasika ama unapoteza haki yake sheria inachukua mkono wake. Kwa hiyo, tunamhakikishia Mheshimiwa Mbunge, kwamba tuko makini na tunaendelea kuhahakikisha kwamba tutakuwa makini kwa siku zijazo kwa maslahi ya taifa letu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, la pili, tuko tayari kuandamana na Mheshimiwa Mbunge, lakini pia na Wabunge wengine ambao wataona inapendekeza kufanya hivyo na tumekuwa tukifanya hivyo na Mheshimiwa Waziri wangu na mimi mwenyewe tumekuwa tukishirikiana na Waheshimiwa Wabunge, akiwemo Mheshimiwa Chacha Wangwe, tarehe 19 tulikuwa naye Mara na Mheshimiwa Waziri hivi karibuni alikuwa Geita kusuluhisha akishirikiana na Mheshimiwa Mabina, Mbunge wa Geita. Kwa hiyo, suala hili tuko tayari na tutaweza kufanya hivyo kwa maslahi yetu. (*Makofi*)

**MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri katika maelezo yake amesema kwamba wanatoa elimu kwa wana vijiji kwa sehemu hizo ambazo zinatolewa *prospective license* pamoja na vipeperushi. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa nini mpaka hivi leo kuna malalamiko mengi sana ya wana vijiji hasa kwa mfano jirani zako Nyakabale, *Geita Hill* na Nyamarembo kule Geita?

Je, Mheshimiwa Naibu Waziri, utakubaliana na mimi kama Waziri kivuli wa Nishati na Madini utakuwa tayari tufanye safari na mimi twende Geita tuone watu wanavyonyanyaswa pamoja na maji machafu? (*Makofi*)

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, naomba kumjibu Mheshimiwa Mnyaa baada ya majibu mazuri kutoka kwa Naibu Waziri. Nataka kusema kwamba kauli hii ya kusema wananchi wananyanyaswa naona si sahihi. Nataka niseme si sahihi kwa sababu ya mambo mawili yafuatayo:

Mheshimiwa Naibu Waziri, alivyozungumza tutofautishe vitu viwili *prospecting license* na *mining license. Prospecting license* mtu anapoipata siyo maana kwamba watu wanaondoka kwenye maeneo hayo mwenyewe bado anatafuta tu anachimba mashimo hapa na pale. Sasa kama shimo atalichimba kwenye shamba lako hapo wewe ndiyo utahitaji fidia kwa sababu mwenyewe bado anatafuta. Mpaka hapo atakapopata *mining license* ndiyo inaweza ikakumba watu walio wengi wakataka kuhamishwa.

Tunajua matatizo yaliyopo sasa hivi yako katika sehemu mbalimbali, kwanza kuna watu kutokubali kufanyiwa tathimini ya viwanja vyao. Kuna watu wengine wanapinga ile fidia inayotolewa. Kuna watu wengine wakijua tu kwamba kuna eneo ambalo lina uwezekano wa kuwekewa fidia wanaanza ku-*rush* kukimbilia kwenye eneo hilo.

Kwa hiyo, matatizo yako ya aina mbalimbali ndiyo sababu tumesema kwamba kila panapotokea matatizo, mimi Waziri, Naibu Waziri, Kamishina wa Madini pamoja na Wabunge husika tutakwenda kwenye maeneo yao, tutakutana na wananchi kusudi kubaini tatizo liko upande gani ili tuweze kulitatua kwa sababu matatizo yote hayafanani. (*Makofi*)

Na. 49

**Zao la Kahawa**

**MHE. GODFREY W. ZAMBI** aliuliza:-

Kwa kuwa mapema mwaka 2006 Waziri Mkuu, alikutana na wadau wa mazao mbalimbali nchini ikiwa ni pamoja na zao la kahawa ambalo ndilo zao kuu kwa wananchi wengi wa Jimbo la Mbozi Mashariki na kwa kuwa katika Mkutano wake na wadau wa zao la kahawa Waziri Mkuu alitangaza kuondolewa kwa baadhi ya kodi zilizokuwa zinatozwa kwa zao hili:-

(a) Je, ni kodi ngapi zilizotolewa na kodi ngapi mkulima wa zao hilo anastahili kukatwa?

(b) Kwa kuwa kumekuwa na malalamiko mengi sana kutoka kwa wakulima kwamba wanakatwa kodi nyingi sana kwenye zao la kahawa. Je, Serikali imechukua hatua gani za kuwaelimisha wakulima kuhusu aina za kodi wanazokatwa na faida zake kwa maendeleo ya taifa hili?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA (MHE. DAVID M. DAVID)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Godfrey Zambi, Mbunge wa Mbozi Mashariki, lenye lenye sehemu (a) na (b) napenda kutoa maelezo yafuatayo:-

Ni kweli kwamba kati ya tarehe 12 na 18 Mwezi Mei, 2006 Mheshimiwa Waziri Mkuu, alifanya mikutano na wadau wa mazao ya korosho, tumbaku, pamba na kahawa. Lengo la mikutano hiyo lilikuwa ni kutoa fursa kwa wadau kujadili fursa na changamoto mbalimbali wanazokabiliana nazo katika uzalishaji wa mazao hayo. Katika mikutano hiyo pamoja na mambo mengine, suala la ushuru uliokuwa unatozwa na Bodi za Mazao lilijadiliwa.

Baada ya maelezo hayo sasa napenda kujibu swali la Mheshimiwa Godfrey W. Zambi, Mbunge wa Mbozi Mashariki, kama ifuatavyo:-

(a) Ushuru uliofutwa kwa zao la kahawa kuanzia Julai, 2006 ni kama ifuatavyo:-

(1) Ushuru wa Bodi *(Tanzania Coffee Board Levy);*
(2) Ushuru wa aina zote za leseni za kahawa; na
(3) Ushuru wa *VAT* wa asilimia 20 kwa mauzo au manunuzi ya kahawa.

Mheshimiwa Spika, aidha, mkulima anastahili kukatwa ushuru kwa ajili ya kugharimia utafiti kutokana na makubaliano ya wakulima ambao wanachangaia uendeshaji wa *TACRI*. Pia wakulima hulipia gharama za viwanda vya kukoboa kahawa. Mbali na gharama hizo Halmashauri za Wilaya hutoza ushuru *produce cess* ambayo haizidi asilimia tano ya bei ya mkulima. Sera ya Serikali ni kumpunguzia mkulima makato ili kumwongezea kipato kinachotokana na mazao yake. Hata hivyo inapobidi mkulima huchangia shughuli nyingine za maendeleo, inabidi wakulima wenyewe washirikishwe na kuamua kwa hiari ni shughuli gani za maendeleo na makato kiasi gani yakatwe.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kutoa elimu na kuwaarifu wakulima kwa njia mbalimbali ikiwa ni pamoja na kipindi cha redio cha kahawa ni mali kinachotayarishwa na Bodi ya Kahawa, kuhusu uamuzi wa Serikali wa kuondoa kodi zilizotajwa hapo juu. Hili ni zoezi linaloendelea.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri naomba kuuliza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kutokana na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, vyovyote vile kodi ambazo mkulima anakatwa kwenye zao la kahawa ni tatu ingawa sina hakika na hii ya ugharimiaji wa *TACRI* kwa sababu nadhani yenyewe Mheshimiwa Waziri Mkuu, aliitamka sina hakika lakini kama ndiyo hivyo bado ziko tatu. Katika hali ya kawaida tatu

kwa mazao mbalimbali ya wakulima bado ni nyingi sana ni mzigo mkubwa kwa wananchi hawa ambao wanalima zao hili la kahawa pengine na mazao mengine.

(a) Je, Serikali inasema nini juu ya hilo?

(b) Mheshimiwa Naibu Waziri anasema kwamba zoezi hili la kuondoa kodi ya zao la kahawa ni zoezi linaloendelea. Linaendelea mpaka lini kwa sababu Waziri Mkuu alishatamka zile zimefutwa au zimeondolewa sasa anasema bado ni zoezi linaloendelea wananchi waendelee kutumaini mpaka lini kwamba hizo kodi nyingine zitaondolewa? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA (MHE. DAVID M. DAVID):** Mheshimiwa Spika, kwanza niseme kwamba kodi zipo za aina mbili, zipo zile za hiari, lakini zipo zile za kisheria kwa mfano kuna *produce cese* ambayo inakatwa asilimia zisizozidi tano ile ni kodi ya kisheria. Nyingine ni gharama za kukoboa kahawa. Ile lazima wakatwe na zinatofautiana sehemu hadi sehemu. Kwa mfano, Mbozi kuna kiwanda cha Mlowo chenyewe kinakata shilingi 58 kwa kilo. Kuna kiwanda kingine kinaitwa *CT Coffee* chenyewe kinakata shilingi 62 kwa kilo. Lazima kahawa ikobolewe. Lakini vile vile makato mengine ni kugharamia upakiaji wa kahawa kwa ajili ya *export* yaani kusafirisha nchi nje ya nchi. Mkulima anagharamia shilingi 1,680 kwa gunia la kilo 60 na tunaelewa kabisa soko la nje lazima uwe na *package* yaani hupakiwa vizuri ile kahawa kusudi iweze kununuliwa maana *packaging* ni muhimu katika soko.

Lakini vile vile kwa kuwa sasa hivi tuna Kituo cha *TACRI* ambacho kinazalisha miche. Kwanza inazalishwa kwa muda mfupi lakini vile vile inazaa sana halafu iko *resistance* kwa magonjwa basi wanazalisha miche hiyo na wanahitaji *support*. Kwa hiyo, baada ya bei mnadani Mkulima hukatwa asilimia 0.75 baada ya kwamba bei ya mnadani imetolewa pale Moshi. Ni hizo nne ambazo nimezitaja.

Sasa nasema zoezi hili linaendelea tutaendelea kutathimini ni vipi tunaweza tukaipunguza lakini kwa sasa hivi zote zina umuhimu wake. Huwezi ukaondoa *cess* ya maendeleo, huwezi kusema kwamba hawatanunua magunia kwa ajili ya ku-*pack*. Huwezi kusema kwamba watasafirisha ile kahawa bila kuikoboa.

Na. 50

**Ahadi ya Kuchimba Bwawa Ussongwangala**

**MHE. TEDDY KASELLA – BANTU** aliuliza:-

Kwa kuwa kuna ahadi ya siku nyingi ya kuchimba bwana kubwa kama la Mwanzugi, Igunga katika Mbuga ya Ussongwanhala Kata ya Uduka na Kahama ya Nhalanga iliyotolewa na aliyekuwa Waziri Mkuu wa Zamani Hayati Edward Sokoine,

kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji na kwa kuwa ahadi hiyo ni ya Serikali na kwa kuwa, kilimo cha umwagiliaji ndicho kinafaa kuwaondolea wananchi kwenye umaskini uliokithiri:-

Je, Serikali itatekeleza ahadi hiyo lini kama ilisahaulika, nakumbushia kwa njia hii?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA (MHE. CHRISTOPHER K. CHIZA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Teddy Louise Kasella-Bantu, Mbunge wa Bukene, napenda kutoa maelezo mafupi kama ifuavyo:-

Mkakati wa kuendeleza kilimo cha umwagiliaji kama ulivyoelezwa katika Mpango Kabambe wa Kilimo cha Umwagiliaji 2002 na programu ya kuendeleza sekta ya kilimo 2004 unaweka vipaumbele kama ifuatavyo:-

(i) Kukarabati skimu za umwagiliaji za zamani zilizochakaa hasa zile zinazopata maji kwa *gravity*.

(ii) Kuvuna maji ya mvua na vijito vya majira kwa njia ya maruba na ujenzi wa mabwawa.

(iii) Kujenga skimu mpya za ukubwa wa kati ya (500-2000) hekta na kubwa kuanzia hekta 2000 na kuendeleza. Aidha kuandaa taarifa muhimu kwa waendelezaji wanaotaka kuwekeza katika kilimo cha kibiashara kama vile kilimo cha mazao yanayotoa nishati mbadala.

(iv) Kutumia maji ya ardhini kwa kuchimba visima vifupi.

Lengo kubwa ni kuwa na miradi ya gharama nafuu inayoweza kusimamiwa na wakulima wenyewe na mashamba makubwa yatakayosimamiwa na wawekezaji ili kutoa ajira kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo napenda sasa kujibu swali la Mheshimiwa Kasella – Bantu, kama ifuatavyo:-

Ujenzi wa bwawa kama lile la Mwanzungi maarufu kwa jina la Mwamapuli unahitaji kuwa na *Site Gorge* ya kujenga banio kati ya vilima viwili katika eneo lililopo juu *up stream* ya sehemu inayotarajiwa kulimwa.

Hata kama *site* ingepatikana ujenzi wa bwawa la ukubwa sawa na lile la Mwampuli ambalo linakadiriwa kugharimu zaidi ya shilingi bilioni tano ingekuwa vigumu kupata kiwango hicho cha fedha, kugharamia ujenzi wa bwana la ukubwa huo.

Mheshimiwa Spika, Mbuga yote ya Bukene imo katika maeneo tambarare. Teknolojia inayofaa wakati huu ni kujenga mabwawa madogo madogo yenye tuta la kina kifupi kati (3-5 m) na gharama nafuu. Mabwawa 12 ya ukubwa huu yalijengwa zamani mengine kabla ya uhuru katika Wilaya ya Nzega, ikiwa ni pamoja na mabwawa ya Malolo, Kisasiga, Itobo na Ikindwa yanayozunguka Mbuga ya Bukene.

Kinachotakiwa sasa ni kuyafufua mabwawa hayo na pale inapowezekana kuyaongezea uwezo wa kuhifadhi maji zaidi. Aidha, kujenga mabwawa mapya yenye gharama ya kati ya shilingi 90 – 200 milioni na kuyatumia kuendeleza kilimo cha umwagiliaji katika Mbuga ya Bukene.

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua kuwepo kwa mbuga yote ya Bukene na historia yake ya uzalishaji wa mpunga na mpango wa uendelezaji wake umekwishaainishwa katika Mpango Kabambe wa kilimo cha Umwagiliaji. Kinachotakiwa sasa ni kuhakikisha kuwa mradi wa ujenzi wa mabwawa madogo madogo unaibuliwa na kuwekwa katika mipango ya maendeleo ya wilaya ili iingizwe katika utaratibu wa kuombewa fedha katika *basket fund* ya *ASDP*.

Mheshimiwa Spika, katika Mpangokazi wa muda mrefu, Wizara yangu imepanga kuanza upimaji na usanifu wa mabwawa na miundombinu ya umwagiliaji katika mbuga ya Bukene katika mwaka 2007/2008. Aidha, chini ya utaratibu wa kuvuna maji, Wizara yangu inatarajia kukarabati na kujenga mabwawa mapya katika Mikoa kame ya Dodoma, Shinyanga na Singida.

**MHE. TEDDY KASELLA – BANTU:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ili niulize maswali mawili madogo ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba kukumbushia kwamba ahadi ya Hayati Edward Sokoine, ni ya zaidi ya miaka 20 sasa. Kwa kuwa ahadi ni deni na kwa kuwa sasa hivi tuna Ilani ya Uchaguzi ya miaka mitano ambayo Waziri Mkuu, naye ni Edward Lowassa na kwa kuwa karibu tutafika miaka 25 tangu amefariki Hayati Sokoine.

(a) Je, Serikali inaweza kuanza sasa hivi katika hayo mambo niliyosema katika mwaka wa fedha huu unaokuja na vile vile kuhitimisha wakati wa kumbukumbu za miaka 25 ya Hayati Sokoine?

(b) Kwa kuwa mabwawa sasa hivi yanatengenezwa katika hali ya kisasa yaani *modern work* yanakuwa *multiple* na kwa kuwa bwawa hili likijengwa litaweza kufanya vile vile majosho kwa ajili ya mifugo na vile vile yatawekwa mabomba kwa ajili ya maji ya nyumbani. Vile vile unaweza kuweka samaki pale kwa ajili ya kitoweo na kadhalika........

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge, uende kwenye swali sasa.

**MHE. TEDDY KASELLA – BANTU:** Ndio niko kwenye swali Mheshimiwa Spika.

**SPIKA:** Hapana lazima tuzingatie muda.

**MHE. TEDDY KASELLA – BANTU:** Sasa unaonaje katika Ilani ya Uchaguzi kutimiza katika maji, kutimiza Ilani ya uchaguzi katika mifugo na kilimo, pamoja na ajira kwa kuweka samaki pale, ifanyike sasa? (*Makofi*)

**SPIKA:** Majibu mafupi Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA (MHE. CHRISTOPHER K. CHIZA):** Mheshimiwa Spika, nampenda kumhakikishia Mheshimiwa Kasella – Bantu kwamba tumefuatilia ahadi hii ya Mheshimiwa Hayati Edward M. Sokoine na kwamba ni ya kweli tumeisoma katika majarada yaliyoko kule kijijini. Lakini nataka nimhakikishie kwamba kama nilivyosema katika majibu yangu ya swali la msingi kwamba katika mpango kazi wetu mwaka 2007/2008 Mbuga ya Bukene imepangwa kuanza kufanyiwa kazi.

Kwa hiyo, hilo naomba alielewe hivyo. Lakini pia labda nimshauri kwamba tunapojenga mabwawa tunaangalia hizo gharama za kujenga bwawa. Tunaelewa mabwana *multipurpose* kama alivyosema mwenyewe ya kilimo, mifugo, majosho, maji ya kunywa yanahitaji upembukizi yakinifu wa muda mrefu na gharama kubwa kusudi yasilete athari baada ya kujengwa.

Mheshimiwa Spika, labda nimhakikishie kwamba utafiti kama nilivyosema utaanza na kwa ajili ya kumbukumbu za Mheshimiwa Sokoine, naweza nikamshauri Mheshimiwa Mbunge kwamba wengine huamua kwa ajili ya kumuenzi kama bwawa litajengwa basi tunaweza kuliita *Sokoine Dam* ili uweze kukumbuka. Naomba niishie hapo. (*Makofi*)

**MHE. MOHAMED H. MISSANGA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Mheshimiwa Naibu katika majibu yake ya msingi ameeleza azma njema nzuri ya Serikali kukarabati *scheme* za zamani ikiwa ni pamoja na *scheme* ya Mang'oni katika Tarafa ya Ikungi na kwa kuwa katika Serikali ya awamu tatu *scheme* hii ilishaanza kusaidiwa fedha na Serikali ili iweze kukarabatiwa vizuri na ikaonekana kwamba *scheme* inahitaji fedha nyingi na Serikali ilianza kuangalia uwezekano wa kutafuta wafadhili ili kusaidia kupata fedha za kutosha kwa ajili ya kukarabati wa *scheme* ya Mang'onyi.

Je, Serikali imefikia wapi katika mfadhili kwa ajili ya ukarabati wa *scheme* hii ya Mang'oni ambayo ni muhimu sana kwa wananchi katika Tarafa ya Ikungi? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA (MHE. CHRISTOPHER K. CHIZA):** Mheshimiwa Spika, mradi wa Mang'onyi ni mradi

ambao unaendelea. Kwa kawaida tunapofanya Bajeti tunaanza na viporo. Kwa hiyo, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Missanga, hata katika mwaka ujao kwa sababu mradi ule, ni mradi ulikwishaanza na unaendelea tunaupa kipaumbele tutauombea fedha chini ya utaratibu wetu *ASDP*.

**SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea sasa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi. Swali linaulizwa na Mheshimiwa Juma Njwayo, Mbunge wa Tandahimba, CCM.

**MHE. JUMA A. NJWAYO:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza. Lakini naomba kutamka kwamba pamoja na marekebisho ya swali niliyokuwa nimefanya nilipoletewa bado swali hili linaonekana limekosewa na halina *concept* ile niliyokuwa nahitaji kwa kukosekana maneno ni mkoa upi una shule chache.

Sasa sina hakika Mheshimiwa Waziri alipopelekewa alipata na maneno hayo? Kama aliweza kuyapata niko tayari sasa kusikiliza majibu. Lakini ningeshauri kama alikuwa hajapata na kwa sababu linahitaji *data* ningeomba labda lirudishe ili lijibiwe siku nyingine.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Tulipata.

**SPIKA:** Basi kwa uthibitisho huo Naibu Waziri kwa majibu.

Na. 51

**Uwiano wa Shule za Sekondari na za Msingi Nchini**

**MHE. JUMA A. NJWAYO** aliuliza:-

Kwa kuwa Elimu ni nguzo kubwa ya maendeleo:-

(a) Je, ni Mkoa gani unaongoza kwa kuwa na shule nyingi za msingi na za sekondari na katika shule hizo ni zipi za Serikali, taasisi za dini na zile zilizojengwa na watu binafsi?

(b) Je, ni hatua gani zitachukuliwa na Serikali ili kurekebisha tofauti ya Mikoa yenye shule nyingi na yenye shule chache?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Juma Abdallah Njwayo, Mbunge wa Tandahimba, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, pamoja na marekebisho ambayo tumeyazingatia, Mkoa unaoongoza kwa kuwa na shule nyingi za msingi ni Shinyanga ambao una jumla ya shule 1,099. Kati ya hizo shule 1086 ni za Serikali, 13 zisizo za Serikali. Kati ya shule zisizo za

Serikali saba (7) ni za watu binafsi, 5 ni za Taasisi za Dini na shule moja inamilikiwa na Kampuni ya Almasi ya Mwadui. Mkoa wenye shule chache za msingi ni ni Mkoa wa Dar es Salaam wenye jumla ya shule 393 kati ya hizo shule 331 ni za Serikali na shule 62 zisizo za Serikali. (*Makofi*)

Mkoa unaongoza kwa kuwa na shule nyingi za sekondari ni Kilimanjaro, ambao una jumla ya shule 298. Kati ya hizo shule 205 ni za Serikali na shule 93 zisizo za Serikali. Kati ya shule zisizo za Serikali shule 82 zimejengwa na watu binafsi na 11 ni za taasisi za Dini ikilinganishwa na Mkoa wa Lindi wenye shule chache zaidi za Sekondari. Mkoa huo una jumla ya shule 47 zikiwemo 44 za Serikali na zisizo za Serikali ni tatu (3) tu ambazo mbili ni za taasisi za dini na moja ni ya binafsi. (*Makofi*)

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali ilijitahidi kurekebisha tofauti za elimu katika Mikoa kwa kuhamasisha wananchi kujenga shule za sekondari za Kata hasa katika maeneo yaliyo nyuma kielimu. Serikali inaunga mkono juhudi za wananchi katika ujenzi wa shule hizo kwa kutoa ruzuku ya maendeleo kwa ajili ya ujenzi na ruzuku ya uendeshaji, kwa ajili ya kununulia vifaa vya kufundishia na kujifunzia.

Aidha, Serikali katika mwaka wa fedha 2006/2007 ilitoa upendeleo kwa kutoa ruzuku ya maendeleo zaidi katika Mikoa iliyo nyuma ukiwemo Mkoa wa Lindi, ili kusaidia kuongeza kasi ya ujenzi wa shule za sekondari katika Mikoa hiyo. Ahsante. (*Makofi*)

**MHE. JUMA A. NJWAYO:** Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa majibu mazuri. Baada ya kusema haya nina maswali kama ifuatavyo:-

(a) Kwa kuwa ni dhahiri kuwa tofauti kubwa ya shule kati ya Mikoa imeleta tofauti ya maendeleo miongoni mwa Mikoa hasa ile ya pembezoni. Na kwa kuwa uko utaratibu wa kutoa kipaumbele kielimu kwa Mikoa ya pembezoni. Je, Serikali iko tayari kufungua shule za kidato cha tano na sita, kwa Wilaya za Mikoa za pembezoni ikiwemo Wilaya ya Tandahimba ili kusaidia kupunguza tofauti ya maendeleo? (*Makofi*)

(b) Kwa kuwa shule zetu nyingi zina tatizo kubwa la maji linalosababisha baadhi ya wakati kukatisha masomo ili kutafuta maji na hivyo kupunguza ubora wa elimu yetu. Je, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, ina mkakati gani wa dharura ili kumaliza tatizo hili kwa shule zetu na hivyo kuongeza ubora wa elimu zetu nchini? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Njwayo kama ifuatavyo:-

Awali ya yote, Serikali kama ilivyoelekeza mwaka jana katika Bajeti yake Mikoa ya pembezoni imepatiwa upembeleo. Suala la kuomba kupatiwa Kidato cha tano na cha Sita ni suala la Kimkoa. Naomba wajadiliane katika mikutano ya *RCC* waweke mapendekezo ni shule zipi wanazipendeza nasi Serikali tutatii maombi yao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, suala la pili kuhusu maji nakiri na nimethibitisha mwenyewe kwamba Wilaya yake ni moja ambayo inapata matatizo makubwa sana ya maji hasa mashuleni.

Tulielekeza na ninaomba kuendelea kutoa ushauri kwamba wakati tunapojenga zile shule tutumie mbinu za kisasa za kuvuna maji ili tujihifadhie maji pamoja na hayo pia kushirikiana na wenzetu wa Wizara ya Maji kuona namna tunavyoweza kuchimba visima virefu au vifupi ili tuweze kuzipatia shule zetu maji. Nakushukuru. (*Makofi*)

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Ahsante. Nashukuru Mheshimiwa Spika na mimi kupata nafasi ili niongezee kidogo kwenye majibu mazuri aliyotoa Naibu Waziri kutokana na maswali ya Mheshimiwa Njwayo. Nilitaka kuongezea tu kwamba Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi baada ya kushirikiana na Serikali kwa ujumla na wananchi, shule nyingi za Sekondari zimejengwa kama tulivyosikia. *(Makofi)*

Mwaka huu tu karibu shule 994 zimefunguliwa. Kwa hiyo, imeona kuna umuhimu wa kuangalia mpango mzima wa sekondari ili tuzingatie zaidi upanuzi wa elimu ya sekondari hasa Kidato cha tano na sita. Kwa hiyo, nilitaka kutoa taarifa tu kwamba kweli kuna umuhimu sisi Tanzania kuongeza shule za kidato cha tano na sita na ndiyo linafanyiwa kazi katika andiko jipya la maendeleo ya shule za sekondari. *(Makofi)*

Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge vuta subira tu na hasa kwa kutilia mkazo kwamba shule za sekondari hasa katika kidato cha tano na sita kwa kweli zinatakiwa ziwe na msingi, ziwe bora zaidi, kubwa zaidi, nyumba za walimu nzuri zaidi, mazingira mazuri zaidi. Kwa hiyo, tutasaidiana na Serikali katika upanuzi wa elimu katika ngazi hiyo. Nashukuru Mheshimiwa Spika. *(Makofi)*

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Ahsante Mheshimiwa Spika, kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa Serikali imefanikiwa katika mpango wa kuongeza shule nyingi za msingi na idadi ya wanafunzi wanaomaliza shule za msingi wanaendelea kuongezeka na idadi ya wanaofaulu kupata nafasi imeongezeka. Idadi ambayo inaenda sambamba na wanafunzi yatima wasio na uwezo wa kujisomesha elimu ya sekondari. Je, Serikali inaweza kuweka mkakati wa kuongeza msaada wa idadi ya kuwalipia wanafunzi wanaomaliza shule za msingi? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA):** Mheshimiwa Spika, Wizara yangu kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya na Halmashauri zingine tumekuwa tukisaidia wanafunzi hawa yatima.

Mheshimiwa Spika, kama ikikumbukwa nilijibu kwamba Wizara sasa hivi inawasaidia wanafunzi katika shule za sekondari wapatao 45,000. Wanafunzi katika shule za msingi wanafadhiliwa na Halmashauri zao.

Mheshimiwa Spika, naomba kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba Bajeti ikituruhusu na vyanzo vya fedha vikiongezeka nasi tutasaidia yatima hawa. Kwani suala la yatima ni letu sote na siyo la mtu mmoja. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa nitaongeza muda kidogo kuzingatia kwanza tulianza na matangazo ya Spika na nimwona Mheshimiwa Phares Kabuye anasimama kwa ukakamavu mara kwa mara, kwa hiyo, naomba nimpe nafasi aulize swali la mwisho la nyongeza. *(Makofi)*

**MHE. PHARES K. KABUYE:** Nashukuru sana Mheshimiwa Spika. Swali langu ni kwamba kwa kuwa nchi yetu tangu zamani ina sifa nzuri ya kujenga usawa miongoni mwa Watanzania, sasa ni kwa nini mkoa mmoja unaweza ukawa na shule nyingi za serikali
kuliko mikoa mingine wakati tunataka kujenga usawa miongoni mwa Watanzania? Ahsante. (Makofi)

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Ahsante sana Mheshimiwa Spika, mimi nilitaka kushauri kwa nia nzuri tu kwamba tugange yajayo. Ndiyo maana unaona Serikali imetilia mkazo sana ujenzi wa shule za Kata ili tuende kwa kasi kama tulivyoiona, shule 994 kwa mwaka huu tu wa 2007. *(Makofi)*

Kwa kweli kazi kubwa imefanyika. Mimi kwa msingi huo ningependa tuangalie mbele na kama alivyosema Naibu Waziri pale katika jibu lake la pili nadhani kwamba tumeshaona kwamba kuna mikoa ipo nyuma, ndiyo maana Kigoma ambako ndiko mkoa wako unakotoka Mheshimiwa Mbunge ! Oh! Kagera sawa sawa. Anatoka Kagera! *Okay!* Ndiyo maana tumeona kwamba mikoa ambayo ipo nyuma tuisaidie.

Mimi ningependa kutoa taarifa katika Bunge hili tukufu kwamba katika shule ambazo tutaanza kutembelea ni shule katika mikoa ile 8 ambayo tuliwapa fedha za ziada ili nao wapige kasi zaidi wafikie angalau wenzao. *(Makofi)*

Kwa hiyo, ningependa kusema kwamba Mkoa kama Kigoma, Lindi, Mtwara, Shinyanga, Pwani mtutegemee, hapana! Mtutegemee kuja kuona ni vipi mmetumia ule msaada wa ziada mliopewa katika bajeti ya 2006/2007 ili tuone kumbe kweli mikoa iliyo nyuma ikisaidiwa inapiga kasi.

Lakini nadhani kwa utaratibu huo huo Serikali itaendelea kuangalia ni wapi ambapo wapo nyuma wasaidiwe zaidi. Lakini ningependa kurudia kutoa wito kwa wananchi wote tupige kasi zaidi ili tuendelee mbele. Nashukuru. *(Makofi)*

Swali Na. 52 liliondolewa na Muuliza swali.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge swali linalofuata Mheshimiwa Makwetta ameliondoa kwa sababu sasa hivi karibuni ameteuliwa kuwa Mjumbe wa Baraza la Ushauri la Waziri wa Elimu na kwa hiyo isingestahili tena. Ushauri wake huo atautoa huko huko wanakokutana. *(Kicheko/Makofi)*

Na. 53

**Kufungwa kwa Shirika la *National Youth Forum***

**MHE. KABWE Z. ZITTO** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali ilifunga shirika lisilo la Kiserikali la *National Youth Forum,* mwaka 2002 lilikuwa linafanya kazi zake za ushawishi na utetezi wa vijana:-

(a) Je, kwa nini asasi hiyo ilifungwa?

(b) Je, Serikali haioni kuwa ufutaji wa Asasi zisizo za Serikali ni ukiukwaji wa misingi ya demokrasia ya uhuru wa kujiunga?

(c) Je, ni lini Serikali itaacha kufuta Asasi za aina hiyo ambazo zinafanya shughuli zake kwa misingi ya sheria za nchi?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA (MHE. DR. EMMANUEL J. NCHIMBI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Zitto Kabwe Zuberi, Mbunge wa Kigoma Kaskazini, kama ifuatavyo:-

Kwanza ,naomba kutoa maelezo ya awali kuwa wadhamini wa taasisi ya *National Youth Forum* walisajiliwa tarehe 10 Juni, 1998 chini ya Sheria ya Muungano wa wadhamini, Sura ya 318 ya Sheria za Tanzania, Toleo la 2002. Sheria hii inasimamiwa na Msimamizi Mkuu wa Wadhamini *(Administrator General of Trustees)* Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini (RITA), Wizara ya Katiba na Sheria.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya, sasa naomba nijibu swali la Mheshimiwa Zitto Zuberi Kabwe, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Muungano wa wadhamini wa *National Youth Forum* ulifutwa kwa kuwa ulishindwa kuthibitisha taswira waliyojiwasilisha nayo kwa umma kuwa wao ni taasisi ya vijana ya kitaifa. Msimamizi Mkuu wa Wadhamini, baada ya kugundua kasoro hii ya misngi alitumia mamlaka yake chini ya sheria ya muungano wa wadhamini na kuifuta taasisi hii.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali haina nia ya kukiuka misingi ya demokrasia ya uhuru wa kujiunga ila inasisitiza kwamba uundaji wa asasi ni muhimu ukaambatana na wajibu wa asasi husika na hasa kuzingatia sheria, kanuni na

taratibu zinazounda asasi husika. Kimsingi Serikali inayo nia na inataka watu wajiunge na kutoa mawazo yao. Hata hivyo, ni vizuri asasi zisizo za Kiserikali zikafahamu kwamba katika demokrasia kuna mipaka yake ambayo inaongozwa na sheria.

(c) Serikali haina lengo la kuzifuta asasi zisizo za Kiserikali ambazo zinafanya shughuli zake kwa misingi ya sheria, kanuni na taratibu za nchi. Namhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali inatambua mchango mkubwa unaotolewa na asasi zisizo za Kiserikali na hasa zinapofuata na kuzingatia sheria za nchi. *(Makofi)*

**MHE KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu ambayo Mheshimiwa Naibu Waziri ameyatoa. Kufuatana na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, amesema kwamba shirika hili halikuonyesha taswira yake kama jinsi ambavyo lilivyokuwa linapaswa kupata sura ya kitaifa. Lakini naamini kabisa kwamba Mheshimiwa Naibu Waziri, yeye ni mmojawapo wa watu ambao walifaidika na kazi mbalimbali za shirika hili nikiwemo mimi, akiwemo Mheshimiwa Halima Mdee, akiwemo Mheshimiwa Aziza na Mheshimiwa Mkuu wa Wilaya ya Lindi, Martin Shigela.

Je, Mheshimiwa Waziri haoni kwamba ilikuwa ni busara kwa Serikali kuwaita wadhamini wa Shirika hili na kufanya nao mashauriano na kuwashauri yale maeneo ambayo wanahisi kwamba wanakiuka taratibu za kisheria au za kikanuni badala ya kulifuta na hivyo sasa hivi vijana wamekosa jukwaa la kusemea masuala yao kwa sababu Baraza la Vijana Taifa bado halijaundwa?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA (MHE. DR. EMMANUEL J. NCHIMBI):** Mheshimiwa Spika, kwanza naomba kukanusha kwamba sijanufaika kwa vyovyote vile na Taasisi hii. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, pili naomba nilitaarifu Bunge lako hili Tukufu kwamba tunaposema haikubeba taswira ya uwakilishi wa vijana nchini, tunataka kusema nini? Tunataka kusema kwamba vijana mwaka huo wa 98 walikutana Arusha, wakakubaliana katika mkutano ambao ulitambulika kama *National Youth Forum* kwamba waunde taasisi inayowaunganisha kitaifa na wakaisajili Mambo ya Ndani, lakini watu wanne peke yao wakaenda kwa *Trustee* kujisajili na kujiita wao Taasisi ya Vijana Kitaifa yenye jina hilo hilo.

Kwa hiyo, kwa vyovyote vile Serikali kwa kutambua wajibu wake wa *moral and legal obligation* ilipaswa kuchukua hatua.

Kwa hiyo, Serikali ilichukua hatua sahihi na kwa kweli siwezi kusema walikuwa na nia mbaya au nzuri. Lakini niseme watu wanne ningependa kuwataja kwa majina.

Hebron Mwakagenda, Israel Ilunde, Ema Kalunga na Wahida Maabadi, ndiyo waliokwenda kujisajili na kujiita *National Youth Forum.* Kuwaita watu wanne waliojisajili peke yao kwamba ni wawakilishi wa vijana wa kitaifa ni kosa kubwa sana ambalo haliwezi kuachiwa na vijana wenyewe wala na Serikali.

Mheshimiwa Spika, naomba niseme Serikali itaendelea kuchukua hatua bila kusita sehemu ambayo tunahisi haki za watu kwa makundi mbalimbali zinaporwa. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa majibu yaliyokamilika. Waheshimiwa Wabunge nadhani ni vizuri tuishie hapa kulingana na muda unaopangwa kwa ajili ya maswali na pia Spika ametumia hekima yake, ili swali linalofuata la wanaume kuruhusiwa kuingia *Labour Room* ni zito sana. Nadhani ni vizuri tulizingatie kuanzia siku ya Jumatatu. Kwa hiyo, Wizara ya Afya maswali yake tutaanza Jumatatu. *(Makofi)*

Matangazo, bado tunao pale kwa *Speaker's Gallery* wageni wetu ambao ni wa mradi wa *Dippening Democracy* kutoka katika *Development Partner's* mbalimbali. *We appreciates your following on proceedings of Parliament. And please feel free to be here in Dodoma and to interrupt with MPs. Thanks for being here. (Applause)*

Wageni wengine Mheshimiwa Zitto, ana mgeni wake anaitwa Hussein Msabila, ni mwanaharakati anayetokea *National Youth Forum* sijui ndiyo hii iliyofutwa. Kwa hiyo, nadhani Bwana Hussein Msabila huna cheo chochote, maana *National Youth Forum* sasa haipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, ameniomba tumtambue mgeni wake, yeye Kamishna Mstaafu wa Magereza, Bwana Ganja Geneya, yuko kule upande ule. Karibu sana! Karibu sana! ahsante sana. Huyu bado mkakamavu, ndiyo uzuri wa kazi za askari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Meris Mussa, ameomba niwatambulishe wageni wake ambao ni wanae, John Mussa na Japhet Mussa, sijui wako wapi, ah! wale pale vijana! Ahsante sana. Karibuni sana vijana.

Mheshimiwa Mwanawetu Zarafi, ameniomba niwatambulishe wanae, mmoja anaitwa Salma Makuti na mwingine Irini Miyingua. Irini na Salma, kwa majina haya mmh! labda nisiseme zaidi. *(Kicheko)*

Waziri wa Nishati na Madini, Mheshimiwa Nazri Karamagi, ameniomba nimtambulishe mgeni wake ambaye ni mpiga kura na mwanaharakati ambaye ni hodari sana kwa kampeni huko Bukoba Vijijini, Bwana Omar Abdallah Kabaka. Yule pale, karibu sana na pole kwa safari ndefu. Ahsante.

Waheshimiwa Wabunge wa Mkoa wa Kagera wameomba tutambue uwepo wa wageni wao ambao ni Bibi Constansia Buhie, Mwenyekiti wa UWT Mkoa wa Kagera, yule pale, karibu sana Mheshimiwa Mwenyekiti. Yuphrazia Mgimya, Katibu wa UWT, Mkoa wa Kagera yule pale na Janet Mussa Kayanda, Mjumbe wa Baraza la UWT Taifa. Karibuni sana. Hawa akina mama wa Kagera wanaonyesha wana umoja kweli kweli. *(Makofi)*

Zaidi ya hapo ninayo matangazo ya ziada yafuatayo:- Mheshimiwa Mbunge wa Nanyumbu, Mheshimiwa Dunstun Mkapa, ameomba niwafahamishe Wabunge na pengine kwa njia hii kulifahamisha Taifa kwamba binti Diana Dunstun, anayesoma Bwawani Sekondari, Kidato cha Tatu, ametoweka nyumbani kuanzia tarehe 9 mwezi wa nne na hadi leo hajulikani alipo.

Kwa tangazo hili naomba wote wahusika pamoja na vyombo vya usalama tuweze kumsaidia apatikane huyu mtoto Diana Dunstun Mkapa aliye Kidato cha Tatu pale Sekondari ya Bwawani Morogoro.

Vikao: Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mwenyekiti wa Maendeleo ya Jamii, anaomba niwatangazie kwamba leo tarehe 13 Aprili, 2007, kutakuwa na Mkutano wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii, Ukumbi Na. 133 na kwa kuzingatia suala la Ijumaa basi itakuwa ni saa nane na robo. Saa nane na robo Kamati ya Maendeleo ya Jamii, Ukumbi Namba 133. *(Makofi)*

Mheshimiwa Alhaj Mohamed Missanga, Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu ameniomba nitangaze kwamba Kamati ya Miundombinu Wajumbe wote mkutane saa 5 asubuhi Ukumbi Na. 428. Saa tano asubuhi Kamati ya Miundombinu Ukumbi Na. 428 bado kukamilisha mjadala kuhusu *Roads Bills* ya 2007.

Mheshimiwa William Kusila, Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama, anaomba Wajumbe wote wa Ulinzi na Usalama kutakuwa na kikao kifupi leo tarehe 13 Aprili, 2007, kuanzia saa 5 asubuhi katika Ukumbi Na. 219. Kamati ya Ulinzi na Usalama saa 5 asubuhi, Ukumbi 219.

Mheshimiwa Zainab Matitu Vulu, ameniomba nitangaze kwamba Wabunge wote wanaotoka katika mikoa ya zao la korosho wanaombwa kuhudhuria kikao kitakachofanyika leo mara baada ya kipindi cha maswali ,Ukumbi Na. 428 ghorofa ya nne.

Waheshimiwa Wabunge nimeombwa kuwakumbusha kwa tangazo nililopatiwa hapa na *Chief Whip* kwamba kama tulivyokubaliana leo tutafanya hitima ya mwenzetu Mheshimiwa Juma Jamaldin Akukweti. Na hitima hii itafanyika pale katika eneo la

viwanja vya *Kilimani Club,* Ukumbi wa Kilimani saa nane na robo baada ya swala ya Ijumaa na sote Wabunge tunaalikwa.

Naarifiwa kwa tangazo hili kwamba Mheshimiwa Waziri Mkuu atakuwepo, Makamu wa Rais pia atakuwepo. Ni dhahiri Spika atakuwepo. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge tumuenzi mwenzetu kwa kuhudhuria hitima hii. Shughuli itaanza rasmi saa 8.10 kwa kisomo halafu sadaka na chakula. Ni vizuri nivitaje vyote hivi ili mtu uende umejiandaa, maana yake isifike wakati wa sadaka mwenzetu ukawa unatazama juu tu, hujui la kufanya. *(Kicheko)*

Tumehakikishiwa kwamba shughuli itakuwa imekamilika kufikia saa 10 kutuwezesha saa 11 kuendelea na kikao chetu cha leo. Ahsante sana, Katibu kwa shughuli za leo.

## MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

### Muswada wa Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa wa Mwaka 2007 *(The Prevention and Combating of Corruption Bill, 2007)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, sasa naomba kutoa hoja kwamba Muswada wa Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa wa Mwaka 2007 ( *The Prevention and Combating of Corruption Bill, 2007),* sasa usomwe kwa mara ya pili.

Mheshimiwa Spika, hatimaye Muswada huu uliosubiriwa sana sasa upo tayari. Hata hivyo, awali ya yote kwa vile hii ni mara yangu ya kwanza kusimama katika Ukumbi huu, naomba nitoe pongezi zangu za dhati kabisa kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Uchaguzi la Mbulu, kumpongeza Mheshimiwa Abdallah Mtutura, kwa kuchaguliwa kuwa Mbunge wa Tunduru. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Muswada huu unaopendekeza kutungwa kwa Sheria mpya ya Kuzuia na Kupambana na rushwa, ni muhimu kwa Watanzania kwa vile vita dhidi ya rushwa ni ajenda muhimu kwa Serikali katika azima yake ya kuwa na jamii inayozingatia haki na uadilifu katika harakati za kujenga nchi na kujiletea maendeleo. Kwa kweli mapambo dhidi ya rushwa yanaenda sanjari na programu nyingi za maboresho na mipango ya maendeleo katika sekta mbalimbali hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, historia ya binadamu inatuonyesha kwamba toka enzi za Adam na Hawa rushwa imeambatana na maisha ya binadamu. Katika Afrika rushwa ilijionyesha kama adha, uovu na uozo katika jamii hasa wakati wa Utawala wa kikoloni mara baada ya uhuru na hadi sasa. Wasomi wetu maarufu katika Afrika muda wote wameandika kwa uchungu kuhusu ubaya wa ufisadi na adha hii na katika kuwasilisha Muswada huu ningependa hata kuwanukuu lakini kwa vile muda hautoshi, itoshe tu kutoa mifano michache ya maandishi ya kina yenye busara yaliyoandikwa na Waandishi Mashuhuri kama vile Ngugi wa Thiong wa Kenya katika vitabu vyake *The Grain of Wheat, The River Between,* na hivi karibuni *The Wizard of the Crown.* Chinua Achebe wa Nigeria katika kitabu chake cha *Things Fall Apart,* I Kwey R. Mawagana, katika kitabu chake mashuhuri, *The Beautiful Ones Are Not Yet Born.* Usi Mbene wa Senegol katika kitabu chake cha *Ghosts Beatiful of Woods* na wengineo. Wengi wetu tumesoma vitabu hivi na tunafahamu vina maudhui i katika mapambano dhidi ya rushwa. Napenda kutaja hapa kwamba waandishi hawa siyo wenyewe duni ani kote, mambo mengi yameandikwa kuhusu rushwa, nawataja hawa tu kwa vile tamthilia zao zinagusa jamii ambazo zinafanana na zetu.

Mheshimiwa Spika, busara zao kwa pamoja zinaainisha uovu na uozo wa rushwa katika jamii kama ifuatavyo:- Kwamba, rushwa hudhoofisha demokrasia na kwa hakika pale kura inaponunuliwa kama bidhaa sokoni husabisha kutoweka kwa demokrasia na kuathiri utawala bora. *(Makofi)*

Kwamba nyakati za uchaguzi rushwa husababisha kupatikana kwa viongozi wabovu. Kwamba rushwa ni matumizi mabaya ya madaraka Serikalini, katika mashirika ya umma na makampuni binafsi pia. Kwa lugha nyingine *abuse of position of our authority,* kwamba rushwa husababisha uwazi na uwajibikaji kuadimika. Hivyo kusababisha jamii kuwa katika hali ya hofu na kutokuaminiana, kwamba rushwa ni ishara ya udhaifu katika uendeshaji wa shughuli za siasa, na Serikali kwa ujumla katika nchi husika. Kwamba rushwa [huleta upendeleo katika utumishi wa umma na hivyo husabisha watu waaminifu kabisa na wenye uzoefu kukosa ajira. Kwamba rushwa ama ni udhaifu uliokithiri sana au kutokuwepo kwa uhuru katika dola kama vile Mahakama. Kwamba rushwa ni ishara ya kukosekana kwa umiliki sahihi wa kiitikadi. Kwamba pia rushwa ni ishara ya dosari katika desturi, mila na maadili ya jamii husika.

Kwamba rushwa husababisha tofauti na matabaka katika jamii, rushwa ni sumu ya maendeleo. Kwa hakika kwenye rushwa iliyokithiri hakuna maendeleo. Rushwa kubwa inaitwa *Grand Corruption,* ni uhalifu unaofanywa kwa umakini na tena kuna watu wajanja sana. Hivyo haiathiri tu shughuli za kiuchumi pekee, bali pia huduma za jamii, kwani fedha zinazotengwa kwa ajili ya shule, hospitali, barabara, madaraja na kadhalika. Kwa viwango tofauti huenda kwa watu binafsi. Jamii au nchi iliyotumbukia katika lindi la rushwa hukosa hadhi, na hudharauliwa katika jumuiya ya kimataifa.

Mheshimiwa Spika, rushwa ni gharama kubwa sana. Katika mwaka 2004 Bwana Daniel Coffman, Mkurugenzi wa Masuala ya Utawala Bora katika Taasisi ya Benki ya Dunia (*The World Bank Institute),* alitoa taarifa kuwa kiasi cha dola za Marekani *trillion 1* yaani kwa shilingi za Tanzania kwa thamani ya leo *trillion 1,250* duniani kote zilitumika katika ulipaji wa hongo. Hii haihusishi wizi na uharibifu wa mali ya uma unaotokea siku hadi siku. Hivyo hii ni biashara kubwa haramu. Bila shaka hali hii ndiyo inasababisha Muswada huu kuvutia hisia za watu wengi ndani na nje ya nchi yetu. Taasisi nyingi za kiraia zimeujadili sana Muswada huu ikiwa ni pamoja na kuchambuliwa kwa kina na mabingwa katika fani mbalimbali ikiwa ni pamoja na waandishi wa habari na wanasheria.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Serikali huu ni wakati muafaka wa kutunga sheria mpya ya kupambana na rushwa. Mtakumbuka kuwa hapa nchini petu Serikali ya mkoloni ilibaini kuwepo kwa rushwa katika watumishi wa ngazi ya kati t angu kabla ya vita vikuu vya pili. Kwa mara ya kwanza kabisa rushwa iliorodheshwa kama kosa la jinai mwaka 1932. Sheria ya kwanza ya rushwa yaani *The Privention of Corruption Ordinance Cap. 400* ilitungwa mwaka 1958. Ilipofika mwaka 1975 Serikali iliunda kikosi cha Kuzuia Rushwa kupitia Sheria Na. 16 ya mwaka 1971.

Serikali ilichukua hatua hii ili kuimarisha mapambano dhidi ya rushwa na kuwa na misingi imara ya kudhibiti mmomonyoko wa maadili hapa nchini. Sheria hii ambayo inatumika hadi sasa ilianisha makosa manne tu ya rushwa ambayo kwanza ni kutoa na kupokea rushwa. Pili, kutumia nyaraka kumdanganya mwajiri. Tatu, Afisa wa umma kujipatia manufaa kwa kutumia Ofisi, na nne, limbikizo la mali kwa njia ya rushwa.

Mheshimiwa Spika, lengo la sheria hii ya mwaka wa 71 kwa muda huu wote limekuwa ni kupambana na vitendo vya rushwa katika sekta ya umma tu. Wakati Sheria hii inatungwa watumishi wa umma hawakuruhusiwa kumiliki hisa au mali, au nyumba za kupangisha, au kuendesha miradi kama vile ufugaji na kadhalika. Pia wakati huo kulikuwa na mfumo wa chama kimoja cha siasa, tofauti na ilivyo sasa ambapo kuna vyama vingi vya siasa. Pia wakati Katiba inaruhusu watumishi wa umma kumiliki mali, hisa na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, tangu Sheria ilipotungwa, kumekuwepo na mabadiliko makubwa sana katika jamii, kiuchumi, kisiasa, kimazingira na kiteknolojia ambavyo kwa pamoja kumeifanya sheria hiyo kutokidhi mahitaji ya wakati na hivyo kuwa na umuhimu wa kuifuta na badala yake kutunga sheria mpya ambayo itaweka utaratibu wa kuzuia na kupambana na rushwa kwa kuzingatia mahitaji ya sasa.

Mheshimiwa Spika, vilevile mkakati wa kupambana na rushwa, *the national anticorruption strategy and action plan,* Cap. 1999, ulielekezwa kutungwa kwa sheria mpya ya kuzuia na kupambana na rushwa nchini itakayokuwa na wigo mpana zaidi wa kuzuia na kupambana na rushwa.

Aidha, kutokana na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuridhia mikataba ya kimataifa na itifaki dhidi ya rushwa ambayo ni pamoja na Mkataba wa Umoja wa Mataifa dhidi ya Rushwa, (*The United Nations Convention Against Corruption*) wa mwaka 2003, Mkataba wa Umoja wa Afrika wa Kuzuia na Kupambana na Rushwa *(African Convention on Preventing and Combating Corruption*) wa 2003 na Itifaki ya Jumuiya ya nchi za Kusini mwa Afrika, ( *SADC Protocol Against Corruption*) na kwamba kwa sababu hiyo sasa kuna umuhimu mkubwa wa kupitisha sheria ambayo inakidhi matakwa ya mikataba hii.

Mheshimiwa Spika, mambo muhimu yaliyozingatiwa katika Muswada huu ni pamoja na:

(a) Kuanzishwa kwa taasisi huru, kuzuia na kupambana na rushwa chini ya Ofisi ya Rais itakayotekeleza majukumu yake bila ya kuingiliwa kiutendaji na chombo au mamlaka yoyote wakati wanatekeleza jukumu lake la upelelezi na kuendesha mashitaka yaani *operation independence.*

(b) Inaweka misingi ya ushirikiano kati ya taasisi na vyombo vingine vya Serikali ndani na nje ya nchi katika kupeana taarifa fiche. Kushirikiana katika chunguzi mbalimbali kufungua mashitaka mahakamani na kadhalika.

(c) Kuwapa mamlaka maafisa wa taasisi hii kupata taarifa na ushahidi kutoka kwa mtu au taasisi yoyote.

(d) Muswada unaipa taasisi uwezo wa kufilisi mali zitakazopatikana kwa njia ya rushwa na kisha kuzirejesha Serikalini kwa kushirikiana na Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

(e) Muswada unaipa taasisi mamlaka ya kuzuia kwa muda (*freezing of assets*), mali za watuhumiwa ambazo zinahisiwa kupatikana kwa njia ya rushwa wakati uchunguzi unaendelea. Uzuiaji huu wa muda utafanyika wakati kibali cha kuzuia mali kinaombwa kutoka kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

(f) Muswada unaongeza na kuainisha makosa mbalimbali ya rushwa kwa kuzingatia mikataba na Itifaki ya kimataifa dhidi ya rushwa hususan katika maeneo ya mikataba zabuni na minada, na hapa ningependa kutaja badala ya makosa yale manne.

Muswada unapendekeza makosa mengine 20. Muswada huu sasa unapendekeza sheria ya baadaye ya rushwa iwe na makosa 24.

(g) Muswada unajumuisha sasa sekta binafsi katika mapambano dhidi rushwa. Aidha, maafisa wa umma wa nchi za nje na maafisa wa taasisi za Serikali za mataifa mengine waliopo nchini watashughulikiwa pia na Sheria hii.

(h) Muswada unaowalinda watoa taarifa za vitendo vya rushwa na pia mashahidi.

(i) Muswada unaipa Taasisi kutunga kanuni za uendeshaji na maadili kwa watumishi wake.

Mheshimiwa Spika, Muswada ulipokuwa unajadiliwa na kuchambuliwa katika nyakati tofauti ilikuwa imependekezwa kuwa vitendo vya rushwa katika chaguzi hizi za siasa kuongezwa katika makosa yaliyoorodheshwa katika Muswada huu. Lakini baada ya kutafakari hili imeonekana si vema kufanya hivyo kwa sasa kwa vile hivi sasa kuna maandalizi ya mjadala wa kitaifa kuhusu namna bora zaidi ya kuendesha chaguzi za kisiasa hapa nchini, kwa lengo la kuangalia kwa kina zaidi sheria za uchaguzi na ile ya vyama vya siasa.

Mheshimiwa Spika, kwa kifupi sana Muswada huu umegawanyika katika sehemu saba kama ifuatavyo:-

Sehemu ya kwanza ya Muswada, yenye ibara ya 1,2,3 na 4 inapendekeza masharti juu ya mambo ya utangulizi ambayo yanajumuisha jina la sheria, tafsiri ya maneno mbalimbali yaliyotumika katika sheria na walengwa wa sheria hii.

Sehemu ya pili ya Muswada ni Ibara ya 5 hadi 14, inapendekeza kuanzishwe kwa taasisi ya kuzuia rushwa, zaidi taasisi ya kuzuia na kupambana na rushwa ili baada ya mapendekezo haya, taasisi ya kuzuia rushwa iwe ni chombo huru cha kutekeleza majukumu yake kwa maana ya kutoingiliwa kiutendaji na chombo au mamlaka yoyote wakati inatekeleza jukumu lake la upelelezi.

Sehemu ya tatu ya Muswada , ibara ya 15 mpaka 41 zinaainisha makosa ya rushwa ambayo ni pamoja na makoasa mengine yanayohusiana na kupinga vitendo

hivyo. Pia inaainisha adhabu mbalimbali zinazopendekezwa kutolewa kwa watakaovunja masharti ya Sheria hii.

Seheumu ya Nne ya Muswada yaani ibara ya 42 mpaka 46 inapendekeza kuwa masharti yanayoiwezesha Serikali kufungua kesi za madai ili kupata amri ya mahakama kufilisi mali zilizopatikana kwa njia ya rushwa.

Sehemu ya tano ya Muswada yenye Ibara 47 na 48 inapendekeza masharti yatakayowezesha taasisi ya kuzuia na kupambana na rushwa kuwa na mahusiano na vyombo vya ndani na nje ya nchi katika kupeana taarifa za siri, kushirikiana katika chunguzi mbalimbali na pia kushitaki watuhumiwa kwa vitendo vya rushwa.

Sehemu ya sita ni ibara 40 hadi 51, inapendekeza masharti yanayohusu masuala ya fedha kama vile vianzio vya ofisi ya mapato vya taasisi hii.

Sehemu ya saba na ya mwisho ya Muswada yenye Ibara ya 52 hadi 63 inapendekeza masharti ya jumla yanayohusu kinga kwa watumishi wa taasisi ya kuzuia na kupambana na rushwa, na pia kuwalinda mashahidi wanaotoa taarifa za vitendo vya rushwa juu ya upatikanaji wa kibali cha mwanasheria mkuu wa Serikali kutokuendesha kesi za rushwa mahakamani pamoja na uwezo wa Waziri kutengeneza kanuni chini ya Sheria hii. Hatimaye Sheria inapendekezwa kufutwa kwa Sheria ya Kuzuia Rushwa, sura ya 329.

Mheshimiwa Spika, katika kuhitimisha napenda kusema kuwa hakuna ubishi kuwa sote tunachukia rushwa, kwa vile rushwa pia inatuumiza sote. Malengo yetu ni kupambana na rushwa kwa nguvu zote, kwa vile katika jamii matendo ya rushwa hufananishwa na malazi mabaya na huwaumiza wananchi wengi hasa wa kipato cha chini. Katika jamii jamii yetu watu wanaonufaika na matendo ya rushwa ni wachache sana. Huu ni wakati mzuri katika historia ya nchi yetu kwa wananchi kujihusisha na mapambano dhidi ya rushwa kwa nguvu zaidi kwani kwa hakika kuna utashi wa kisiasa upande wa viongozi wa Serikali.

Sheria mpya na taasisi huru ya kuzuia na kupambana na rushwa zitakazotokana na Muswada huu zitakuwa ni silaha zingine katika mapambano haya.

Mheshimiwa Spika, bila shaka Bunge lako Tukufu pamoja na Wabunge wenzangu wote tutakuwa vinara katika mapambano hayo hivyo, naomba basi Waheshimiwa Wabunge waujadili Muswada huu kwa kina na hatimaye kuupitisha. Katika kufanya hivyo, napenda kusema kwamba baada ya kuwasikiliza wadau mbalimbali pamoja na wataalamu waliobobea katika maeneo haya, na maoni ya Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala, tumekubali kufanya mabadiliko mengi katika Muswada na mimi naamini utakidhi mahitaji ya Wabunge, mabadiliko haya yana kurasa sita, yana Ibara 24.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri, kabla sijamuita Mwenyekiti au mwakilishi wake wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, kuna matangazo muhimu ambayo yamenifikia, na naomba kutangaza kama ifuatavyo. Wajumbe 10 wa PAC na LAAC waliofanya ziara ya mafunzo London Uingereza, Februari, 25 hadi Machi, 3 leo saa sita mchana yaani baada ya dakika 50 hivi wakutane katika ukumbi Na. 432 jengo la Utawala. Hili ni tangazo kutoka kwa Mwenyekiti wa Kamati za Hesabu za Serikali, Mheshimiwa John Cheyo, ambalo nilipaswa kutangaza mapema lakini nilighafilika. Kwa hiyo, Wajumbe wa PAC na LAAC watakuta na CAG na staff wake saa sita kamili katika ukumbi Na. 432 leo.

Waheshimiwa Wabunge kwa maandalizi ya semina yetu ya kesho wajumbe wote wa TAPAC wanaombwa mara baada ya kusitisha shughuli saa saba wakutane kwa mkutano mfupi chumba Na. 133 ghorofa ya kwanza. Mwenyekiti Mheshimiwa Lediana Mafuru Mng'ong'o anaomba wajumbe wote mkutane mara baada ya kusitisha shughuli hapo saa saba, ili kukamilisha maandalizi ya kesho. Kwa Waheshimiwa Wabunge wote sasa kesho saa nne kamili katika ukumbi wa Pius Msekwa kutakuwa na semina muhimu iliyoandaliwa na Balozi wa Marekani ,Bw. Michael Laizer kwa kushirikiana na TAPAC.

Mnaombwa ili tuanze katika muda basi Waheshimiwa Wabunge mjisajili saa tatu na nusu, ili ikifika saa nne, wageni wetu hawa kutoka Dar es Salaam wa USAID pamoja msaidizi wa Balozi tuweze kuanza katika muda, saa tatu na nusu kesho katika ukumbi wa Pius Msekwa. Kwa Wabunge wote Semina hii ni muhimu yenye takwimu si tu tatizo la UKIMWI, lakini pia mgao wa fedha za vyanzo mbalimbali za mataifa unavyoelekezwa katika wilaya mbalimbali, hili ni muhimu sana kulijua Waheshimiwa Wabunge.

**MHE. TATU M. NTIMIZI (k.n.y MWENYEKITI WA KAMATI YA KATIBA, SHERIA NA UTAWALA):** Mheshimiwa Spika, kabla sijaanza kutoa maelezo ya Kamati naomba kumpongeza Mheshimiwa Mtutura kwa kuchaguliwa kwake kuwa Mbunge wa Tunduru, hongera sana nakutakia kazi njema.

Lakini pia naomba kutoa pole kwa familia ya aliyekuwa Mbunge wa Gairo na Waziri wa Afya katika Serikali ya Awamu ya Tatu, na mimi wakati huo nikiwa Naibu Waziri wake ambaye amefariki dunia leo katika hospitali ya Hindumandal. Kifo kimenigusa kwa kuwa nimefanya naye kazi kwa ukaribu na kwa upendo. Dr. Chiduo, alikuwa anatayarishwa kwenda India kwa tatizo la kansa ya damu, lakini asubuhi Mwenyezi Mungu kachukua roho yake. Kwa hiyo, nimeona ni vema nitoe rambirambi zangu na Mwenyezi Mungu aiweke roho yake peponi Amen!.

Mheshimiwa spika, baada ya hayo kwa niaba ya Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala, napenda kuchukua fursa hii kukushukuru kwa kunipa nafasi hii muhimu kuwasilisha maoni ya Kamati kuhusu Muswada wa Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa wa Mwaka 2007 (*The Prevention and Combating of Corruption Bill, 2007*) kwa mujibu wa Kanuni ya 70(2), Kanuni za Bunge, Toleo la 2004. Lakini kabla sijafanya hivyo napenda nielezee kwa kifupi hatua iliyotangulia kabla ya kuujadili muswada huu.

Mheshimiwa Spika, Kanuni ya 69(2) inatamka kwamba, Kamati iliyopelekewa Muswada inaweza baada ya kupata idhini ya Spika, kumwalika mtu yeyote afike kutoa maoni yake mbele ya Kamati, kwa lengo la kuisaidia katika uchambuzi wake. Aidha, Kanuni ya 88(6) inatamka, pamoja na mambo mengine kuwa, Kamati inaweza kuwaruhusu Wabunge ambao si Wajumbe wa Kamati au watu ambao si Wabunge kuhudhuria kushiriki katika shughuli za Kamati, lakini hawatapiga kura.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuipatia Kamati yangu kazi ya kuufikiria muswada huu, iliwaarifu wadau na wakipenda kwa kutumia utaratibu wa kusikiliza maoni ya wananchi (*public hearing*) kama ulivyoainishwa katika kanuni nilizozitaja, kufika kwenye Kamati kwa ajili ya kusikiliza au kutoa maoni yao kuhusu maeneo mbalimbali ya muswada na kuisaidia Kamati. Utaratibu huu ni njia mojawapo ya kuwashirikisha wananchi katika mchakato wa kutunga sheria na ulianza kutumika katika miaka ya tisini na elfu mbili, hususan wakati wa kujadili muswada wa Sheria ya Makosa ya Kujamiiana ya mwaka 1998, Sheria ya Ardhi ya mwaka 1999 na Sheria ya Ardhi ya Vijiji ya mwaka 1999, Marekebisho ya 13 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 2000, ambapo Kamati zilizohusika ziliwaalika wadau wengi waliosaidia kuboresha miswada iliyotajwa.

Mheshimiwa Spika, Kamati hii ilikutana tarehe 27 Machi, 2007 katika Ofisi ya Bunge, Dar es Salaam, na kupokea maelezo ya Serikali yaliyowasilishwa na Mheshimiwa Philip S. Marmo, (Mb.), Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Utawala Bora), kuhusu mapendekezo yaliyokusudiwa katika Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kupokea maelezo hayo ya Serikali, Kamati iliitenga siku hiyo kwa ajili ya kupokea na kusikiliza maoni ya Wadau kama ilivyo kuwa kawaida ya kuwapa fursa kutoa maoni yao. *(Makofi)*

Kwa kuwa muswada huu uligusa maslahi ya jamii (*public interest)*, wadau wengi walijitokeza. Wengi waliojitambulisha walikuwa kutoka makundi mbalimbali kama vile, kundi la *National Organization For Legal Assistance (NOLA), The Leadership Policy Forum, Tanzania Youth Coalition, TANLET, Legal and Human Rights Centre, FEMACT, YUNA, UDASA, TADEA,* Chama cha Wabunge cha Kupambana na Rushwa *(APNAC)* na wadau wengine.

Mheshimiwa Spika, tuliwasikiliza wadau tarehe 27 – 28 Machi, 2007 na baadaye Kamati ilianza kazi yake ya kuujadili muswada huu kama kanuni zinavyoelekeza.

Mheshimiwa Spika, maoni ya wadau wengi yalijielekeza kuipa nguvu Taasisi ya Kuzuia Rushwa na Kupambana na Rushwa na kupendekeza iwe huru, inayojitegemea na itakayoundwa kikatiba kama zilivyo taasisi nyingine nchini. Napenda nichukue fursa hii kuwashukuru wadau hao kwa michango yao mizuri ambayo napenda kuwahakikishia kuwa Kamati iliifanyia kazi na kuishauri Serikali kwa yale yaliyowezekana.

Mheshimiwa Spika, nikianza na maoni ya jumla, Kamati inakiri kuwa muswada huu una umuhimu wa pekee kwa wakati uliopo katika kuimarisha juhudi za Serikali za kuzuia na kupambana na rushwa inayozidi kushamiri siku hadi siku katika sura tofauti.

Mheshimiwa Spika*,* katika kuujadili muswada huu ibara kwa ibara, katika sehemu ya tafsiri, Kamati iliona kuwa tafsiri ya neno rushwa kama ilivyo ina upungufu, kwamba haitoi tafsiri pana ya kuhusisha makosa mengine yakiwemo yanayohusiana na siasa hususan chaguzi mbalimbali za kisiasa.

Hata hivyo, Serikali ilisema kuwa hakuna tafsiri maalumu ya neno rushwa isipokuwa tafsiri hupatikana kutokana na vitendo atakavyovifanya mtu kama ilivyoainishwa katika muswada na kwamba hata rushwa ya kisiasa imeguswa katika muswada huu. Kamati iliupokea ufafanuzi huu na kuridhika na maelezo ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine linahusu utaratibu mzima wa utoaji wa zawadi kwa watumishi wa umma. Katika kuliangalia suala hili, Kamati imebaini kuwa iwapo sheria iliyoweka ukomo wa zawadi kwa mtumishi wa umma inayoweka masharti kuwa akiwa katika utumishi anastahili kupokea zawadi isiyozidi shilingi elfu hamsini, na kwamba anapopewa zawadi inayozidi kiwango hicho anahitajika kuwasilisha kwa mwajiri wake. Pamoja na kuwepo kwa sheria hii, Kamati ilibaini kuwa uzoefu unaonyesha kuwa yapo mazingira ambapo mtumishi wa umma hupokea zawadi zinazozidi kiasi hicho na kutotoa taarifa, hali ambayo huweza kuashiria kuwa zawadi inayohusika imetolewa katika mazingira ya rushwa.

Aidha, Kamati imebaini kuwa taasisi za umma zikiwemo idara, wizara na mashirika ya umma, zimekuwa zikipokea zawadi kutoka kwa wahisani, vikiwemo vifaa vya ofisi, samani, magari, n.k. Katika mazingira hayo, Kamati ilionyesha wasiwasi wake kuwa zawadi za namna hiyo, zinaweza kutumiwa vibaya na wafadhili ama wa ndani au nje kuitumia Wizara, idara au shirika linalohusika, kukiuka utaratibu pale mhisani atakapokuwa na jambo lake ambalo angependa lishughulikiwe na chombo hicho.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa taasisi nyingi za umma zimekuwa zikipokea zawadi za aina hiyo, Kamati inashauri kuwa kuanzia sasa zawadi zinazokusudiwa kutolewa na watu au vikundi vya namna hiyo hazinabudi zichunguzwe na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa ikiwa ni pamoja na kuchunguza nyendo za wafadhili wanaohusika, na Taasisi hiyo ipewe uwezo wa kisheria wa kuishauri Serikali au chombo chochote cha umma kupokea au kutopokea zawadi. Aidha, kuhusu zawadi zinazotolewa kwa watumishi wa umma, Kamati inashauri kuwa sheria inayohusika iangaliwe upya na kujumuishwa katika Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Pili ya Muswada inaanzisha Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa pamoja na kuainisha majukumu mbalimbali ya Taasisi hiyo. Majukumu hayo yameainishwa katika Ibara ya 7 (a) – (g), ambayo ni pamoja na kutoa taarifa kwa umma juu ya ubaya na athari za rushwa kwa jamii. Kwa kuzingatia kuwa zipo desturi na tamaduni fulani fulani katika jamii ambazo zikitumiwa vibaya zinaweza kuhalalisha vitendo vya rushwa, Kamati inashauri kuwa ibara ya 7(a) – (c) iboreshwe na kuandikwa upya ili pamoja na mambo mengine, iiongezee Taasisi jukumu la kuuelimisha umma juu ya madhara ya desturi na tamaduni za aina hiyo.

Mheshimiwa Spika, katika kulitazama kwa upana suala la rushwa, Kamati imetafakari juu ya vitendo mbalimbali vya uharibifu wa mali za umma unaofanywa na baadhi ya watumishi wasio waaminifu na waadilifu. Vitendo hivyo ni pamoja na matumizi holela ya vifaa vya Serikali kama karatasi, fotokopi, magari, ununuzi wa spea na samani na kadhalika.

Kamati inaona kuwa matumizi ya namna hii yanajenga mazingira yanayosababisha rushwa na ukiukwaji mkubwa wa taratibu, kanuni na sheria zinazohusika. Kamati inashauri kuwa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa ikabiliane kikamilifu na vitendo hivyo vinavyorudisha nyuma maendeleo ya Taifa na kuzishauri taasisi au vyombo vinavyohusika kuwadhibiti watumishi wake.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine linahusu madaraka makubwa aliyopewa Mkurugenzi wa Mashitaka kuingilia shughuli za Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa. Madaraka hayo ni pamoja na sharti lililowekwa katika Ibara ya 7(f) ya Muswada kuitaka Taasisi kufungua mashitaka ya rushwa baada ya kupata maelekezo kutoka kwa Mkurugenzi wa Mashitaka.

Pamoja na maelezo ya Serikali kumhusisha Mkurugenzi wa Mashitaka ni katika kutekeleza dhana nzima ya kuchunguzana na kudhibitiana (*checks and balances),* Kamati inashauri kuwa madaraka ya Mkurugenzi wa Mashitaka katika sheria hii yawekewe mipaka, kwamba, katika mazingira fulani apewe siku za kutekeleza madaraka yake na akishindwa bila kutoa sababu maalumu, basi Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa iendelee, vinginevyo Kamati inaona kuwa kutofanya hivyo kutaipunguzia Taasisi hadhi ya kuwa huru na inayojitegemea.

Aidha, Kamati iliijadili kwa kina ibara ya 9(2) ya muswada inayotamka kuwa Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi au afisa aliyemuidhinisha atakayeshindwa kufungua mashitaka baada ya kukamata mali ya mtuhumiwa wa rushwa kama ilivyofafanuliwa katika ibara ya 9(1), hanabudi kuomba muda usiozidi miezi sita kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali baada ya muda wa awali kumalizika iwapo atataka kuendelea kushikilia mali ya mtuhumiwa. Kamati inashauri kuwa kifungu hicho kiangaliwe upya, kwani muda ni mrefu na haki inatakiwa itendeke haraka kwa mtuhumiwa.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya III ya Muswada inaanzisha na kuainisha majukumu ya Bodi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa. Kamati ilieleza tatizo la muundo wa Bodi hiyo pamoja na majukumu yake yanavyoingiliana na Taasisi. Nafurahi kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa Serikali imeamua kuifuta Bodi hii kama inavyoonekana kwenye jedwali la Marekebisho.

Mheshimiwa Spika, katika sehemu ya IV ya Muswada inayohusu makosa ya rushwa na makosa mengine yanayohusiana na vitendo vya rushwa na adhabu mbalimbali zinazopendekezwa kutolewa kwa wakosaji, Kamati inaona kuwa adhabu zilizotolewa ama zina upungufu au hazilingani na kosa husika. Hivyo, inashauri kuwa adhabu zitakazotolewa ziwe kali. Aidha, adhabu ya faini ilingane na kifungo.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine linahusu ibara ya 28 ya Muswada inayowataka watumishi wa umma kuonyesha mapato yao wanapoajiriwa. Kamati inashauri kuwa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa iweke mazingira ya kisheria kuwataka watumishi wa Idara, Wizara na Mashirika ya Umma kuorodhesha mali zao pindi wakiajiriwa ili iwe rahisi kuwafuatilia.

Mheshimiwa Spika, kwa muhtasari haya ndiyo maeneo ya jumla ambayo Kamati yangu iliyatolea maoni na kuishauri Serikali. Napenda nikuhakikishie kuwa sehemu kubwa ya ushauri wetu umefanyiwa kazi na Serikali kama inavyoonekana katika Jedwali la Marekebisho la Muswada huu.

Mwisho, napenda nikushukuru kwa kunipatia nafasi hii muhimu. Vilevile napenda nimshukuru Mheshimiwa Philip S. Marmo, (Mb.), Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Utawala Bora) akisaidiwa na Mheshimiwa Johnson Mwanyika, (Mb.), Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Bw. Edward Hosea, Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia Rushwa, Bw. Casmir Kyuki, Mwandishi Mkuu wa Sheria na wataalamu wao, ambao walishirikiana vema na Kamati hadi kufikia hatua hii. Pia nachukua fursa hii kuwashukuru wadau wote kwa kufika mbele ya Kamati na kutoa maoni yao yaliyoisaidia sana Kamati kuishauri Serikali.

Mwisho kabisa, nawashukuru wajumbe wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, kwa kufanya uchambuzi wa kina na kuuboresha muswada huu. Jedwali la Marekebisho ni matokeo ya kazi nzuri waliyoifanya. Na sasa naomba niwatambue Waheshimiwa walioshiriki katika Kamati hiyo: Mhe. George Malima Lubeleje, Mwenyekiti, Mheshimiwa Tatu M. Ntimizi, Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Pindi H. Chana, Mheshimiwa Stephen J. Galinoma,Mheshimiwa Athumani S. Janguo, Mheshimiwa Rajab Hamad Juma, Mheshimiwa Shoka Khamis Juma, Mheshimiwa Charles N. Keenja, Mheshimiwa Salim Yussuf Mohammed, Mheshimiwa John P. Lwanji, Mheshimiwa Fatma M. Maghimbi, Mheshimiwa Ramadhan A. Maneno, Mheshimiwa Halima J. Mdee, Mheshimiwa Nimrod E. Mkono, Mheshimiwa Abbas Z. Mtemvu na Mheshimiwa Dr. Wilbrod P. Slaa.

Pia nawashukuru makatibu wa Kamati hii, Ndugu Emmanuel Mpanda, Ernest Zulu na Charles Mloka, kwa kuihudumia Kamati na kutayarisha maoni haya.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naiunga mkono hoja hii na naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MHE. SHOKA KHAMIS JUMA (MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, napenda kuwasilisha maoni ya Kambi kuhusu Muswada wa Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa wa Mwaka 2007 (*The Bill on the Prevention and Combating Corruption Act,* 2007, kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, Kanuni Ndogo ya 43(5) (c) na 70(2), Toleo la 2004.

Mheshimiwa Spika, kabla sijaanza kutoaupungufu kama ambavyo umejitokeza katika muswada huu, napenda kutoa pongezi zangu binafsi kwa Mheshimiwa Kabuye kwa kuchaguliwa na chama chake cha *TLP* kuwa Makamu Mwenyekiti wa chama hicho. Aidha, napenda kumpongeza Ndugu yetu Benedicto Mutungirehi Mutachoka kwa kuchaguliwa kwake kuwa Katibu Mwenezi wa chama cha T*LP.* Aidha ninamtakia Spika wa Bunge letu Tukufu afya njema ili afanye vizuri kazi tuliyomkabidhi kwa niaba ya Watanzania katika ujumla wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nichukue wasaa huu kutambua kazi iliyofanywa na Serikali ya kuridhia mikataba ya kimataifa ya kupambana na adui rushwa na ufisadi ikiwemo, Mkataba wa Umoja wa Mataifa dhidi ya Rushwa *(United Nations Convention against Corruption (UNCAC),* Mkataba wa Muungano wa Afrika wa Kuzuia na kupambana na Rushwa *(The African Union Convention on Prevention and Combating Corruption),* na Protokali ya *SADC* dhidi ya rushwa *(Southern African Development Community Protocol against Corruption).*

Mheshimiwa Spika, pia napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa wadau wote ambao waliitajirisha sana Kamati yetu wakati wa *Public Hearing*. Pamoja na kwamba kuna malalamiko kutoka kwa baadhi ya watu, Kambi ya Upinzani inadhani kuwasikiliza Wadau wote wakiwemo wahisani wetu kwa Muswada mzito kama huu, ni busara kuliko kulalamikia tukio hilo.

Mheshimiwa Spika, ni ukweli kuwa katika utungaji wa sheria ni lazima na muhimu sheria inayotungwa iambatane na tafsiri ya sheria nyingine zilizopo, hivyo basi ilikuwa ni vizuri sheria hii iziangalie sheria zingine za kimataifa za kupambana na rushwa ambazo tayari tumekwisha ziridhia pamoja na sheria zetu zingine za ndani na kuziweka katika sheria moja. Kwa mfano, kuna vifungu vingine vilivyomo katika sheria ya maadili ya viongozi wa umma ambayo madhumuni yake ni kuzuia rushwa lakini haijahuishwa na sheria hii tunayotunga leo.

Mheshimiwa Spika, katika tafsiri ya maneno, kifungu cha 3, kina maneno "*illicit enrichment*" maana ya kuongezeka kwa dhamana ya mali kwa mtumishi wa Serikali ambayo hawezi kuzitolea maelezo kulingana na kipato chake. Lakini katika Muswada haionyesha kutumika kwa neno hilo na inavyoeleweka dhahiri vitendo hivyo kwa watumishi wa Serikali ni vingi mno.

Hata hivyo, tunatambua kuwa Serikali kwa marekibisho yaliyowasilishwa sasa hivi ndani ya Bunge lako imefuta kipengele hiki. Aidha pamoja na maelezo mengi ya Serikali, Muswada huu umeshindwa kutoa tafsiri ya neno "*corruption*", japokuwa limetumika mara nyingi katika muswada.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inamtaka Waziri atoe ufafanuzi juu ya matumizi ya neno hilo na jinsi sheria hii itakavyoweza kushughulika na jambo hili kwa watumishi wa Serikali. Aidha, mbali ya hayo Kambi inaona haya ni upungufu wa utunzi wa sheria bila ya kuangalia na kuoanisha sheria zingine zilizopo kama ambavyo tumeoanisha hapo juu.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 5(2) "*bureau shall be an independent public body*", kwa mantiki hii inaonyesha kuwa taasisi hii ina mamlaka ya kushitaki ama kushtakiwa na kwa mujibu wa kifungu cha 10(2) taasisi inafanya kazi zake kwa kufuata maelekezo ya Mkurugenzi wa Mashtaka na vile vile inawajibika moja kwa moja kwa Mheshimiwa Rais. Kambi ya Upinzani inauliza kuwa kwa vifungu hivi uhuru wa Taasisi upo wapi? Kwa mtu makini, ukiacha kifungu hiki, vifungu vyote vinavyofuata havionyeshi kuwa Taasisi hii ni huru, hasa kiutawala na utoaji wake wa Taarifa. Taasisi inajiwajibika kikamilifu kwa Mheshimiwa Rais kama ilivyo katika sheria ya sasa. Taasisi bado inapokea "maelekezo" kutoka kwa *DPP*, mamlaka ya *DPP* kuweka *Nolle Presqui* yapo pale pale hata katika kesi zilizoanzishwa na Mkurugenzi Mkuu na hata bila kutoa sababu za hatua yake hiyo. Hii ni kudhoofisha uhuru wa Taasisi hii muhimu katika vita dhidi ya Rushwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inaamini kuwa chombo huru cha umma katika utendaji wake kwa mujibu wa sheria hakiwezi kuingiliwa na idara nyingine za Serikali, mashirika binafsi na asasi za kiraia. Hivyo basi ili kulinda uhuru wa chombo hiki ni lazima uhuru huu utamkwe ndani ya katiba ya nchi. Kama ilivyotamkwa ndani ya Katiba Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, hivyo hivyo suala la kuzuia na kupambana na rushwa litamkwe bayana ndani ya Katiba.

Mheshimiwa Spika, ahadi ya tano ya Chama cha TANU inaeleza kuwa "rushwa ni adui wa haki sitapokea na kutoa rushwa", kwa bahati mbaya, wana-TANU na wana-*ASP* walioandika Katiba ya CCM baada ya kukamilisha katiba ya CCM walisahau suala hili kuliainisha wazi wazi ndani ya Katiba ya nchi. Sasa ipi kubwa? Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali badala ya kuweka kiraka kingine katika Katiba yetu hili suala la TAKUKURU iliyo huru liingizwe ndani ya Katiba, ni vyema Watanzania wakapewa fursa ya kuandika Katiba mpya shirikishi, itakayoliingiza suala la kuzuia na kupambana na rushwa pamoja na mambo mengine ndani ya Katiba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 6(1) kinaelezea jinsi taasisi itakavyokuwa, lakini utaratibu unakuwa wa kisiasa na kukifanya chombo hiki kuwa cha kulinda kundi fulani zaidi badala ya kulinda maslahi ya Taifa. Hivyo basi, kutokana na kutokuwekewa utaratibu unaoeleweka wa vigezo vya kumpata Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Kupambana na kuzuia rushwa, Kambi ya Upinzani inaona kuwa itakuwa ni bora kama nafasi hii muhimu katika chombo hiki muhimu iwe ni ya kikatiba na utaratibu wake uelezwe wazi na kama ikibidi utaratibu ulioainishwa katika sheria ya uanzishwaji kwa mamlaka ya mawasiliano Na. 12 ya mwaka 2003 katika kifungu cha 13(2) zitumike. Kifungu hiki kimeorodhesha vigezo vya mtu kuwa Mkurugenzi Mkuu wa TAKUKURU na kwa kufuata utaratibu kama huo na vigezo hivyo hivyo sifa za kumpata Mkurugenzi Mkuu wa TAKUKURU zielezwe wazi. Aidha Mkurugenzi huyo pamoja na chombo hicho wawajibike moja kwa moja kwa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kuleta maana halisi iliyolengwa na kifungu cha 5(1) yaani kuifanya Taasisi kuwa chombo huru. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani kwa mantiki hiyo inaungana na wadau mbali mbali kuwa mtu yeyote mwenye sifa za kuwa jaji wa mahakama kuu au mwenye cheo cha *Assistant Commissioner* wa Polisi au Magereza, mwenye uadilifu mkubwa katika utendaji wake wa kazi na awe pia na uwezo mkubwa katika ngazi ya utawala, mtu huyu anaweza kuwa Mkurugenzi Mkuu wa TAKUKURU.

Mheshimiwa Spika, kwa maana hiyo basi ni wazi kuwa chombo hiki hakitokuwa na ulazima wa aina yoyote wa kuwa na Bodi ya Wakurugenzi kama ambavyo ofisi ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali inavyofanya kazi japokuwa na yenyewe inatakiwa iwajibike moja kwa moja kwa Bunge na sio kwa Mheshimiwa Rais. Nafurahi kuwa katika marekebisho yaliyowasilishwa sasa hivi Serikali imefuta eneo lote linalounda Bodi yaani sehemu yote ya Tatu ya Muswada.

Pamoja na kwamba sina uhakika kama kuifuta yote ni jambo bora, kwani sasa *Civil Society*, na jamii kwa ujumla zimeondolewa moja kwa moja katika kushirikishwa kwenye mapambano dhidi ya rushwa kupitia Taasisi hii. Kihali halisi kufuta kipengele hiki kimehalalisha sasa Taasisi kuwa moja kwa moja chombo cha Serikali na hivyo kuondoa uhalali wa kifungu cha tano kinachofanya Taasisi kuwa chombo huru.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inaona ni muhimu kwa Mkurugenzi Mkuu pamoja na maafisa wa juu wa TAKUKURU wawe na kinga ya ajira (*Security of Tenure*), jambo ambalo halikuainishwa katika Muswada huu. Kufukuzwa kwao kazi kufuate utaratibu uliowazi na isije kuwa wanaweza kufukuzwa kwa sababu ya kufuatilia na kuchunguza vitendo vya rushwa vya wanene katika Serikali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Kambi inatoa rai hiyo kwa ukweli kuwa kwa muundo wa Taasisi unaopendekezwa katika Muswada na marekebisho yake wa utendaji wa TAKUKURU viongozi wakuu wa Serikali kwa maana ya Rais, Makamu wake na Waziri Mkuu chombo hiki kinakosa nguvu za kuwafanyia kazi pale wanapobainika kuwa wanatakiwa wachunguzwe. Mfano mzuri ni kujiuliza je, chombo hiki kipya kwa muundo huo kinaweza kufanya kama kile cha Afrika ya Kusini kilivyofanya kwa aliyekuwa Makamu wa Rais, Bwana Jacob Zuma kuhusiana na tuhuma za kupokea rushwa? Isitoshe ikumbukwe kuwa historia duniani inaonyesha kuwa wanaohamisha fedha nyingi za nchi na kuziweka kwenye akaunti za nje kama vile Switzerland ni viongozi wazito wa nchi husika na mifano ipo mingi, tusitunge sheria kwa ajili ya leo, lakini tutunge sheria inayoweza kutokea hata nchini kwetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 12 kinawapa uwezo Mkurugenzi Mkuu na maafisa wa chini yake wa kupeleleza, kupekua na kukamata mali za watu wanaotuhumiwa kuhusika na rushwa. Hata hivyo kifungu hicho hakielezi taratibu za kuwa na kibali cha upekuzi (*search warrant*). Kambi ya Upinzani inaona ni lazima kuwepo na mipaka katika kufanya ukaguzi huo, mamlaka na *powers* wanazopewa ni kubwa mno na kuna uwezekana mkubwa wa kuzitumia vibaya.

Mheshimiwa Spika, usiri wa kiutendaji wa TAKUKURU kwa kulingana na mamlaka waliyopewa yanaweza kupelekea vitendo vya rushwa zaidi badala ya kupingana nayo. Muswada unatoa nguvu zaidi kwa watendaji kuanzia kushuku, kuchunguza na kushtaki na kufungua mashtaka na hii kwa maana nyingine ni hatari. Hapa ndipo msemo wa "*absolute power corrupts absolutely*". Ni muhimu kuwe na chombo cha kutoa "*checks and balances*" kwa watumishi wa TAKUKURU ili kuwa na ufanisi ulio bora na kuondoa dhana ya chombo hiki kuweza kutumika kwa matakwa binafsi. Hata hivyo katika marekebisho yaliyoletwa sasa hivi, kifungu cha 10(2) kinafanyiwa marekebisho kwa kuondoa neno "*investigation*". Sina hakika na tafsiri halisi ya hatua hii, Mheshimiwa Waziri alifafanulie Bunge hili, je, kwa marekebisho haya TAKUKURU haina tena mamlaka ya kufanya upelelezi (*Investigation*)? Iwapo jibu ni ndiyo, je, huku si kuipunguzia mamlaka na uhuru tuliousema hapo juu? Je, kama ndivyo hakuna namna ya kujenga "*Checks and Balances*" ndani ya TAKUKURU yenyewe lakini wasipunguze madaraka? Kambi ya Upinzani inahitaji maelezo ya kina kuhusu hatua hii ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 17(2) kinaonyesha adhabu pamoja na faini kwa wale waliopatikana na hatia ya rushwa. Kambi ya Upinzani inaona kwa vyovyote vile sio haki kutamkwa katika sheria jinsi hakimu anavyotakiwa kutoa hukumu kwa yule mwenye hatia ya rushwa. Hii inambana hakimu kutokutoa adhabu ya juu na inambana kuweka adhabu ya chini kwa makosa ya rushwa.

Hata hivyo, katika marekebisho yaliyowasilishwa sasa hivi naona Serikali imevifanyia marekebisho vifungu hivyo, pamoja na kwamba Kambi ya upinzani inadhani bado sheria haichanganui ukubwa wa kosa na adhabu inayoambatana nayo.

Mheshimiwa Spika, hivyo basi ni bora majaji wakapewa uwezo wa kuamua ukubwa wa adhabu kulingana na kiasi na thamani ya rushwa yenyewe, vinginevyo watuhumiwa wataendelea kudharau mahakama kwani watakuwa wanajua adhabu ya kosa husika na itakuwa rahisi kwao kuhakikisha faini wanazilipa. Mfano rushwa ya mabilioni katika rada halafu mtuhumiwa alipe faini ya Tanzania ya Sh.5,000,000/= au 10,000,000/= tu. Kwa hili haki ipo wapi kwa walipa kodi wa Tanzania? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 18 kinazungumzia wanaofanya vitendo vya rushwa kwa mamlaka za umma na watumishi wa umma kuwa wote watakuwa wametenda kosa. Hapa Kambi ya Upinzani inadhani kuwa rushwa ni rushwa tu na kwa kuelezea kuwa ni kwa kuhusisha watumishi wa umma tu ni makosa kwani hata watumishi binafsi wao kwa wao kama vitendo vya rushwa vimetumika na huko ni lazima sheria ichukue mkondo wake. Vinginevyo inaonyesha kuwa sheria hii haina uhusiano na sekta binafsi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mambo mengine lakini madhumuni makubwa ya Muswada huu ni kuhakikisha utawala bora na nidhamu na uadilifu kwa watumishi wa Serikali. Katika kutimiza hilo jamii ya Watanzania inategemea kuwa Muswada wa sheria hii uweke wazi utaratibu wa jinsi ya utendaji kazi wa TAKUKURU utakavyokuwa, hii ni pamoja na kutoa taarifa za utendaji kazi wake kwa jamii nzima ikiwa ni pamoja na kuleta

taarifa zake kwa kipindi cha mwaka katika Bunge na kuweza kujadiliwa na wawakilishi wa wananchi yaani Waheshimiwa wabunge.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa kifungu cha 28 kinachosema kuwa mtumishi wa umma anatakiwa kutoa orodha ya mali zake ni wazi kuwa kifungu hiki kipo katika sheria ya maadili ya viongozi wa umma ya mwaka 2002. Kambi ya Upinzani inaona kuwa kama sheria ipo na bado haitekelezwi kama ilivyopaswa, je, ni kwa kiasi gani haya tunayotaka yawemo katika Muswada huu yatafanyiwa kazi?

Mheshimiwa Spika, tunaitaka Serikali itoe tathmini mpaka sasa ni viongozi wangapi waliweka wazi mali zao wakati wanakuwa viongozi na wakati wanamaliza uongozi walitangaza mali zao? Na wale waliodanganya kuhusu thamani ya mali zao wakati wa kumaliza uongozi wao Serikali imewachukulia hatua zipi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pamoja na maelezo yote ya Waziri, Kambi ya Upinzani inadhani tunafanya makosa makubwa na ni vigumu sana kwa Serikali kueleweka na Wananchi kwa kuacha kipengele cha rushwa katika siasa katika Muswada huu. Kwa kutofanya hivyo, TAKUKURU imezuiwa kufanya uchunguzi wowote, na kuchukua hatua kuhusu rushwa ndani ya Siasa. Hata kama Sheria ya Uchaguzi, na Sheria ya Vyama vya Siasa zitafanyiwa marekebisho, Sheria hii ndiyo mlango wa TAKUKURU kuingia maeneo yote ya rushwa na wala si sheria ya Uchaguzi wala ya Vyama vya Siasa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hatimaye sheria hizo zinaweza kufafanua na kupanua maeneo mahususi ya rushwa katika siasa. Ndicho tulichofanya katika rushwa ya ngono, rushwa katika manunuzi, rushwa katika ajira, rushwa katika mikataba. Maeneo yote hayo yanayo sheria zake mahususi, lakini kwa kuziingiza katika sheria hii ndio mlango unafunguliwa kwa TAKUKURU kuzishughulikia. Kambi ya Upinzani inashindwa kuelewa Serikali inapata kigugumizi gani kuingiza angalau sentensi chache katika sheria hii ili TAKUKURU ipate uhalali wa kuingilia masuala ya rushwa katika siasa. Au ndio usemi mitaani kuwa 'Wanasiasa wanashindwa kuingilia rushwa kwa vile wamepitia chaguzi zilizojaa rushwa'? Kambi ya Upinzani hatutaki kuamini rasmi kauli hiyo, ndiyo maana tunamtaka Mheshimiwa Waziri atoe maelezo ya kina na siyo maelezo kuwa sheria hizo zinafanyiwa marekebisho. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kulingana na Muswada huu, ni dhahiri kuwa TAKURU haikutakiwa kuwa Idara ya Serikali ili vita dhidi ya rushwa vieweze kweli kupiganwa kikamilifu na kushinda. Kwa hali halisi Serikali na vigogo wa Serikali ndio wanalalamikiwa kwa tuhuma za rushwa, ni vigumu sana mtu anayetuhumiwa kujiundia taratibu za kujidhibiti. Ni kweli sisi ni miongoni mwa nchi za mwanzo mwanzo kutunga sheria ya kupambana na rushwa baada ya Mikataba ya Kimataifa ya Kupambana na Rushwa kama vile ya Umoja wa Mataifa ya Umoja wa Afrika na kadhalika. Kwamba sisi ni wa mwanzo mwanzo, haihalalishi tutunge sheria isiyo bora, kuanzia sasa ingekuwa bora sisi tukawa mfano Duniani kwa kutunga sheria ambayo wengine watakuja kujifunza kwetu na kuifanyia "*reference*".

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani naomba kuwasilisha, nawashukuru wote kwa kunisikiliza. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Msemaji wa Kambi ya Upinzani, Waheshimiwa Wabunge orodha yangu ya wachangiaji ni wachangiaji 21 na ninapenda nitoe nafasi maalumu kwa Kiongozi wa Upinzani humu Bungeni kwa kutambua nafasi yake awe msemaji wa kwanza. Baada ya hapo atafuata Mheshimiwa Wilson Masilingi, Mheshimiwa Dr. Guido Sigonda, Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa, Mheshimiwa Victor Mwambalaswa, Mheshimiwa Mohamed Rished Abdallah, Mheshimiwa Agrey Mwanri, Mheshimiwa William Shellukindo, Mheshimiwa Dr. Harrison Mwakyembe, Mheshimiwa Dr. Chrisant Mzindakaya, Mheshimiwa Dr. Zainab Gama, Mheshimiwa Richard Nyaulawa, Mheshimiwa Mohamed Habib Mnyaa, Mheshimiwa Juma Abdallah Njwayo, Mheshimiwa Dr. Binilith Mahenge, Mheshimiwa Juma Killimbah, Mheshimiwa Vedastusi Manyinyi, Mheshimiwa Godfrey Zambi, Mheshimiwa Chacha Wangwe, Mheshimiwa Lucy Owenya na tutamalizia na Mheshimiwa Manju Msambya. Ni dhahiri basi kwamba mjadala huu utaendelea hadi Jumatatu, tutaanza leo na tutaendelea jioni kwa hiyo, uzito wa jambo hili nakusudia karibu kila aliyejiorodhesha aweze kutoa maoni. (*Makofi*)

Kwa hiyo, sasa namwita Mheshimiwa Kiongozi wa Kambi ya Upinzani Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed.

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, kwanza nikushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii ya kwanza ya kuchangia Muswada huu muhimu sana katika Taifa letu. Lakini niungane na Mheshimiwa Tatu Ntimizi kwa kutoa pole na rambirambi kwa ndugu zetu wafiwa wa Dr. Chiduo, wengi tunamfahamu tulikuwa naye Bungeni miaka mingi, tunatoa rambirambi zetu kwa Wananchi wa Morogoro, kwa familia na Watanzania wote kwani yeye aliwatumikia Watanzania wote kwa muda mrefu sana. Mungu ailaze mahali pema peponi roho yake.

Mheshimiwa Spika, kwanza nilitaka kuanza na utangulizi kwamba sheria hii ambayo imefanyiwa kazi kwa muda mrefu ni sheria moja nzito sana na muhimu sana katika Taifa letu. Kwa uzito huo basi tulitegemea kabisa kwamba Serikali itazingatia sana kwamba idara hii ya rushwa isingebaki kama idara tu ya kawaida katika Wizara yoyote au katika chombo chochote bali kingekuwa ni chombo ambacho kimo ndani ya Katiba. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nasema hayo kwa sababu nilikuwa naangalia rikodi za Serikali, kuna kitabu cha Serikali kilichotolewa cha *state of the public service report* ya mwaka 2004. Katika kitabu hiki kinazungumzia sana mambo yote ya utawala, kuna *section* moja ambayo ni sehemu ya rushwa. Sasa ukiangalia mambo ambayo yanatokea ndani ya rushwa mojawapo ni katika kutoa huduma na ndio chanzo cha rushwa inapoanzia. Sasa katika mpangilio wa vyombo ambavyo vimekuwa juu katika rushwa ni kama vifuatavyo kwa mujibu wa taarifa ya Serikali. Kwanza ni *Ministry of Home Affairs* asilimia 90, *Prime Minister's Office* asilimia 78, *Ministry of Community Developments,*

asilimia 72, *Ministry of Defense* asilimia 70, *Foreign Affairs* asilimia 66, *Office of the Vice President,* asilimia 59, *State House* asilimia 51 na vingine vinafuatia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa chombo hicho unakwenda kukiweka katika Wizara hizo hizo au sehemu hiyo hiyo *efficency* na uhakika utavipata wapi? Sasa nasema tulivyokuwa tunasemwa kwamba ni muhimu chombo hiki kikabaki *independent* kwa maana ya kuingizwa ndani ya katiba lakini *independence* yake vile vile kwamba kiwajibike kwa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ukishaiacha *executive* ambayo tayari yenyewe katika rikodi zake zenyewe za Serikali katika upungufu wake wa utendaji wa kutoa huduma ambao ndio chanzo cha rushwa kina isiyoridhisha, huwezi tena chombo hicho kitakachosimamia hao watendaji ukakiweka chini yao.

Mheshimiwa Spika, sasa mimi nasema ukibakisha kama Idara ya Serikali bado ni tatizo la msingi ambalo Serikali lazima ilikubali *efficiency* ya chombo hicho itakuwa dhaifu sana na *output* yake itakuwa ni ndogo sana. Pamoja na nia nzuri, leo tuna Rais pengine kuwa na nia nzuri maana yake unapotunga sheria huitizami ilivyo unaitizama leo, kesho na kesho kutwa, leo unaweza kuwa na mtu *serious* katika hili lakini kesho akatokea mtu akakitumia chombo hicho vibaya utafanyaje? Inabidi urudi tena Bungeni kuja kubadilisha. Kwa hivyo, ninasema ni chombo ambacho kinahitajiwa kuingia katika katiba na ni chombo ambacho kinatakiwa kweli kiwe *independent* na si idara kama idara nyingine za Serikali, hilo halitaweza kufanikiwa na madhumuni makubwa ya sheria hii hayatafanikiwa, hilo lilikuwa la kwanza.

Mheshimiwa Spika, la pili ugumu wa kazi yake chombo hiki ukitizama taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali na ukitizama sheria yenyewe sehemu ya tatu ambayo inazungumzia juu ya suala la maafisa wa Serikali kuhusu maadili, ukitizama taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi wa Serikali hakuna Afisa ambaye ataachwa kwenda kwenye TAKURU kuhojiwa, watakuwa wachache sana, *eleven billion shillings* maafika wahasibu hawakueleza matumizi yake, *four billion shillings procurement* mbovu.

Kwa hiyo utakuta watu wengi sana watahojiwa na chombo hiki, kwa hiyo kuna mambo ya msingi yanatakiwa kufanyika. Kwanza, chombo kikiwa *independent* kitakuwa na uhuru wa kuajiri watu ambao wanaweza kufanya kazi yenyewe, leo ukishawekwa utaratibu huu wa kawaida wa ajira chombo hiki hakitakuwa *efficient* hata kidogo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nasema tuna sababu za msingi za kuona kuwa chombo hiki kinasimama chenyewe kufanya kazi. Sasa hivi tunazungumza hapa tunaona kama ni jambo dogo lakini ukiona majukumu ya kisheria waliyopewa na uzito wa kazi unaotaka kufanya, humu ndani watabaki watu wachache sana ambao hawatakwenda kuulizwa au kuhojiwa na chombo hiki, sasa unapokiacha chini ya idara unafika mahali unasema wanamuhoji nani? Hamad Rashid, hebu muache huyu ni mwenzetu kwa sababu wame-*control* ule uwezo wao na ninasema bahati mbaya tunajiangalia kwa sababu tunatunga sheria tunajiangalia sisi leo, tuangalie mbele ya safari tutakuwa na *type* gani ya *leadership* tutakayokuwa nayo, je, wapo *serious,* tumechukua muda mrefu hapa, tumeingia kwenye mambo ya *ladder* tumeingia mambo chungu nzima ya rushwa lakini leo tunakuja na sheria hii, basi hatujifunzi kwamba mambo makubwa ya rushwa

yaliyotokea hapa nchini tumeshindwa kuchukua hatua, kwa sababu gani? Kwa sababu ya kulindana, halafu chombo kama hiki unategemea kiwe *efficient* unaenda kukiweka pale pale mahali ambapo kuna *source* ya kulindana, hakiwezi kuwa *effective*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tutamlaumu Mkurugenzi, ninakuhakikishia kabisa kwamba tutakilaumu chombo hiki baada ya siku tano kutoka hapa Bungeni, hata tukiwa *serious* kiasi gani bado chombo kinatakiwa kweli kiwe *independent,* acha kiwe na upungufu wake katika utendaji lakini chenyewe kisheria basi kipate ile *independency* yake tunayoizungumza hasa *independency, auditor general* kwa nini tumempa mamlaka hayo na ndio maana amekuwa *efficient* kuweza ku-*produce* hizi *report, otherwise* angekuwa na yeye vile vile anatingwa tingwa tu basi ingekuwa ni tatizo. Kwa hiyo, tunayo *experience* ya kwamba chombo ambacho unakipa mamlaka kamili basi kinakuwa na matatizo madogo.

Mheshimiwa Spika, hapa Bungeni leo tunasema Bunge letu bado lina kasoro, tunategemea bajeti ya Serikali ndio wanaotuamuliwa kwamba leo, pesa zenu hizi hapa kesho wanachukua, kesho kutwa wanarudisha kama watoto wadogo tu. *Independency* ya vyombo hivi ni muhimu sana, taasisi lazima ziwe *independent.* Hatuwezi ku-*question* matumizi ya Rais *the executive,* kama tunaweza wasingeweza kutumia *billions of money* 2003 wanakuja *after four years* kwenye *Parliament* kuomba idhini ya Bunge. Wanavunja sheria na pesa zinatumiwa kwa sababu Bunge halina uwezo, huwezi ukavunja sheria ya nchi lakini kwa sababu madaraka ya Bunge bado ni madogo, ndio hali inakuwa hivyo *independency* yetu pia inaondoka, kwa hiyo, na vyombo kama hivi kama havikuwekewa utaratibu wa kuwa *very much independent* bado tutaendelea kupata matatizo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mimi ushauri wangu wa kwanza ni huo kwamba ni vizuri Serikali ikaliangalia hili tusije tena hapa Bungeni tukakilaumu chombo hiki kwa nini hakikufanya kazi yake kwa sababu hatukukipa mamlaka kamili ya kufanya kazi, kazi hii ni nzito sana tunaiona ni nyepesi sasa hivi tunazungumza hapa lakini ni nzito tu. Ni nzito kwa sababu inamgusa kila Mtanzania, leo ukitaka kufanya *lobbing* kwa mujibu wa sheria hii inaweza ikatafsiriwa kama ni rushwa, wakati katika utandawazi huu tulionao sasa hivi tunasema *lobbing* ni *part of the business*. Sasa je, nani atakayetafsiri kwamba wewe Mheshimiwa Cheyo katika biashara zako unafanya *lobbing* bila kutoa rushwa? Kwa hivyo tunataka watu ambao ni *competent*, *capable* na kuweza kusema fulani anahusika au hausiki na jambo fulani, hao hautawapa kama hautakuwa na utaratibu wa chombo hiki kujisimamia chenyewe, hilo lilikuwa ni jambo ambalo nilitaka kulisisitiza.

Mheshimiwa Spika, la pili ni ajira ya watumishi wa chombo hiki. Sasa hivi wanatumia hizi sheria za *civil service* zilizopo na nafikiri tunayo matatizo makubwa katika utaratibu huu ukiangalia *volume* yake kwa sheria hii watahitaji watu wengi sana kuwaajiri. Ningeshauri sana utaratibu wa *vetting* wa watu watakaoajiriwa basi waangaliwe kwa makini sana, inatakiwa wapatikane watu wenye uwezo, waadilifu waweze kufanya kazi hii. Kwa hiyo, suala la *vetting* ni *very important* kwa chombo kufanya kazi yake.

Mheshimiwa Spika, la tatu ni suala la *procurement.* Ukitazama Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu utakuta kuna kiasi cha *billion 1.3 shillings* zimekuwa hazikutumika vizuri kutokana na manunuzi ya ovyo. Kwa hiyo, nilikuwa nashauri kazi moja ya TAKURU ni kuzuia rushwa na njia moja ya kuzuia rushwa ni kuwa wazi katika shughuli zetu za kufanya biashara.

Nilikuwa nashauri wakati umefika sheria nyingine za *procurement* nazo zitamke wazi suala zima la kuingia katika *electronic procurement* kwa sababu inapunguza kwa kiwango kikubwa sana *level of corruption.* Tafiti mbalimbali zimefanywa na *World Bank,* zipo taasisi hizo zinafanya, kazi hiyo imesaidia sana. Kwa bahati mbaya sheria hii haikugusia kabisa eneo hilo na kwa sababu eneo ambalo Serikali inapoteza fedha nyingi sana ni katika eneo la manunuzi, eneo la manunuzi ni sehemu moja ambako rushwa inatamkwa sana.

Kwa hiyo, mimi nilifikiria katika kuzuia rushwa suala la *electronic procurement* ni la msingi sana na ni jambo ambalo linaeleweka na mimi nafikiri lingeweza likafanyiwa kazi na sheria hii pengine ingetamka ingeweza kusaidia sana.

Mheshimiwa Spika, hayo ndio maeneo ambayo nilitaka nianze nayo na ninaomba Mheshimiwa Waziri atakapojibu atusaidie ufafanuzi wa kina kabisa suala la *independence* ya TAKURU.

**MHE. WILSON M. MASILINGI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi niweze kuchangia hoja iliyopo mbele yetu ambayo ni Muswada wa Sheria ambao unakusudia kufuta sheria ya mwaka 1971 na tuwe na sheria mpya ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa.

Kabla sijaendelea kuchangia napenda niungane na wachangiaji walionitangulia kutoa salaam za rambirambi kwa familia, ndugu, jamaa na marafiki wa familia ya Marehemu Dr. Aaron Chiduo, nami nilimfahamu sana tulikuwa naye ndani ya Bunge hili alikuwa Mbunge wa Gairo. Tunaomba Mwenyezi Mungu ailaze roho yake mahali pema peponi. *Amin!*

Pili, napenda kumpongeza Mheshimiwa Mtutura Abdallah Mututura, Mbunge wetu mpya ambaye amechaguliwa kuwa Mbunge wa Jimbo la Tunduru, namuahidi kwa niaba ya Wananchi wa Jimbo la Muleba Kusini, ushirikiano wa karibu katika kutekeleza majukumu yake ndani ya Bunge na nje ya Bunge.

Tatu, napenda kuipongeza Serikali kwa kuendeleza mapambano dhidi ya rushwa na kuleta marekebisho ya sheria ya kuwezesha vita hii kubwa na ngumu dhidi ya rushwa na pia ninampongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Utawala Bora, kwa jinsi alivyowasilisha Muswada huu, hotuba yake imeeleza kwa mapana historia, uzoefu na majukumu ya nchi yetu Kimataifa na ndani ya nchi kukabiliana na tatizo hili la rushwa.

Vile vile niwapongeze wasaidizi wake wote na hasa niseme rasmi nilishampongeza Mheshimiwa Edward Hosea, Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia

na Kupambana na Rushwa na Msaidizi wake Ndugu Lilian Mashaka na pia wasaidizi wao wote, kazi zao ni nzuri na uteuzi wao uliofanywa na Mheshimiwa Rais kwa kweli ulistahili kwani ni vijana waadilifu na wachapakazi na hii itawapa moyo wale ambao wanafanya nao kazi kuiga mfano wao ili na wao baadae waweze kufika juu. Isije Serikali ikalazimika kutekeleza yale mapendekezo niliyosikia ya kutafuta viongozi wa TAKURU kutoka nje ya taasisi yenyewe.

Mheshimiwa Spika, baada ya pongezi hizo, nina machache tu na ni ushauri. Ushauri wa kwanza naishauri Serikali kwa sababu imeonyesha mfano mzuri sana wa kuzingatia mapendekezo ya wadau wakiwemo Waheshimiwa Wabunge katika mjadala wa mapendekezo, isifunge milango yake ya kupokea ushauri na vile vile isifunge roho yake katika kukubali kama ilivyofanya na kudhihirishwa na marekebisho yaliyoletwa mbele yetu kupitia *Schedule of Amendments* iliyoletwa na Mheshimiwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Utawala Bora. *(Makofi)*

Kwa kweli marekebisho makubwa yamefanyika na ukiangalia unaona yote kwa sisi ambao tulipata fursa ya kushiriki katika semina mbalimbali. Serikali wamekuwa wasikivu sana. Kwa hiyo, naomba Serikali msifunge milango.

La kwanza katika kulifikiria ni ushauri mzuri ambao umetolewa na Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala. Maoni yake ambayo yametolewa ni mazito na ni mengi sana lakini ambalo napenda kusisitiza ni hili ambalo limetoka dhahiri kuhusu uhuru wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wamekwenda mbele zaidi kushauri kwamba ifanywe vipi. Kamati kwa niaba yetu imependekeza na tumesikia kwa taarifa yake kwamba kuhusu uhuru wa utekelezaji *(Operational of Independence)* kwa kukosa kuweka ukomo, kumfunga mikono *DPP* kwa kiwango cha kuheshimu uhuru wa utekelezaji wa TAKURU. Mkurugenzi wa Uendeshaji wa Mashtaka yaani *DPP,* anaweza kusitisha nisingependa kutumia neno baya la kuhujumu, kusitisha kasi ya TAKURU kufanya kazi zake.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hili naamini Mheshimiwa Waziri anaweza akalichukua mapema sana, *DPP* apewe muda kama Kamati ilivyoshauri wa kufanya maamuzi yake iwapo TAKURU watakuwa wamempelekea kwa njia ya mashirikiano jambo fulani ambalo anapaswa ashirikiane nao katika utatuzi.

Katika kuwawezesha waendelee na kazi yao, si vizuri kuacha *DPP* aamue mwenyewe, TAKURU wasubiri hata kama ni miaka miwili au mitatu au mitano. Sasa mimi sitaki kusema *DPP* si muadilifu, kwanza naye ni mpya, naye pia ni kijana safi, ameteuliwa na Mheshimiwa Rais. Mimi nilikuwa simfahamu lakini vyombo vilivyompendekeza vime m-*vet* na mimi sina pingamizi, kwa hiyo, sina ugomvi naye kwa sababu simfahamu.

Mheshimiwa Spika, lakini tunachozungumza kwa uzoefu ni kwamba yalikuwepo manung'uniko kwamba Mkurugenzi wa Mashtaka anachelewesha maamuzi, sasa hilo

kwa sababu ni dhahiri na limezungumzwa sana na wadau ni vema likafanyiwa kazi kwa sababu limeletwa rasmi na Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala. *(Makofi)*

La pili ambalo napenda kushauri ni kwamba huu uhuru kama alivyosema Kiongozi wa Kambi ya Upinzani, uhuru wa TAKURU bila fedha za kutosha za kuendesha mambo yake una walakini. Sasa hivi wako mpaka Wilayani na wachache sana ingawa waliajiriwa wengi wasomi. Ni wachache na hata kwa kiwango cha mafunzo wanahitaji kuongezewa mafunzo ya uchunguzi, Sheria na Haki za Binadamu na kadhalika. Vitendea kazi, mishahara mizuri sana kuzidi hata ya *TRA* ni muhimu ili kusudi waweze kufanya kazi zao bila kukwama kwa sababu ya fedha. Hili ni jambo jema ambalo ningeshauri Serikali iangalie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Bungeni kuna malalamiko, fedha zinazotengwa hazitoshi kulingana na Bajeti kubwa ya Serikali, Mahakama ina malalamiko. Basi si vizuri tukaendelea kutiliana mashaka kwa sababu sote tuna jukumu moja la kujenga Taifa kwa kushirikiana na kufanya mambo sawa sawa. Kwa hiyo, kipengele cha uhuru wa kifedha ni muhimu sana katika uhuru wa aina yoyote ile kwa sababu hata Taifa ambalo halijitegemei kiuchumi, linategemea fedha kutoka nje haliwezi kusema ni uhuru. Sasa sisemi TAKURU wawe wanajichukulia fedha Hazina, hapana. Tunasema wapewe fedha za kutosha kulingana na usimamizi wa Waziri husika. Kwa hiyo, nalisisitiza hilo kwa sababu mishahara yao ni midogo.

Pia nawapongeza Mamlaka ya Kukusanya Mapato ya Serikali *(TRA)*. Walipowezeshwa kifedha na uhuru wa kusimamia mambo yake na wao katika mageuzi yao wamewezesha hata walipakodi waweze kujipima wenyewe na kuamua walipe kodi kiasi gani. Tumesikia mafanikio makubwa kwa muda mrefu, jana tu tumeelezwa kwamba mwezi Machi Serikali kwa mwezi mmoja tu imekusanya fedha bilioni 258.9. Hiyo ni mwezi Machi tu na ni wastani mzuri. Kwa hiyo, Serikali inapaswa kupongezwa na *TRA* inastahili kupongezwa.

Mheshimiwa Spika, mwezi Desemba walikusanya shilingi bilioni 258.7 kwa hiyo, wako kwenye wastani wa shilingi bilioni 200 na kuendelea. Kwa hiyo, hakuna sababu kwa kweli, tukiweka vipaumbele vyetu sawa sawa kwa nini Bunge walalamike mambo ya Bima. Kwa nini Mahakama walalamike na kwa nini TAKURU wasipewe fedha ya kutosha ambao tumewapa jukumu kubwa la kusimamia sheria muhimu kwa jamii ambayo kwa kweli inavuka mipaka ya itikadi za kisiasa. Ndiyo maana namuunga mkono huyu kiongozi wa Kambi ya Upinzani na siyo kwamba naunga mkono *CUF,* amesema *point* na akisema *point* ni lazima tumpongeze. *(Makofi)*

Kwa hiyo, kwa vile fedha zinaongezeka basi mishahara ya TAKURU iongezwe na Polisi iongezwe na majeshi yetu pia iongezwe na ya watumishi wengine wa umma vile vile. Kama Mheshimiwa Rais alivyoahidi katika hotuba yake mbele ya Bunge. Alisema ataiangalia hii mishahara. Sisemi kwamba ndiyo chanzo cha rushwa. Kwa sababu mwizi ni mwizi hata ungempa pesa kiasi gani, wala rushwa wengi ni matajiri tayari na hawajaacha, watapokea tu na anapokea kutoka kwa maskini siyo kwamba anamuuliza wewe unanizidi pesa kiasi gani ili unipe, hapana, anachukua hata kwa yule ambaye anajua hana kitu hata kama ni kwa mkopo uzilete ama sivyo nakufunga au hupati huduma fulani. Lakini ni lazima tutoe fursa ya watu kuishi maisha mazuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ulitupatia fursa ya kwenda Denmark, tulichojifunza na viongozi wengine wa Kamati pamoja na jirani yangu Mheshimiwa Omar Shabani Kwaangw', ni shahidi. Walitueleza kwamba kule rushwa ukisema rushwa wanashangaa kwa nini unasema rushwa hapa ni kitu gani? Watu wanashangaa. Tukauliza ni kwa nini mmeweza ninyi kuwa karibu *zero corruption infected,* wakatueleza kwamba ni hatua za muda mrefu katika historia yao kuhakikisha kwamba jamii inapata huduma zote inazostahili bure. Tena wakasema kwamba walipa kodi ni lazima walipe kodi kweli kweli kama wanapata mapato. *(Makofi)*

Lakini huyo mlipa kodi akishalipa kodi atibiwe bure, watoto wake wasome elimu bora bure kuanzia *kindergartens* mpaka Chuo Kikuu, wakifa wapewe huduma na mtu ambaye hana kazi apewe fedha ya kula. Sasa hiyo sisemi tujilinganishe na wao halafu kesho tuanze kufanya hivyo. Lakini nataka kushauri hapo kwamba tujenge uchumi wetu katika sera hii nzuri ya kukuza uchumi na kupambana na umaskini kwa kuongeza mapato ili tuwezeshe utekelezaji wa sheria hii. Kwa sababu uzuri wa sheria hii umo katika utekelezaji na wakishapata uhuru wakatekeleza wakiwa wametosheka vijana hawa Wilayani, Makao Makuu kuweza kushauri namna ya kudhibiti hii rushwa kubwa kubwa mambo yatakuwa mazuri kwa Taifa letu na nchi itakuwa inakwenda kwa kasi. *(Makofi)*

Nimalizie kwa kushauri tena, naomba Serikali muwaelimishe wafanyakazi wa umma yaani *Public Servants* juu ya sheria hii, wasije wakawa waoga, wapo wanatusikiliza tunapitisha sheria hii. Wengine huwa hawana hata muda wa kusoma sheria wakadhani tunapitisha sheria ya kuzuia watu kupata hela na kutajirika. Sheria yetu hii haizuii mtumishi kulima, kufanya biashara ili kutajirika kihalali. *(Makofi)*

Nawapongeza Taasisi ya Kuzuia Rushwa, huwa wanalirudia mara nyingi na Mheshimiwa Waziri nimemsikia akilisema kwenye semina kwamba haizuii mtumishi wa umma kuwa tajiri sana kihalali, kuwa na nyumba. Lakini isije watu wakaelekea kwenye kulewa ili asionekane na kifusi kwenye kiwanja akapelekewa fomu, hayo ndiyo tuliyokuwa tunasikia kwenye miaka ya 1970. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ilipoanza hiyo Taasisi ya Kuzuia Rushwa na sheria ya mwaka 1971 wazee wengine bila kuielewa ile sheria na kuisoma hawakujenga kabisa, lakini vile vile watumishi ambao hawaijui sheria katika utekelezaji walikuwa wanawasumbua sana, mtu anakunywa wanachukua vizibo wanawatisha mpaka kwenye bia wakaanza kuiogopa kuinywa. Akipeleka kifusi cha kokoto au mchango anapewa fomu ajieleze kwamba umepata wapi hela na kadhalika. Sasa waelimishwe watu tusije tukaweka *break* kwenye maendeleo. Vijana wakakaa maskini eti uadilifu ni kutokuwa na chochote. Hata kutokuwa na chochote na mshahara wako ni mzuri lazima tukuulize wewe hela unapeleka wapi? Milioni mbili kila mwezi wewe huna nyumba wala mlango, wala chuma, hata dirisha, ukasema nimeshindwa hapa hapa ukasaidiwa. Huna kitu unasema wewe ni muadilifu hata shati hubadilishi, kwa nini? Unasema mimi ni muadilifu, uadilifu gani huo? *(Makofi)*

Mheshimiaw Spika, kwa hiyo, tuwaelimishe watu wasije wakapotosha nia nzuri ya Serikali ya kujenga jamii ya uadilifu wakadhani Serikali inataka kujenga watumishi maskini ndiyo kigezo cha uadilifu. Hapana.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo nikushukuru tena kwa kunipa nafasi ya kuchangia, naunga mkono sana hoja hii ipite. Lakini Serikali isikilize ushauri mzuri wa Wabunge kwa kuanzia tunaweza tukaenda hivi. Mimi navutiwa na ulivyochukua marekebisho lakini kwa kweli ushauri uangaliwe. *(Makofi)*

Mimi kabla sijakaa sikufurahishwa kuondoa bodi eti kwa sababu ilileta utata namna ya kuiunda. Lakini mapendekezo mazuri yalikuwepo kwenye semina ya namna ya kuwachanganya watumishi wa umma na watu wa nje kufanya kazi pamoja na TAKURU. Sasa baada ya kusitasita mkaiondoa kabisa. Kweli inatia mashaka kwamba labda Serikali haina nia njema. Inakwepa kuipanua sheria kwenda kwenye sekta binafsi ambayo mimi najua kwamba siyo nia ya Serikali. Kwa hiyo, mliangalie hilo kwamba msiwaogope watu wa nje ya Serikali kuwa nao katika kuitekeleza sheria mradi tu wawepo na *Chief Secretary* siyo lazima awe Mwenyekiti wa hiyo Bodi. Mwenyekiti anaweza akatoka nje, mna mashaka gani? *Director General* ni mtumishi wa umma. Bungeni mtatuletea taarifa kupitia kwa Waziri. Hilo ni wazo zuri TAKURU wanapeleka taarifa kwa Waziri na Waziri analeta taarifa Bungeni kikao kinachofuata haraka *(immediately following session),* sheria imesema hivyo katika mapendekezo, naipongeza Serikali. Kwa hiyo, Bunge tutakuwa na uwezo wa kufuatilia wamefanya nini, wametoa taarifa kwa Serikali haraka iwezekanavyo. Kwa *DPP* ifanyike hivyo hivyo haraka kujibu TAKURU iwezekanavyo ili twende kwa *speed. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Masilingi. Kwa mpangilio sasa anafuatia Mheshimiwa Dr. Guido Sigonda, atafuatiwa na Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa na nadhani tutamalizia na Mheshimiwa Victor Mwambalaswa.

**MHE. DR. GUIDO G. SIGONDA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa hii nafasi na mimi nichangie kidogo katika huu Muswada ambao uko mbele yetu. Lakini kabla ya hapo naomba nitoe salaam za pongezi kutoka kwa wananchi wa Jimbo la Songwe kwa ndugu yetu Mheshimiwa Mtutura Abdallah Mtutura, kwa kupita kwake katika uchaguzi uliopita hivi karibuni. Nampongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi kwa kweli katika Muswada huu sina kubwa zaidi mbali na yale ambayo tayari yameshazungumzwa na Kamati pamoja na upande wa Upinzani pamoja na mwenzangu aliyezungumza sasa hivi.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa na suala moja tu kwa upande wa utekelezaji. Sisi Watanzania tunasifika sana katika kuandaa mipango, tunasifika sana, lakini tatizo linakuja katika utekelezaji. Utekelezaji ndiyo unaoturudisha nyuma. Kwa mfano, *PCB* haikuanza leo imeanza toka mwaka 1975 na ilikuwa na majukumu yake ya kiutendaji. Lakini leo hii tunaizidishia tena nguvu. Pengine ingekuwa ni vizuri tukajiuliza katika

hicho kipindi utendaji wake wa kazi wa hii Taasisi ulikuwaje? Nasema hivyo kwa sababu nafahamu kwamba ili tujue kama walifanikiwa ama hawakufanikiwa kuna vile vigezo ambavyo ni lazima tujaribu kuviangalia. Lakini jibu la haraka haraka ambalo linaonekana ni kwamba kwa kweli wametenda kazi yao kwa matatizo. Lakini mimi kwa upande wangu naona kwamba matatizo hayo yanaweza yakaainishwa katika aina mbalimbali, lakini aina mojawapo nina wasiwasi katika upande wa uajiri. Uajiri katika Taasisi nyeti kama hii ina utaratibu wake, huwezi ukaandika tu kwenye gazeti kwamba panatakiwa maafisa waje wajiunge na taasisi hii, haiwezekani! Upo utaratibu wake maalumu katika taasisi kama hii. *(Makofi)*

Kwanza kabisa jinsi ninavyofahamu mimi ni kwamba lazima kufanyika *spotting* ya *officer* ambaye anatakiwa kuingia katika hiyo kazi. *Spotting* ikishafanyika baada ya hapo haitoshi bado kufanyika *vetting* vile vile, sasa hiyo *vetting* ni kwa nini inafanyika? Inafanyika *vetting* ili kutaka kujua *background* ya huyu afisa ambaye tunamtarajia kuingia kwenye taasisi, inafanyika hivyo ili isije ikafika mahali tunamchukua mtu kwa sababu eti nafasi ipo. Hii taasisi ni nyeti, ni baadhi ya sababu ambazo zinazosababisha katika taasisi nyingi kutokufanikisha majukumu yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mbali na hiyo bado ukishaamini kwamba huyu ni kweli analingana na maadili ya Taasisi ndipo unamfanyia *recruitment,* ndipo unamuingiza na ukiishamuingiza bado haijatosheleza bado itabidi lazima huko kwenye kazi nako vile vile tufanye hayo ambayo mwenzangu Mheshimiwa Wilson Masilingi, alikuwa anayazungumza kuangalia hali ya afisa mwenyewe wakati akiwa kazini.

Mheshimiwa Spika, haya mambo bado mimi nayaona kwamba katika kuimarisha hii taasisi kufuatana na Muswada wenyewe ni vizuri kabisa tukakumbushiana kwamba vile vile vigezo na maadili ya kazi ni vizuri yakazingatiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la pili ni hivi karibuni kumekuwa na malalamiko dhidi ya Idara ya Polisi kwamba kumekuwa na kesi nyingi ambazo baadhi ya askari wanawabambikiza watuhumiwa. Wasiwasi wangu ni kwamba kwa sababu moja ya kazi ambazo zilikuwa zinafanywa na polisi ndiyo hizi ambazo tunazihamishia kwenye taasisi hii.

Mimi natoa rai tu kwamba pengine tusije tukafikia huko taasisi kutuhumiwa kwamba pengine inaamua kufanya vitu ambavyo ni tofauti ya maadili kumbambikizia kesi na kwa nini watu tunasema kwamba kuna kubambikiziwa kesi? Kuna sababu nyingi tu mojawapo ni chuki tu, pengine mtu uko kazini wewe ni *Director* pale kazini sasa kwa sababu ya chuki binafsi ndani ya watumishi wenzako anapeleka *report* taasisi. Sasa kitu kinachojitokeza pale ni *harassment*.

Mheshimiwa Spika, ninazumguza hivyo kwa sababu kuna mfano ambao ninao kama nitatakiwa kuutoa mimi nitakuja kuutoa, sehemu moja kuna Mkurugenzi mmoja yeye alikuwa anatafuta nafasi ya uongozi kwenye Bunge, utamaduni wetu Watanzania tuna ile dhana ya kusaidiana wakati wa raha na wakati wa shida. Huyu Mkurugenzi baada ya kuamua hivyo akaenda kuomba michango kutoka kwa wenzake kwa sababu

uchaguzi ni gharama. Wakajitokeza watu na marafiki, kwa bahati mbaya marafiki ambao walikuja wakachangia ni watu ambao wana nafasi zao na kutokana na kazi ya yule Mkurugenzi kidogo kuna mahusiano na kwamba ikaja fikra zingine kwamba hawa wamemchangia ili wawe wanapata *favour.* Yule Mkurugenzi aliitwa kuja kuhojiwa kwamba wewe umeomba rushwa kutoka kwa watu. Kitu kama hiki mimi nadhani ni kutokana pengine na mafunzo hafifu ya hao wanataasisi.

Mimi naomba kwamba tusije tukafikia hiyo hatua. Kwa kweli nia yetu ni ya kuimarisha hii taasisi, maana yake ni kwamba ni lazima tuzingatie yale maadili, tusiwe tunakwenda tu na kuingia tu. Ni vema tujue kwamba kuna unafiki, fitina na chuki, hilo vile vile litafanikiwa tukitambua kuwa tutawaandaa vizuri hawa maafisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika Muswada huu *section* ya 7 inampa uwezo Mkurugenzi kufanya utafiti, kutoa ushauri na kuchunguza kwenye sekta ya umma na sekta ya binafsi. Mimi bado sijaona hii sekta ya vyama vya siasa kwa nini yenyewe isiingizwe? Kwa nini isitamkwe? Hii sekta ya mashirika ya dini kwa nini isiingizwe humu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukifuatilia sawa sawa katika upande wa vyama kuna matatizo mengi sana yanayojitokeza, unaweza kuona kwamba pengine hii rushwa tunayoipigapiga kule inawezekana pengine inaanzia kule na mifano tunayo, sasa hivi mtu kama anatafuta nafasi ya uongozi kupitia kwenye chama chake ni lazima uwe na nguvu kweli kweli, vinginevyo unaweza ukadondoshwa eti kwa sababu huna uwezo, ni rushwa ile! Siyo kitu kingine ni rushwa ile. Mimi nilikuwa naomba huu Muswada ujaribu kupitiwa uone kwamba hii inaweza kuwa ni *source,* vile vile tunaweza kuwa tunapiga piga hapa lakini huko? Tutafute chanzo cha hili tatizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi sikisemi chama chochote kile, lakini nilikuwa nafikiria kutokana na uzoefu naona kwamba vyama vya siasa navyo vingeangaliwa yaani apewe uhuru huyu Mkurugenzi ili avipitie pamoja na mashirika ya dini. Sasa hivi tuna mashirika ya dini chungu mzima unakuja kuona leo limeibuka halafu baada ya muda unakuja kuona kwamba wanatajirika! Hii inatisha! *(Makofi)*

Kwa mfano, kuna shirika lingine yaani kiongozi kwenye Mahakama kwenda kukata rufaa ni kitu cha kawaida, hela anazipata wapi? Zinapatikana wapi hizo hela? Haya maeneo ambayo ni madogo sana lakini mimi nilikuwa nafikiri kwamba ili kusudi kuipa nguvu hii taasisi basi tuipe uwezo vile vile wa kuweza kupenyeza katika maeneo hayo. Kwa sababu mengi yamezungumzwa nilifikiri kwamba nizungumzie kwa ufupi hayo tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ahsante sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana, kama nilivyosema sasa namwita Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa, atafuatiwa na Mheshimiwa Victor Mwambalaswa. *(Makofi)*

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi, naomba niungane na wenzangu awali ya yote katika yote waliyoyasema lakini nitofautiane na baadhi yao katika kuunga mkono Muswada huu na kabla sijasahau

niseme kabisa kwamba sitaunga mkono Muswada huu isipokuwa tu kwamba pale nitakapopatiwa maelezo ya kutosheleza wakati wa majibu ya Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa niseme kwa nini siungi, mkono siungi mkono kwa sababu kadhaa nzito. La kwanza, Muswada huu unangojewa sana na Watanzania na kwa kuwa Watanzania wote wanachukizwa na rushwa wanaamini na Serikali yao pia inachukizwa na rushwa kama na wao wanavyochukizwa na rushwa na kwa msingi huo wanategemea kuona sheria ambayo ina meno tofauti na sheria iliyopo sasa. *(Makofi)*

Sasa mimi niende moja kwa moja kwa kusema kwamba sheria hii ukiiangalia juu juu kwa mtu ambaye hujasoma kwa makini utaona kweli inatoa meno *PCB,* lakini kwa msomaji makini aliyesoma vizuri sheria hii akaunganisha na nyingine za nchi hii na akaunganisha na marekebisho yaliyoletwa akasoma na mapendekezo ya wadau ataona kabisa kwamba Muswada huu haukuleta kitu chochote kipya kile kidogo kinachoonekana kwenye vifungu vya hapa vikachukuliwa kwa mkono mwingine na sheria nyingine. Kwa hiyo, tulichopata hatunacho hapa, natumia mfano wa kilichotumika kwenye Katiba tunatoa haki kwa mkono tunaondoa kwa *claw back* kwa mkono mwingine na tulichofanya hapa ndicho hicho kwa hiyo, hatujafanya kipya chochote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la kwanza kabisa ni suala ambalo tulilipigia kelele kwenye Kamati, wadau wamepigia kelele, *APNAC* wamepigia kelele. *APNAC* ambao ni Mtandao wa Wabunge na niseme tu kwamba ni kweli inaonekana katika *schedule of amendments* kuna mengi yamechukuliwa. Naomba niseme katika *page 7, page* zaidi ya nne zinashughulikia masuala ya faini na masuala ya faini hakuna mtu mwenye utata nayo na bado tuna tatizo kwa sababu faini bado ziko ndogo katika makosa makubwa na nitayaeleza. Lakini yale mengine yote mazito yaliyotajwa hakuna hata moja ambalo limewekwa hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la kwanza kabisa ambalo nataka niliseme ni suala la *DPP,* hakuna maelezo ya kutosheleza na hoja ya kwamba mamlaka ya *DPP* ni ya Katiba ni wimbo ambao unataka kuinyima taasisi hii haki zake na nguvu yake na madaraka yake, kwa sababu kazi tunazopendekeza humu ni kazi zile zile. *TRA* leo inaweza kumpeleka mtu Mahakamani haihitaji tena kibali cha *DPP,* kwa nini Mkurugenzi wa *PCB* ahitaji kibali cha *DPP?* Serikali isifanye vitu *double standards, TRA* inakwenda kushitaki haihitaji mamlaka yoyote wala kibali chochote kwani huyu mtu ana tofauti na huyu kama sisi tumedhamiria kutoa madaraka kwa chombo hiki na tunataka kupiga vita, kwa nini tusimpe huyu Mkurugenzi madaraka akaachana kabisa na kibali cha *DPP?* Serikali itupe taarifa ya kuridhisha katika hilo. *(Makofi)*

La pili, suala la Mamlaka ya *DPP* wakati wowote kuingiza hati ya kufuta kesi na hatakiwi kueleza sababu, hiki ni kikwazo. Mwanasheria Mkuu wa Serikali pamoja na *Parliamentary Draftsman* kwenye Kamati walitueleza kwamba tumechukua mfumo huu kutoka Uingereza, huu ni wimbo ambao pia unatudanganya Bunge hili, kuna mengi tumechukua Uingereza na mengine tukaacha na mengine tukayatumia kwa hiyo tusitumie kisingizio kwamba haya mambo yote yanayofanana katika nchi zote za *Commonwealth.* Yale yanayotufaa tuyachukue yasiyotufaa tuachane nayo, madaraka ya *DPP* yanaleta

kikwazo kwa sababu *DPP* anaweza kuingiza *Nolle prosequi* katika kesi ambayo huyu Mkurugenzi ameianzisha na ikafutwa na hatakiwi yule bwana kutoa sababu yoyote, hiki ni kikwazo kikubwa, haina dhamira yoyote ya kupiga vita rushwa katika suala hili.

La tatu, katika suala hilo hilo ni mamlaka ambayo vilevile DPP anapata, sisi tulisema sawa kama mnang'ang'ania basi ni ya Katiba, basi angalau apewe muda aeleze sababu ya kuiingiza ile *Nolle prosequi,* hivi Serikali inapata kigugumizi gani kuweka hata muda kwamba ndani ya siku 60 aeleze kwa nini alifuta kesi. Hivi hapa kuna kigugumizi gani? Ile ya Katiba sawa tusema tuiruhusu na mimi sioni kama ni ya Katiba kwa sababu tayari *TRA* inafanya. Sasa kuna tatizo gani hapa na Ibara inayozungumziwa ya Katiba 59(2) kila mtu anaisoma. Inatoa mamlaka kwa *DPP* kuzisimamia hizo kesi hata akifanya kazi huyu haimkatazi kwenda kujua nini kinafanyika kule. Ni vitu viwili tofauti, lakini hakisemi kwamba yeye lazima atoe kibali kwa kila kesi na hilo neno la kibali mimi sijaiona kwenye Katiba. Nadhani hapo tuna tatizo nzito sana kama tuna nia ya kupiga vita rushwa kweli katika nchi yetu. Niache suala la *DPP.*

Mheshimiwa Spika, suala zito lingine ni suala la *transparency* katika mamlaka ya uteuzi wa huyu bwana. Ni kweli tunasema Mheshimiwa Rais kwa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ndiye anayeteua wakuu wote wa Idara mbalimbali za Wizara na kadhalika. Mimi sina tatizo na hilo. Lakini hatuzungumzii suala la uteuzi wa mwisho. Nchi hii tumefanywa kama hatujui kama kuna *models* zipi duniani. *Model* tunayoizungumza si lazima Rais aache kuteua huyo bwana. Hivi kuna tatizo gani kuwa na *panel* kwa mfano ya Majaji au hata Kamati ya Bunge ikapendekeza majina matatu Rais akateua, *loyalty* ya yule bwana haitakuwa kwa Rais tu, itakuwa kwa Bunge pia. Hapa kuna shida gani? Tatizo liko wapi? Kwa nini Serikali haitaki kuliona hili? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri ametueleza kwamba hii ni taasisi ya Serikali. Kwa kueleza kwamba hii ni Idara kama Idara nyingine za Serikali ametuhakikishia kwamba hakuna *independence* inayozungumziwa katika kifungu cha 5 na kwamba hiyo kifungu cha 5 ni kiini macho. Tukubali kabisa kwamba kifungu cha 5 katika sheria hii ni kiini macho kwa sababu mtu mwingine ambaye hasomi ndani anasema ni kweli taasisi hii ni uhuru na kama hawaoanishi na hizo sheria zingine ataona ni uhuru. Lakini kwa mtu anayefanya tathmini, anayefanya *analysis,* anayeunganisha sheria anaiona *obligations* ya hizi sheria zinavyoingiliana, anaona kabisa ule uhuru umeondolewa.

La pili, katika suala hilo ni suala la *security of tenure*. Huyu ni mtu anayeenda kuchunguza rushwa hata katika ofisi nyeti kama Rais, Rais labda hatachunguzwa akiwa bado madarakani, *procedure* zake zitafuatwa. Lakini watu wake wanastahili kuchunguzwa wote na Katiba inasema Rais ndiye hatachunguzwa akiwa madarakani, wengine wote wanastahili kuchunguzwa. Hivi ni kweli kwamba huyu mtu kama hana *security of tenure,* akianza kumchunguza mkubwa yeyote chini ya Rais, hivi usalama wake uko wapi. Nchi zote zinazojali kwamba *watch dog instruments* ni lazima zitenganishwe na *Executive* kwa sababu hiyo. Kwa sababu mwenye kumteua ana

mamlaka ya kumwondoa akiona kwamba kuna chuki wakati wowote. Tusipofanya hivyo hakuna dhamira ya kweli.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri asiponipa jibu sahihi katika hili, tunaogopa nini? Ni kweli ni taasisi ya Serikali na hata kwa kumpa *security of tenure* kama tulivyowapa Majaji. Tumempa Mwenyekiti wa Haki za Binadamu, hivi tunashindwa nini kumpa huyu apate *security* akiteuliwa kuwa na *elaborate procedure* ya kumwondoa? Mimi sisemi asiondolewe akifanya makosa aondolewe. Lakini aondolewe kwa taratibu zilizo *transparent* ambazo zinamlinda kwamba mpaka afanye hayo kweli anajua sasa anaweza kuondolewa. Bila hivyo Muswada huu haujaleta kipya na hautafanya makusudio ambayo Watanzania wanayategemea. Bunge hili tutaonekana kwamba tumepitisha tu kama tunavyopitisha mengine.

Mheshimiwa Spika, la mwisho amelisemea ndugu yangu Mheshimiwa Wilson Masilingi, sitaki kulirudia la *financial independence,* lakini niweke tu msisitizo kwa sababu amelieleza vizuri sitaki kulirudia.

Mheshimiwa Spika, ningependa sasa nigusie kidogo suala la Bodi ambalo Waziri amelifuta katika *Part Three* kwenye sehemu ya tatu ya Muswada. Inaonekana hapo Serikali inasikiliza wadau. Jana katika Kamati nilieleza sina hakika ya tafsiri ya kufuta, sasa usiku nime-*reflect* na nimepata maelezo yangu kwamba kitendo cha kufuta siyo kitendo cha kusaidia Muswada. Wadau hawakupendekeza tu ifutwe kwa sababu kwenye kifungu hicho ndiyo *role* ya *civil society* inaanza kuonekana kwa sababu kwenye wajumbe wa bodi ndiyo kulikuwa na *element* ya watu wa nje kuanza kujua na kuanza kusaidia hasa kwenye elimu.

Mheshimiwa Spika, mifano iko mingi tu tusisemi sisi ni nchi ya kwanza, yeyote anayeweza kuingia kwenye mtandao naomba aingie Mauritius ni mfano, kuna bodi tatu, kuna moja tu inashughulikia elimu na inahusisha watu wa nje kabisa wala siyo vyombo vya Serikali. Kwa sababu wale ndiyo wana uwezo, wanajua wanaishi na watu wanaopokea na kutoa rushwa. Sasa sisi tunashindwa nini, mifano iko mingi tufanye kazi. Waziri ametoa mfano wa *SCORPION* jana, lakini *SCORPION is independent* inaripoti hata Bungeni. *SCORPION* ni chombo kama chetu, cha Afrika ya Kusini kinaripoti Bungeni na ndiyo maana kiliweza kikamshughulikia Makamu wa Rais, baada ya kumshughulikia Mahakama iliona hakuna kitu, mambo yameendelea.

Mheshimiwa Spika, mimi nilikuwa nafikiri kama tuna nia ya kweli ni lazima katika taratibu zetu, chombo hiki kinachoitwa Bodi hata kama tukiacha basi tupate ushiriki wa watu wa nje *civil society, NGO's,* madhehebu ya dini na nini wanajua kabisa.

Mheshimiwa Spika, nitatoa mfano, na naomba niurudie ndani ya Bunge lako Tukufu. Nilitoa mfano kwamba mimi niliombwa na *PCB* ya nyuma siyo ya sasa niende nikasaidie kumkamata mtu kwa bahati nzuri mimi nilikuwa mkubwa huko nyuma. Tulimkamata huyo mtu tumemfikisha *PCB,* njiani aliruka kwenye gari langu karibu ajiue. Siku tatu haijafika yule akaachiwa. Sasa najiuliza hivi tunapokuwa hatuna vyombo vingine vya nje vya ushauri, hivi hii *PCB* ni takatifu kiasi gani hata yenyewe. Tunahitaji

sisi kuwe na *watch dog,* chombo hiki ili kusiwe na malalamiko tena kwamba kuna kesi fulani ya kigogo fulani imeachwa *at least* kuna *information* mahali, kuna watu wanaolinda *interest* ya watu wa nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tusipofanya kitu cha namna hiyo na Waziri asiponieleza kwa nini tunamwogopa huyu tunataka zile taratibu za kawaida, anasema *reporting* ile ya kawaida tunaripoti kwenye Kamati za kawaida za Bunge, kuna kosa gani na kuna kasoro gani. Nasema kosa hakuna kwenye taratibu zile, lakini haitoshelezi. Kwenye Kamati tunaripoti zile taarifa za kawaida, tuna *procedures* hizo zote ziweze kuwa *at wide scope* wananchi wote waweze kushiriki kwa njia yoyote wanayoweza, wapate hata watu wa *PCB* utajiri wa mawazo yanayotoka nje. Chombo kiwe na uhuru wa kufanya kazi na kisiingiliwe katika utendaji wake. Hilo sina tatizo nalo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilifikiri vile vile kuna haja ya kusema suala la faini. Suala la faini ni kweli wamelifanyia kazi sana. Lakini nataka kutoa mfano, hivi kama ni kweli tunayosomwa kwenye magazeti mtu aliyechukua rushwa ya bilioni 12 ya Rada ile kwa namna yoyote atakavyoeleza kama ilivyokuwa kwenye magazeti. Hivi yule mtu akiona ni faini ya shilingi milioni 15 kama ilivyo kwenye Muswada wetu. Hivi inamzuia nini kupiga hesabu na kusema hivi nikichukua bilioni zangu 50, milioni 15 nikatoa anaipigia mahesabu na akachukua rushwa yake akaenda kulipa ile faini na akahesabu mtiririko mzima. Milioni 15 haitoshi kwa kesi kubwa, ni lazima katika Muswada huu tutenganishe kesi nzito au tuhuma nzito ziweze kuwa na faini nzito na kesi za mtu wa kawaida ziende kwa uwezo wa mtu wa kawaida. Bila kufanya hivyo hiki tulichokifanya hakisaidii, jana Waziri na wataalam wake tuliwaeleza sana tulidhani walituelewa, lakini naona imerudia hivyo hivyo.

Mheshimiwa Spika, la mwisho ambalo nataka kuligusia ni rushwa katika uchaguzi. Kama tulivyowahi kusisitiza Watanzania wengi wanapiga kelele kwamba kuna rushwa katika uchaguzi, hakuna atakayekataa hili. Anayetaka kukataa akatae tu, lakini kuna rushwa katika hili ni suala lilo wazi.

Sasa Waziri anaponiambia kwa sababu kuna mchakato wa kutengeneza sheria na nini, mbona tuna sheria ya ngono, humo tumeweka tu *paragraph* moja, inayogusia kwamba huyu bwana atakuwa na uwezo. Lakini katika kuitekeleza atatumia ile sheria ya *Sexual Offences*. Mbona kuna sheria ya ajira, mbona kuna sheria ya mikataba, mbona kuna sheria nyingine nje, hivi inakataza nini katika hili tukiweka *paragraph* inayoruhusu mtu huyo aweze kuingia kwenye vyama vya siasa. Lakini *details* zake tukapata kwenye mchakato ambao unakuja baadaye. *Principle* kuitamka kwamba *PCB* ina mamlaka nayo hata ya kuingia kwenye kesi za siasa, hivi inazuia nini? *Principle,* hatuzungumzi hapa aorodheshe kama ambavyo hakufanya kwenye ngono hakuorodhesha makosa ya ngono. Hata kwenye ajira hakuorodhesha yale makosa yote ya *criminal offences* katika ajira na mikataba. Lakini yale unayapata kwenye sheria nyingine.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri kwenye sheria atakayofanyia *amendments* atatuletea *details* hizo, lakini kwenye hii tunataka huyu bwana asifungwe mkono, awe na mamlaka, aingie kwenye uchaguzi, aingie ndani ya Vyama vya Siasa,

aingie kwenye madhehebu ya dini, aingie popote pale, huyu rushwa popote ilipo ndiyo eneo lake. Tusimwekee mipaka kwa kusema rushwa itakuwa eneo fulani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nimalizie kwa kusema ni kweli kwamba suala la rushwa linatugusa sote. Ni kweli hata Rais anaguswa. Nilikuwa napitia taarifa ya *Auditor General* hivi, Serikali yote iko chini ya Rais na Rais wetu ni *Executive President*. Hapa unakuta *un-vouched* zipo zaidi ya shilingi bilioni 67, unakuta matumizi yasiyoelezwa bilioni mia mbili na kitu. Hata lile deni la Taifa la shilingi bilioni 11, deni la Taifa *of all things* mimi nimeshtuka sana leo, deni la Taifa limekosa rikodi. Sasa tunapopeleka tukasema Rais ndiyo peke yake tunamwamini.

Mheshimiwa Spika, tukumbuke kwamba hatumzungumzii Rais Jakaya Mrisho Kikwete, tunazungumzia Rais wa Tanzania ya leo na wa kesho na wa kesho kutwa. Nchi zote duniani ambapo rushwa imekuwepo hela za nchi zimepelekwa kwenye akaunti za nje, waliopeleka siyo watu wadogo ni watu wakubwa. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kumalizika muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge, kengele ya pili, ahsante sana. Sasa namwita Mheshimiwa Victor Mwambalaswa, nadhani ndiye atakuwa msemaji wa mwisho kwa mchana huu. Halafu akimaliza nitatangaza majina ya wale wataofuata kuchangia saa 11.00 jioni.

**MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili nami niweze kuchangia katika Muswada huu ulio mbele yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwanza, kwa niaba ya wananchi wa Chunya napenda nitoe pole na rambirambi kwa familia ya Marehemu Dr. Aaron Chiduo, natoa salaam za pole na rambirambi kwa familia yake na wananchi wa Gairo.

Mheshimiwa Spika, pili napenda nichukue nafasi hii kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wenzetu ambao wameingia Bungeni hapa kwa mara ya kwanza. Kwanza, Mbunge wa Viti Maalum kutoka Mbeya, Mheshimiwa Florence Kyendesya na Mbunge wa Jimbo la Tunduru Mheshimiwa Mtutura Abdallah Mtutura. Nawapongeza sana na kuwakaribisha tufanye kazi ya wananchi pamoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tatu, napenda nimpongeze sana mtoa hoja, maana yake hoja hii ni ya muhimu sana kama Serikali itataka kutimiza ajenda yake iliyo mbele ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005.

Mheshimiwa Spika, mimi nataka niongelee suala moja muhimu kwangu ninavyoona. Mimi nadhani nyakati hizi kwa Serikali hii ya Awamu ya Nne na Serikali ya Awamu ya Tatu, mdudu anayeila sana Serikali na kuipunguzia heshima ni manunuzi ya umma *(Public Procurement)*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nadhani kwamba sheria ya manunuzi ya umma ya mwaka 2004 ina mashimo ambayo mdudu huyo anapenya na kuweza kuila Serikali na kuipunguzia heshima. Nitatoa mifano. Kwa mfano, tuchukue manunuzi ya vitu vinavyofanana *(common items)*. Wizara inayohusika inaenda kununua *computer* dukani siku hiyo hiyo, Wizara nyingine inaenda kununua *computer* hiyo hiyo dukani, Wizara nyingine inakwenda kununua *computer* hiyo hiyo dukani na siku moja hiyo hiyo vitu vinavyofanana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitatoa mfano, mwaka jana Serikali iliwakopesha Waheshimiwa Wabunge fedha za kununulia magari. Kuna Waheshimiwa Wabunge kama 100 wakaamua kwamba wao watanunua *Toyota,* wakaenda *Toyota,* kwa sababu namba yao walikuwa 100, waka-*negotiate* na mtu wa *Toyota* kwamba bwana wewe unasema *Land Cruiser* yako hii shilingi milioni 40, sisi tunasema shilingi milioni 35 tuko watu 100 unasemaje, akasema ndiyo nitawapa. Kwa hiyo, kila Mbunge afanya *saving* ya shilingi milioni 5 kupata *Land Cruiser GX.* Kwa Waheshimiwa Wabunge 100, nadhani Waheshimiwa Wabunge wenzangu wanaweza kunisaidia. Waheshimiwa Wabunge 100 mara 5 ni milioni 500. Ingekuwa ni Serikali hizi fedha zingesaidia kujenga madarasa ya shule za sekondari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali nayo mwaka jana imenunua magari ya Serikali yaani kila Wizara imenunua magari ya Serikali, gari la Waziri na gari la Naibu Waziri. Kila Wizara imeenda kununua gari *Toyota,* kila Wizara imenunua *Toyota,* imenunua *GX* na nyingine imenunua *VX* na magari ya Makatibu Wakuu. Magari 60 kwa sababu Mawaziri wapo 60. Je, nao wangeweza nao waka-*negotiate* wapunguziwe angalau milioni 3 au milioni 5 zingepatikana milioni 300 zikaenda kujenga madarasa ya shule za sekondari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wangu mimi, naona hii ya kununua mmoja mmoja vitu vinavyofanana kwanza inapunguza *uniformity* Serikali ni hiyo hiyo moja. Waziri huyu ana gari la *GX* au huyu ana gari la *VX,* Naibu Waziri huyu ana gari la *GX* na huyu ana gari la *VX,* haya magari ni tofauti, *GX* ni *GX* na ni tofauti n *VX* inapunguza *uniformity.*

Mheshimiwa Spika, lakini pili, inaongeza mianya ya rushwa kwa sababu mkienda kama timu ku-*negotiate* ni tofauti na kwenda mmoja mmoja. Anajua huyu ni mmoja anaweza akampa rushwa akapokea. Nadhani inaongeza mianya rushwa. Hilo moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la pili, manunuzi ya vitu vikubwa vya bei kubwa na bei ndogo, hii sheria ya manunuzi inasema Idara, Wizara na Wakala wana kikomo cha milioni 50 kwenye manunuzi ndiyo kikomo chao. Baada ya hapo inaenda *Ministirial Tender Board*. Lakini ikienda kwenye *Ministirial Tender Board* ninavyojua ni kwamba Waziri mwenye dhamana ndiyo analivalia njuga suala hilo, yeye ndiye anaamua, anapeleka kwenye *cabinet* kwenda kutoa taarifa tu. Sasa hii ina hatari sana kwa vitu vikubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ndiyo maana mmeona kwenye siku za karibuni watu wa mitaani, kwenye daladala na kwenye vyombo vya habari vinaongea Serikali ilinunua Rada, Serikali ilinunua ndege, Serikali imeingia kwenye mkataba na *Richmond*. Mimi nampongeza Waziri ambaye siyo mtaalam wa ununuzi anaenda kufanya manunuzi. Sana sana mtu akikwambia bwana utakuwa mhasibu wa Wizara hii wakati wewe ni Mwanasheria, utafanya kidogo ile kazi ya uhasibu inabidi umpongeze. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali iheshimu taaluma ya ununuzi ili wataalam waishauri Serikali pale inapotakiwa kununua vitu vikubwa na vya bei kubwa ambavyo vinaileta Serikali gharama. Naiomba Serikali haya yamepita, lakini la *Richmond* sijui kama limepita na kuhusu Rada. Kuhusu ndege ya Serikali imepita. Lakini yako makubwa yanakuja. Kuna Mchuchuma inakuja Waziri mwenye dhamana akienda kichwa kichwa peke yake italeta maneno baadaye. Vitambulisho vya Uraia vinakuja navyo ni mradi mkubwa sana. Naiomba Serikali ichukue tahadhari mapema ili maneno ambayo yameipunguzia heshima Serikali yapungue. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ndiyo maana katika ripoti ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali ni Wizara na Idara 40 ambazo zimepata hati safi. Wizara na Idara 27 zimepata hati za mashaka na Wizara na Idara tatu, zimepata hati chafu. Lakini hizi Wizara na Idara ambazo zimepata hati ya mashaka na hati chafu tutakaa mwezi Juni, tutapitisha mafungu na tutawapelekea tena *Accounting Officers* wale wale ili waendelea tena kutuletea hati chafu na hati za mashaka. *(Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naiomba Taasisi hiyo itakayoanzishwa ya kuzuia rushwa, watu wa kushughulikiwa wa kwanza wawe wale ambao wanapata hati ya mashaka na hati chafu. *(Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nataka niongelee tena manunuzi katika Halmashauri. Kwa ridhaa yako naomba ninukuu inavyosema sheria ya manunuzi Ibara 28(3), *"the composition of local government authority tender board and method of appointment members and procedures to be followed by such tender board shall be prescribed in regulations made persuant to the provisions of section sixty five of the local Government Finance Act, 1992."*

Mheshimiwa Spika, sheria hii inayosema kwamba hiyo *tender board* ya *Local Government* itafanya *regulations* bado hazijatengenezwa hazipo. Kwa hiyo, sasa hivi kwenye *local government* wanafanya manunuzi kwa kuelea tu, hawana *regulations,* hazijatengenezwa. Namwomba Waziri mwenye dhamana hiyo afanye haraka *regulations* hizi zitengenezwe, wapelekewe watu wa *Local Government* ili waweze kununua kwa kufuata sheria.

Mheshimiwa Spika, ndiyo maana katika ripoti ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali ya mwaka jana, Halmashauri saba zilifanya manunuzi bila kufuata zabuni ya ushindani na zilipoteza shilingi milioni 800. Halmashauri 5 zilifanya ununuzi bila idhini ya Bodi ya Zabuni na zikapoteza shilingi milioni 380.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mimi napenda nisisitize hapo kwamba sheria ya manunuzi ya mwaka 2004 inahitajika kufanyiwa marekebisho makubwa ili iweze kuisaidia sheria ya kuzuia rushwa ya mwaka huu. Najua kuwa Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete ana ajenda nzuri kwa Watanzania, anataka kuleta maisha bora kwa kila Mtanzania akimaliza kipindi chake. Najua kwamba Serikali ya Awamu ya Nne, yenye ari mpya, nguvu mpya na kasi mpya ina nguvu zinazoweza kuitekeleza ajenda hiyo. Lakini kama mdudu huyo ambaye anaila Serikali kwa chini *Public Procurement* asipoangaliwa, Serikali imeingia madarakani ikiwa kifua mbele, inaweza ikatoka madarakani ikiwa kifua chini kama haitaangalia mdudu huyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, mimi naomba kuunga mkono Muswada huu na ninashukuru sana. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Mohamed Rished Abdallah, unaweza ukatumia dakika 10? Inatosha.

**MHE. MOHAMED RISHED ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Nilijua sitochangia tena nikaanza kufungusha makaratasi yangu kwa ajili ya jioni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kabla sijampongeza Waziri, nami niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwa kutoa salaam za rambirambi kwa familia ya Marehemu Dr. Aaron Chiduo, aliyekuwa Mbunge mwenzetu. Mungu ailaze roho ya marehemu mahali pema peponi. *Amin!*

Mheshimiwa Spika, taarifa ya Mheshimiwa Waziri juu ya Muswada huu ni nzuri na ninaamini sasa Tanzania tumeanza kuona kwamba rushwa kwa kweli ni adui wa haki na Serikali imeona kwamba sasa kuna haja ya kubadilisha au ku-*amend* sheria zetu ili ziwe na meno zaidi hatimaye wananchi wapate haki zao sawasawa kama Katiba inavyosema.

Mheshimiwa Spika, lakini kabla sijasema lolote, mimi nataka Mheshimiwa Waziri atupe ufafanuzi mdogo kwenye Katiba yetu Ibara ya 46(3) inazungumzia juu ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, nanukuu: "Itakuwa ni marufuku kumshitaki au kufungua Mahakamani shauri lolote la Jinai au la kumdai mtu aliyekuwa anashika madaraka ya Rais baada ya kuacha madaraka hayo kutokana na jambo lolote alilofanya yeye kama Rais wakati alipokuwa bado anashika madaraka ya Rais kwa mujibu wa Katiba hii."

Mheshimiwa Spika, lakini sasa katika Ibara ya 4 ya sheria tuliyokuwa nayo inampa mamlaka Mkurugenzi Mkuu kumshitaki mtu yeyote. Sasa Rais akishamaliza shughuli zake za Urais atakuwa ni raia wa kawaida katika nchi hii japokuwa heshima yake ya Rais Mstaafu itakuwepo. Lakini amekuwa ni raia wa kawaida. Lakini sisi tukifuata mifano ya nchi mbalimbali duniani, kuna mambo mengine ya kulipiza kisasi kwamba safari hii nikishika mimi Urais basi Rais fulani ataniona. Sasa sheria hii mimi naona kama inagongana na Katiba, ni vyema sheria ikawa ipo wazi, angalau basi kukawa na kipengele kinachosema isipokuwa bila ya kuathiri Ibara ya 46(3) ya Katiba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa sababu hizi sheria sisi tunazipitisha kama sheria mama, zikifika kwa wataalamu wanaanza kuzichambua na kuziwekea kanuni na tafsiri na kila kitu. Sasa hapo sisi baadaye tunakuja kuambiwa, lakini si mlipitisha nyie wenyewe Wabunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa hili hebu walitazame tusije tukatumia sheria hii mwanya mdogo tukaja tukaathiri mambo mengine ambayo hayana sababu, tunayo mifano mingi katika Bara letu la Afrika. Marais walioheshimika kabisa wamekuja kudhalilishwa kwa mambo mengine ambayo hayana msingi, yakaleta vurugu katika nchi na hatimaye kukawa hakuna mwelekeo mzuri na amani katika nchi mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, mimi leo nitatuzungumzia mifano, lakini Taasisi hii itazame kesi mbalimbali ambazo zimekwishaanza kushughulikiwa, hatimaye tuondoe dhana ya kwamba Taasisi nayo labda inapokea rushwa, yenyewe ni Taasisi ya kuzuia rushwa, halafu tukapata dhana kwamba mbona haya mambo hayaendi. Ndiyo kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge mmoja hapa mwenzangu kwamba kuwe na *watch dog* au mimi niite kwamba kuwe na *anti-corruption*. Sasa hii inafanyika duniani kote. Wao ni binadamu siyo malaika, wako wengine wanafanya kazi zao kwa uadilifu kabisa. Lakini wako wengine walitaka waajiriwe na *PCB* ili na wao wanufaike kwa kutumia taratibu za rushwa. Hiyo inafanyika duniani kote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa nilimpelekea Mheshimiwa Waziri barua mwaka jana kuilalamikia *PCB* juu ya mtumishi mmoja katika Halmashauri ya Wilaya ya Pangani na nikaambatanisha maelezo ya matatizo yaliyokuwepo humo ndani na nina hakika Waziri aliwapelekea watu wa *PCB* waifanyie kazi. Mpaka sasa hivi Mheshimiwa Waziri hajanipatia majibu. Mimi ninaamini kwamba wataalamu wake bado hawajampa taarifa ndiyo maana yeye hajanipa mimi taarifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa hapa na mimi naanza kuweka alama ya kuuliza? Kwa nini hii kesi haiishi? Ni mtumishi mmoja wa hospitali ya Wilaya ya Pangani anaitwa ndugu Kiparo, nitaje na jina kabisa.

Mimi naona mtumishi yule amesimamishwa kazi na ni mtu ana familia na watoto na mke, leo mwaka wa tatu, hajarudishwa kazini wala hakuna maelezo yoyote ya kusema kwamba kosa lake nini, mbona kesi yake haipelekwi mahakamani. Ingekuwa ni suala limefikishwa Mahakamani baada ya siku 60, kesi ile ingefutwa kwa sababu inaonekana ushahidi hakuna na juzi tumelizungumzia hapa katika sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa mimi nauliza kuna tatizo gani la ndugu Kiparo? Kwa nini kesi yake haiishi? Kesi hiyo inashughulikiwa na *PCB,* kesi hiyo inashughulikiwa na Polisi, sasa nani mwenye maamuzi hapo? Ukienda Polisi wanakwambia hii kesi ipo *PCB* wanafanya uchunguzi, ukienda *PCB* wanasema bado hawajapata vielelezo vya kutosha mpaka lini.

Mheshimiwa Spika, kama havipatikani vielelezo ni kwamba huyo mtu ameonewa na ameonewa na nani, ameonewa na watumishi wakubwa wake katika Halmashauri

waliokuwa na visa na sisi wanasiasa tumeingia humo ndani kwa sababu zisizoeleweka za chuki na hatimaye hao wakubwa wake nao wamesimamisha kazi. Hivi leo na wao hawako kazini kwa sababu na wao wanatuhuma za ubadhirifu wa fedha na wengine bado sasa wamepelekwa huko huko *PCB*. Sasa bado *PCB* haioni kwamba ule ulikuwa ni uonevu? Sasa mifano kama hii ndiyo mimi nasema kuna nini? Kwa nini hizi kesi haziishi? Sasa mifano kama hiyo inawatokea wananchi wengi katika nchi hii wanatuhumiwa mambo lakini kesi hazimaliziki.

Mheshimiwa Spika, ninamwomba Mheshimiwa Waziri bado afuatilie na Mkurugenzi Mkuu amenisikia hapa hebu fuatilia kesi ya Kiparo mimi nina *interest* nayo kujua, hivi tatizo ni nini *PCB* au Polisi?

Mwisho kwa dakika moja iliyobaki na mimi niungane na msemaji mmoja kwamba sasa hivi faini zilizozungumzwa hapa zilingane kwa asilimia ya *corruption* iliyofanyika. Badala ya kusema shilingi milioni 15. Sasa iwe ni asilimia, wewe umechukua shilingi bilioni 15 kama rushwa, basi ni asilimia 75 ya shilingi bilioni 75 ndiyo ulipe faini. Hii itasaidia mtu akitaka kuchukua rushwa kwa sababu anajua faini atakwenda kupigwa kwa thamani ambayo imesemwa amekula rushwa ya mabilioni ya fedha basi alipe faini ya mabilioni kadhaa ya asilimia 75 ya rushwa. Hii inaweza ikasaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na ninaunga mkono Muswada huu. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, muda wa kusitisha shughuli za Bunge kwa mchana huu ndiyo umewadia. Napenda nimshukuru sana Mheshimiwa Mohamed Rished Abdallah, Mbunge wa Pangani kwa kweli ametumia dakika 10 tu. Nilikuwa tayari hata nisimame nimwombe apate dakika 5 saa 11.00 jioni. Lakini naona *point* kubwa sana ya mpigakura wake amekwishaisema na nadhani inatosha. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, sasa wasemaji kwa mpangilio ili wajiandae kwa kipindi cha saa 11.00 jioni tutaanza na Mheshimiwa Aggrey Mwanri, Mheshimiwa William Shellukindo, Mheshimiwa Dr. Harrison Mwakyembe na Mheshimiwa Dr. Chrisant Mzindakaya. Kwa jinsi tunavyowafahamu wasemaji hawa, nawaomba sana Waheshimiwa Wabunge, muwepo hapa ili tuanze vizuri ile saa 11.00 jioni. Ni jopo zuri sana la wasemaji. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nashawishika niseme tu kwamba kama ujumbe tu kwa Serikali itapendeza kama na Waheshimiwa Mawaziri nao watakuwepo kwa wingi kidogo, jambo hili ni zito. Sasa tunapolizungumza kwa kweli tuna Waziri mmoja tu kwa shughuli za Kibunge, *Chief Whip* upo ni wajibu wake, *Attorney General* yupo na Waziri mtoa mada. Waziri peke yake mwingine ni Waziri wa Katiba na Sheria nikiacha Mainabu Mawaziri.

Waheshimiwa Wabunge, kwa nafasi hii naomba sana tumpongeza Mheshimiwa Dr. Mary Nagu, huyu ni mmoja wa Mawaziri ambaye anakaa ndani ya Bunge. Ana nidhamu ya kukaa ndani ya Bunge na mambo haya tuwe tunayaona na kuyakubali. Kwa

sababu kama Waheshimiwa Wabunge mnazungumza kwenye *chamber,* Waziri yuko mmoja au wawili, kidogo inakuwa shida. Natambua uwepo wa Manaibu Waziri kadhaa wao kidogo wanajitahidi. Lakini itapendekeza jioni na siku za usoni kama wenzetu Mawaziri watakuwemo humu Bungeni kwa muda mwingi zaidi. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nimekumbushwa kwamba ni wajibu wangu kutangaza tanzia ingawa tumekwishafahamu. Nasikitika sana kutangaza kifo cha aliyekuwa mwenzetu Marehemu Dr. Aaron Chiduo, ambaye si tu alikuwa Mbunge, lakini kwa miaka mingi amekuwa Waziri wa Afya katika Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, amefariki leo alfariji katika hospitali ya Hindu Mandal na baadaye kupelekwa Muhimbili. Nadhani kwa utaratibu wa kawaida tutatoa taarifa kuhusu mipango ya mazishi ili wale watakaoweza, maana yake Gairo siyo mbali sana tunaweza kufanya utaratibu wa kwenda kumsindikiza mwenzetu. Mwenyezi Mungu aiweke roho ya marehemu mahali pema peponi. *Amin!*

Waheshimiwa Wabunge, sasa nasitisha shughuli za Bunge hadi saa 11.00 jioni.

*(Saa 7.00 mchana Bunge lilifungwa mpaka saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

*Hapa Mwenyekiti (Mhe. Job. Y. Ndugai) Alikalia Kiti*

**MHE. JOB Y. NDUGAI - MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunao wazungumzaji 17 watakaochangia hoja katika hoja iliyo mbele yetu. Kwa hiyo, moja kwa moja tunaanza na mchangiaji wa kwanza ambaye ni Mheshimiwa Aggrey Mwanri. Mheshimiwa, karibu!

**MHE. AGGREY D. J. MWANRI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kutoa mchango wangu katika Muswada huu wa kukabiliana na rushwa katika nchi yetu. *(Makofi)*

Awali ya yote naomba nichukue nafasi hii kwa niaba ya wananchi wa Jimbo langu la Siha, kutoa pole kwa ndugu, jamaa na marafiki wa Ndugu yetu Mheshimiwa Dr. Aaron Chiduo ambaye ametutoka. Nawapa pole sana kwa msiba uliowapata.

Mheshimiwa Dr. Aaron Chiduo alikuwa ni Mbunge mwenzetu, tulishirikiana naye sana na alikuwa katika Serikali. Kwa hiyo, napenda kwa niaba ya wananchi wa Jimbo langu la Siha niseme pole sana!

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kuchukua nafasi hii kuwapongeza wanachama wa Chama cha Mapinduzi ambao wamejiunga na sisi kama Wabunge wanaotoka kule Tunduru na yule anayetoka kule Mbeya.

Mimi naamini kwamba sifa hizi zinakwenda kwa Chama cha Mapinduzi kwa sababu inaonyesha jinsi ambavyo wananchi wa Wilaya ya Tunduru wanakubaliana na

Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi na sera za Chama cha Mapinduzi. Kwa hiyo, napenda kumpongeza sana Mheshimiwa Mtutura Abdallah Mtutura, kwa ushindi ambao ameupata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasikitika kwamba ndugu yetu Chacha Wangwe hayuko hapa, jana aliuliza maswali *very pertinent* hapa ambayo nilikuwa nafikiri kwamba ningechukua hafla hii nikayazungumzia kwa sababu yana uhusiano mkubwa sana na hoja tunayoizungumzia leo. Alikuwa anajaribu kuhoji kama bado Tanzania tunaendelea na siasa ya ujamaa na kujitegemea. Nataka niseme hapa, iko ndani ya Katiba ya Chama cha Mapinduzi na iko ndani ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwamba nchi ya Tanzania ni nchi ya ujamaa na kujitegemea ambayo iko katika mfumo wa vyama vingi na kama anataka, anaweza akai-*check* hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia kuna ma-*comrade* ambao wamezungumzia kuhusu Chama cha Mapinduzi kinasema nini kuhusu rushwa. Unapojiunga na CCM, kazi ya kwanza ni kuapa kama Mbunge unavyoapa hapa. Kuna *clause* namba 4 ya ahadi za mwana CCM inasema: “rushwa ni adui wa haki, sitatoa rushwa wala kupokea rushwa.” Hayo ni masuala ya msimamo, siyo masuala ya kwangu mimi, ni masuala ya msimamo. Kwa hiyo, mimi nazungumza habari ya msimamo hapa na anakwenda mbele zaidi anazungumza habari katika nchi ya kijamaa na katika nchi ya kibepari, mbona tumefika mahali njia kuu za uchumi zimeondoka. Mimi nataka tu niseme, katika nchi ya kijamaa unachoangalia, unaangalia kwamba unatatua matatizo yako kwa njia ya haki na usawa! Ndicho tunachosema pale, hatusemi kitu cha ajabu sana pale. *(Makofi)*

Sasa aseme Mbunge humu ndani anayefikiri kwamba tunaweza tukaendesha nchi hii bila kutatua matatizo kwa njia ya haki na usawa aseme kwamba si vizuri! Haya mengine ya kwamba ooh unajua sasa *private sector* imeingia. Ni kweli ni sera za Chama cha Mapinduzi na tumeeleza kwa nini tumeingia humo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nieleze katika *capitalism* unachotafuta mle ndani ni kitu kinachoitwa faida kibao, ndio unatafuta mle ndani. Katika nchi inayotafuta faida kibao, haitibu wazee wanaoumwa UKIMWI na *TB* bure. Kwa sababu anatengeneza faida kibao, lazima anakwambia leta pesa, kama unakufa, kufa tu. Katika nchi ambayo inatengeneza faida kibao, nchi ya kibepari, hawafiki mahali wakasema watoto wenye miaka 5 kwenda chini, watatibiwa bure bila kulipa. Wanamwambia mama, leta pesa hapa kama mtoto hana pesa, hakuna pesa atakufa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi hii ya Tanzania isipojenga ujamaa, watu watakufa. Nataka nikwambie *integrity* na *credibility* iliyonayo CCM ni kwa sababu imetamka katika matamshi yake kwamba nchi hii ni nchi ya ujamaa na kujitegemea. Hili si jambo la ajabu na nasema mimi kwamba tusiondoke hapo na Watanzania hili siyo suala la Chama cha Mapinduzi, hata *Opposition*. *The moment* Tanzania tunaondoka katika siasa ya ujamma na kujitegemea, *we are gone,* tumekwisha. Baada ya hapo sisi sasa ni watu wa kubeba mizigo kichwani hatuna mbele wala nyuma, hatujui tunakoelekea. Ningepata nafasi nzuri, ningezungumzia mambo haya. Lakini, nilitaka niyaeleze haya ya awali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa rushwa inayozungumzwa hapa, inapigwa vita ndani ya mfumo wa kijamaa na inapigwa vita ndani ya mfumo wa kibepari. Katika hilo, wote tunafanya kitu kimoja. Mabepari wana-*deal* na rushwa *perpendicularly, right, centre* na *left* na hivyo hivyo katika ujamaa tunakabiliana na kitu kinachoitwa rushwa kwa sababu unachotafuta pale ni kupeleka huduma zaidi kwa watu wako. Kwa hiyo, wote wanapambana na rushwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wale akina Clinton, akina Putin wanapambana na rushwa, ukienda China wanapambana na rushwa, wote mifumo yote na ndio maana Mheshimiwa Philip Marmo umepata matatizo makubwa sana kwenye kutoa *definition* ya rushwa. Rushwa huwezi kui-*define* kwa sababu inajitokeza katika mifumo yote ya kiuchumi ya kijamii. Unachoweza kufanya pale ni ku-*characterize*. Huwezi ukasema *definition* yake, ni lazima useme mazingira haya, ngono ikitolewa hapa, hii ilikuwa ni rushwa. Useme hapa walipokuwa wako katika mpango wa kutengeneza barabara, ile iliyokuwa inatengenezwa pale ilikuwa ni rushwa!

Mheshimiwa Mwenyeikiti, huwezi ukai-*define,* na mimi sikushangaa sana uliposhindwa kupata *definition* halisi ya rushwa. *You can not!* Hutaweza kui-*define,* lazima ui-*characterize,* uweke mazingira na mimi *to the best of my knowledge as a Member of Parliament* nimesoma humu ndani. Muswada huu umeweza kuonyesha mazingira yanayoonyesha kwamba hii ni rushwa. Hilo nilitaka niliweke vizuri hapa tuweze kuelewana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisema tumbane Mheshimiwa Philip Marmo hapa sijui ataitapika *definition* ya rushwa! Hakuna Mzee wangu, hutaweza, ni sawa sawa na *peasant, peasant* huwezi kum-*define*. *Peasant* yupo katika *communalism*, *peasant* yupo katika *slavery,* yupo katika *feudalism,* yupo katika *capitalism*, yupo mpaka katika *socialism*.

Huyu anayetokea katika mifumo, huwezi kusema huyu ni mtu wa namna gani. Unachoweza kufanya pale, yule *peasant* unam-*characterize,* unasema tu huyu huwa ana vitu vyake mbili, moja. La kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili tunazungumza hapa namna ya kukabiliana na rushwa. Unajiuliza ni nini kimetokea! Kwani ni nini kimekuja kipya! Kilichotokea ni kwamba ipo Serikali makini ya Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete ambayo ina *political will* ya kusema tunataka ku-*fight corruption* katika nchi hii. Ndicho nilichokuwa nazungmza, *that is the bottom line*. Mimi nimemsikiliza Mheshimiwa Rais, toka siku amekuwa Rais, analihutubia Bunge, anazungumza kuhusu vita dhidi ya rushwa.

Mimi nitawaeleza, wenzangu wamezungumza hapa, nimewasikia wanasema unajua huyu ukiileta awajibike kwa Bunge, ngoja nikwambie, *modes of production* zina-*change in form, but in content* zinabakia pale pale. Ni mpaka ufike mahali umpate mtu ambaye ana *political will* ndio aseme hivi, *there is no corruption* katika nchi hii, anaizuia rushwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata ukisema wawajibike kwa Bunge waje hapa, kama huna *political will,* hutaondoa *corruption* katika nchi hii na hiyo ndiyo *argument* yangu. Hizi zinaweza zikabadilika tu majina, zina-*change in form,* zitahama, mnabaki hivi kama hamko *serious,* yatahamia katika mfumo mwingine hivi hivi, yataingia mle yatatoa *exit,* yatatoka. Kinachotakiwa sasa hapa, ni kwamba hii sheria inayokuja hapa, inaweka mazingira ambayo yatatuwezesha kuzuia rushwa isiendelee kufanya kama ilivyokuwa inafanya kule nyuma. Sasa watu wengine wanataka kwenda haraka sana, hii ni *process*. Kinachotakiwa hapa sisi ni Watanzania kusimama na kusema hivi, hatuwezi kuruhusu habari ya rushwa katika nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nimekwenda Norway, nazungumza na mama mmoja ananiambia Norway tukijua kwamba wewe unataka uongozi katika nchi hii na unatumia rushwa kupata uongozi ule, hatukupi uongozi na hii tunaisema ndani ya CCM na tumewaambia wanachama wenzetu, mtu yeyote anayegombea uongozi ndani ya CCM na anasema kwamba atatumia rushwa kuwa kiongozi katika CCM, hatumpitishi! Wanajua, wanajua! Ngoja kidogo, Mheshimiwa Kabwe Zitto, wewe ngoja, hapa tunazungumza *issues* nzito za nchi. Kama watu hawakujua, basi wajue sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni mjumbe wa Kamati Kuu ya Chama cha Mapinduzi, ni *member* wa *National Executive Committee*, ni Mkuu wa Idara ya Itikadi na Uenezi, nakaa kwenye Sekretarieti. Tumebaini leo, kiongozi huyu anatafuta uongozi katika nchi yetu na anataka kupitia rushwa, haturuhusu apite. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ngoja nitakwambia, ngoja nikwambie, na hili tuzungumze wote na hili *Opposition* mtusaidie na wana-CCM watusaidie. Rushwa katika nchi hii tukiiruhusu, hutaondokana na matatizo uliyonayo katika nchi hii. Nitakueleza, unatakiwa u-*resolve the primary contradiction* ndani ya uchumi, ndipo useme unaondokana na rushwa. Tusikilizane vizuri hapa, ni hivi, hapa ukiwa unajikuna hivi, dawa yake si kuchukua dawa unapaka hapa juu, unatafuta kiini cha kujikuna. Kwa nini unajikuna! Ukikaa unaweka dawa, unaweka hivi, huponi kwa sababu hujatafuta kiini, mpaka akwambie una *allergy*, ukila papai ndio maana unajikuna, unaancha kula papai, utapona! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulisema tutakuwa na *a very serious talk* hapa, tuweke *a serious talk* hapa ndani! Ukitaka ku-*resolve problem* ya rushwa, Mheshimiwa Philip Marmo, ukasema hivi mimi nitakwenda na uchumi wangu hivi ulivyokaa hivi, nitakwenda nao tu hivi potelea mbali, hutaweza! *(Makofi)*

Nitakwambia, lazima ufike mahali, anasema Max; *"Always the economic base determines the super structure."* Haya unayosema hapa juu hapa, hapa chini patakataa patakwambia huna uwezo wa kubeba. Namalizia, usiwe na wasi wasi nitamalizia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima ujenge uchumi, kama huwezi kupeleka dawa pale Muhimbili, rushwa itatoka pale kwa sababu hakuna dawa. Ndiyo! Kama maduka yetu hayana sukari, hayana mafuta, rushwa itatoka! Lazima u-*build economy!* Uchumi huu wa kwetu ni uchumi ulio nyuma, duni na wa kikoloni mamboleo, ndio jina lake. Ni uchumi ambao hauwezi kubeba majukumu yake mpaka usaidiwe na pampu kutoka nje

ndio maana unaona hii habari ya watu kutoka nje na nini na mambo mengine nazungumza. Lazima ufike mahali useme hivi nitajenga uchumi wenye nguvu ambao utatoa huduma kwa watu wangu, Mheshimiwa Wilson Masilingi, alitusaidia, ikiwezekana bure halafu utakuwa una-*fight corruption*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *corruption* katika nchi hii ni lazima tui-*fight,* lazima tukatae. *Corruption* inaondoa mamlaka zilizoko madarakani, zinaondoka kabisa, zinaondoka! Kama kuna *corruption* katika nchi hii, watu hawatalipa kodi. Kama kuna *corruption* katika nchi hii, nataka nikwambie, watoto hawatakwenda shule, ni lazima ujue. Kwa hiyo, hii vita ni ya kwetu sisi wote, tuamue kwamba tunaruhusu tunakwenda na *corruption* mbele kwa mbele au tunaizuia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi imesema nini! Kwanza, kuendelea kuchukua hatua za kisheria, kiutawala na kinidhamu kwa wale wote watakaobainika kuhusika na vitendo vya rushwa.

Pili, kujenga mazingira mazuri zaidi yatakayowapa wananchi uwezo, ari na ujasiri zaidi katika kupambana na rushwa, wizi na ubadhilifu wa mali ya umma. Tatu, kufuatilia malalamiko ya baadhi ya wananchi kwamba kuna watu wengi wanalimbikiza mali nyingi kama majumba, mashamba na kadhalika kuliko uwezo wa mapato halali wanayoyapata na kadhalika. Kwa sababu nataka nimalizie, sasa, hapa haya yote yametamkwa, Mheshimiwa Philip Marmo wanachofanya sasa hivi ni kuitekeleza hii Ilani na ma-*comrade* wanasema CCM haijazungumza hapa, hii ndio anaweka haya mazingira pale, tusaidiane. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wamezungumza habari za *DPP* hapa. Mimi noamba utakaposimama utwambie *role* yake! Ukicheza pale, usipoangalia kwa *DPP,* ndipo itakuwa *exit* ya kutolea mambo, atakwambia hakuna ushahidi umepatikana hapa.

Pili, tumezungumza habari ya Bajeti ya huyu Mkuu wa Taasisi ya TAKURU, wewe una *prerogative* ya kuipitisha au kutoipitisha. Lazima ufike mahali useme hakuna *variation,* iende hivyo hivyo ndio uta-*maintain* hiyo *indepedence* unayozungumzia. Tatu, adhabu zinazotolewa hapa, lazima iwe adhabu kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzetu Marekani kule wana-*deal* na rushwa pale *perpendicular, left, right and centre*. Wanachofanya siyo *percent* hii, wana-*confiscate* kila kitu kilichohusika katika hiyo kitu. Sitaki kuleta *some radical elements* hapa. Huu ni msimamo wa Chama cha Mapinduzi na Serikali ya Chama cha Mapinduzi *must be seen to be on top of business* kuzuia rushwa katika nchi hii. Tuzuie rushwa hii, tusiruhusu kabisa. Tumsaidie Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete ku-*fight corruption* katika nchi hii. Watu walisema kwamba alipewa orodha, TAKURU wamesema kwamba Rais hajapokea orodha ya watu ambao wanachukua rushwa, tumeambia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananachi wa Tanzania lazima tunyanyuke wote tukatae *corruption,* tumsaidie Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupambana na rushwa katika nchi hii. Hii kazi ni yetu sisi wote, Waheshimiwa Wabunge kama tunataka kuondokana na matatizo hapa, mkicheza mtaletewa Wabunge wamejaa humu ndani

wanaotokana na *corruption* na Wabunge wazuri wataachwa huko, watakuja wa ajabu ajabu wataingia humu ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo naomba kuunga mkono hoja. Nakushukuru sana! *(Makofi)*

**MHE. JOB Y. NDUGAI - MWENYEKITI:** Huyo ni Mheshimiwa Aggrey Mwanri. Kwa rafiki yangu Mheshimiwa Habib Mnyaa na Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa, huyo ni Katibu wa Siasa na Uenezi wa Chama cha Mapinduzi. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi nitoe mchango wangu kidogo. Awali ya yote napenda sana kutoa pole zangu nyingi sana kwa familia ya Marehemu Dr. Aaron Chiduo, Mwenyezi Mungu aiweke mahali pema roho yake. *Amin!*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza sana Mheshimiwa Mtutura Abdallah Mtutura, kwa ushindi wake katika Jimbo la Tunduru. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza mimi nimefarijika sana kwamba Mheshimiwa Aggrey Mwanri amezungumza kabla sijazungumza. Amenisaidia kwenye mambo ambayo baadhi nilitaka niyazungumze. Ameeleza wazi wazi kwamba Katiba ya Chama cha Mapinduzi imezungumzia rushwa, wala siyo Msemaji wa Upinzani alizungumzia Katiba ya *TANU,* lakini Katiba ya CCM toleo la mwaka 2005 mwezi Mei, imechukua bado ahadi za mwanachama ambazo Mheshimiwa Aggrey Mwanri amezitaja pale, sina haja ya kuzirudia. Halafu Ilani ya Uchaguzi vile vile ameitaja.

Sasa mimi nataka tu kuongezea ule mwelekeo wa sera za CCM katika miaka ya 2000 hadi 2010, ningependa kidogo ninukuu pale: "Vita dhidi ya rushwa, juhudi za kupambana na uozo wa rushwa nchini zimeanza kutoa matunda." "Kazi ya kupambana na vitendo vya rushwa ni kazi ya kudumu na inahitaji uongozi uliojitolea mhanga kupambana na vitendo hivyo." Ibara ya 103; "kwa kuzingatia uzito wa tatizo lenyewe, CCM itahakikisha kuwa Serikali inaendelea na kupambana nayo kwa kasi kubwa zaidi na kwa kushirikisha wananchi." *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliona haya niyataje ili niendeleze pale kwamba kazi ya kuzuia rushwa kwa kweli siyo ya Taasisi ile. Ile Taasisi itashughulika na wale wakosaji. Lakini kujenga mazingira na kuhakikisha kwamba rushwa haienei nchini, ni ya Bunge hili na wananchi wote kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni dhahiri kabisa baada ya kuangalia vitabu hivi vitatu vya Chama cha Mapinduzi, Chama ambacho kinaongoza Serikali, vimeeleza wazi wazi kwamba rushwa ipo. Hakuna sababu yoyote ile ya kusema rushwa hamna. Tunachotakiwa kufanya ni kwamba hii iliyopo tuiondoe na tuhakikishe kwamba tunaifuta kabisa rushwa na kujenga mazingira ambayo hayaendelezi rushwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, rushwa siyo hapa kwetu tu maana yake watu wanaweza kudhani hii rushwa ni hapa tu. Kuna wenzetu wamesema katika uchumi inategemea

uchumi wako unavyouendesha, unaweza kujenga uchumi ambao una mianya mingi sana ya kukandamiza watu wengine kwa kutumia rushwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Benki ya Dunia kuna Taasisi inaitwa *World Bank Institute* huwa inafanya machapisho na inaangalia masuala mbali mbali ya kidunia na kuweka angalizo kwamba tizameni hili lina matatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kitabu kilichotolewa mwaka jana, ripoti ya *World Bank Institute* inayosema *the role of Parliament in curbing corruption* katika ukurasa wake wa 14, kuna nchi 100 zinazoendelea ambazo zilifanyiwa utafiti wa rushwa na imeonekana kwamba rushwa ina matatizo makubwa sana tena ya hatari. Wanasema hivi, kwanza, huduma za uchumi wa nchi, husababisha kutungwa sera mbovu ambazo zinatumia michakato isiyoeleweka, inasababisha matumizi mabaya ya rasilimali za nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kunukuu; "Hupunguza ushindani katika shughuli za uchumi, huduma za jamii na biashara, husababisha ujenzi wa miundombinu isiyozingatia viwango, husababisha ugawaji rasilimali usiozingatia umuhimu na vipaumbele, rushwa hukatisha tamaa wawekezaji wenye uwezo na kukumbatia wawekezaji wababaishaji, rushwa husaidia ukwepaji wa kodi zinazotakiwa kulipwa kisheria, rushwa husababisha kuingia mikataba yenye gharama kubwa, rushwa husababisha vurugu za kisiasa na migogoro katika jamii, rushwa ni chanzo kikubwa cha utawala mbovu ambao hauzingatii misingi ya haki na sheria za nchi."

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani suala la kujiuliza hapa, ni kwamba, je, Muswada huu umezingatia haya, umejielekeza kwenye kutatua au kuondoa mianya ambayo inajitokeza kwa maana Katiba ya CCM imesema hivyo, mwelekeo wa sera umeelekeza, Ilani ya Uchaguzi ambayo tunaitekeleza sasa hivi, imeelekeza kuhusu rushwa kwamba rushwa ni kitu kibaya sana lazima kipigwe vita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nionavyo Muswada huu, kwanza Muswada umezingatia wazi wazi kwamba rushwa ni tatizo kubwa hapa nchini, hilo ni moja. Vile vile Muswada umeainisha makosa ambayo yanaonyesha wazi wazi haya ni ya rushwa kama tulivyoelezwa na Mheshimiwa Waziri, sheria iliyotangulia ilikuwa imeonyesha makosa mnne tu. Muswada vile vile umeweka vipengele ambavyo vinashughulikia kila aina ya kosa. Muswada vile vile umeonyesha kwamba TAKURU haiwezi kufanya kazi peke yake, kuna ushirikianao ambao unahitajika na vyombo vingine vya dola.

Sheria vile vile imeweka taratibu za kupeleleza na kufikisha wakosaji katika mahakama. Muswada vile vile umeweka vipengele vya kulinda watoaji taarifa, kitu ambacho kwa kweli ni muhimu sana kwamba raia wema wanaweza wakakaa na taarifa wakasononeka tu, wakalalamika tu, wakaogopa kwenda kutoa taarifa kwa kuogopa kwamba wataweza kufahamika na hivyo kupata matatizo hata kuuwawa vile vile, kama mtu amepata burungutu lake la shilingi milioni 300 na wewe unapita kati kati yake, haoni kwa nini asitumie shilingi milioni kama 10 hivi wewe uondoke pale uondoe ghasia. Kwa hiyo, hili nadhani ni jambo la muhimu sana. Vile vile imeweka vifungu ambavyo

vinashughulikia mali za watu ambao imedhihirika wazi wazi kwamba hawakuzipata kwa njia halali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumezungumzia sana hapa, wenzangu wamezungumzia uhuru wa chombo kinachotajwa. Mimi nadhani inategemea wewe mwenyewe unavyotengeneza muundo wa kuongoza nchi yako. Unaweza kukiacha chombo peke yake na bado kisiwe na uhuru na katika uhuru huo unazungumza kitu gani! Chombo hiki ni cha utendaji chini ya Rais, sasa wewe unataka iwajibike kwa Bunge, yaani iwe Taasisi ya Bunge! Sisi kazi yetu ni nini, si kuangalia kwamba hayo yaliyokubaliwa kwenye sheria yanatekelezwa na tunaiuliza Serikali, Serikali ina Rais. Kama tumeshindwa kupata maelezo kutoka kwa Waziri, tunakwenda kwa Rais tunamuuliza mbona hii haiendi vizuri. Hii ya kuzungumza kwa jumla tu kwamba kiwe huru, kiwe huru maana yake nini? Kinachotakiwa hapa ni kwamba chombo kile kiwe na uwezo, kitumie sheria ile kufanya kazi yake bila kuingiliwa na chombo chochote na chombo hiki hakiwezi tu kuachwa peke yake na hapo kinapowekwa kinawekwa chini ya Rais. Sasa kama nchi inaona hicho chombo kikiwa kwa Rais, hapana, hakiwezi kufanya kazi mpaka kije kwenye Bunge, mimi sikubaliani nao! Bunge lina kazi zake, tutamtungia Rais na Serikali yake sheria, tutamsaidia aunde vyombo ambavyo vinafanya kazi yake bila kuzuiwa na chombo chochote na kama kuna sheria inazuia, basi sheria hiyo iletwe katika Bunge ili iweze kutekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninavyoona mimi, hii ni Idara ya Serikali inayojitegemea. Kuna wengine wamesema kwamba ifanane na Idara ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu *(Auditor Office),* ndiyo kwa kweli inatakiwa ifanye kazi hivyo. Inatakiwa ifanya kazi hivyo ndiyo sheria hii inatungwa. Ndiyo maana hakuna watu wengine ambao wanakifanya chombo kije kuwajibika kwao, isipokuwa kwa Rais. Lakini Rais ana Waziri anamsaidia, huwezi kumwondoa yule. Nani ataleta hoja hapa kwenye Bunge! Huu ni utaratibu tu, haina maana kwamba basi Waziri yule ambaye anashughulikia kumsaidia Rais, basi atasema hili acha, hili acha, sheria haimruhusu kufanya hivyo. Lakini anahusika katika kuweka kanuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona vile vile kwamba sheria hii imeweka adhabu za kutosha na Muswada huu umegusa sekta ya umma pamoja na sekta binafsi. Kwa sababu sisi ni Watanzania, tuna ndugu zetu wako sekta ya binafsi, wengine wako sekta ya umma, tunamwingiliano mkubwa sana. Kama utazuia rushwa kwenye vyombo vya umma na kwenye sekta binafsi umeachia tu, hujafanya kazi yoyote ya maana. Kwa hiyo, mimi naishukuru sana Ofisi ya Rais kwa kuweza kuona haya mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa madhumuni ya Muswada huu ni kuzuia rushwa wala siyo kulea rushwa, basi kuna mambo mengine ambayo inabidi yatekelezwe. Nimeangalia mimi katika zile faini, Waziri amefanya marekebisho. Mimi nilikuwa nadhani faini ya mwisho kwenye kosa lolote kubwa, hasa tunaanzia kwenye madogo. Lakini rushwa ni rushwa tu. Mimi nadhani faini ya chini kabisa iwe shilingi 500,000/=. Halafu na kifungo cha chini kabisa kiwe mwaka mmoja. Halafu kwenda juu, tusiende chini ya hapo. Nakumbuka wakati wa hujuma za uchumi, ile sheria nadhani ilikuwa imeweka kiwango cha chini kabisa ilikuwa miaka miwili cha kifungo na vitu vingine.

Kwa hiyo, nasisitiza kwamba hivi faini pamoja na vifungo, viwe kwa utaratibu huo. Faini isiwe chini ya shilingi 500,000/=, ni kwenda juu halafu kifungo kiwe mwaka mmoja kwenda juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi napenda kutoa ushauri kwamba sasa tumefika mahali ile ahadi ya Chama cha Mapinduzi kwamba; "Rushwa ni adui wa haki na sitapokea wala kutoa rushwa."

Mimi nadhani sasa Serikali katika barua hizi ambazo mnawaandikia watu kuwateua kwamba nimekuteua wewe Katibu Mkuu, mshahara wako ni shilingi, kadhaa, utapata gari ya Serikali, ukifika pale mwisho kwenye ile barua uandike rushwa ni adui wa haki, unamkabidhi barua yake atakwenda nayo. Halafu, hawa wanakula viapo pamoja na Wabunge, katika viapo tuongeze sehemu moja ya kiapo ambacho viongozi na watendaji wale wanaoapishwa wanakula kiapo hicho na kiapo hicho kiwe kwamba; "Rushwa ni adui wa haki, sitapokea wala kutoa rushwa. Ewe Mwenyezi Mungu nisaidie." Hiyo itasaidia sana kuwakumbusha watu kwamba na kiapo ulikula kwamba wewe unajua rushwa ni adui wa haki, hutapokea wala kutoa rushwa. Haya mengine haya ni ya kuimarisha, kuongeza nguvu ya kushughulikia suala hili. *(Makofi/Kicheko)*

Vile vile napendekeza taasisi hii iwe na ofisi za wazi za elimu ya umma *(Public Relations Office)* zisiwe kwenye zile ofisi wanazoshughulikia kwenda kutoa mashitaka kule. Iwe wazi tu kila Mkoa, mwananchi aende pale akaelimishwe rushwa ni nini na inatolewaje, halafu waache ofisi hii isishughulike na kusikiliza watu wanaokuja kutoa mashitaka kwamba kuna mtu anataka rushwa kwa sababu ofisi hizi mara nyingi zinaogopwa na wananchi kwa sababu ziko katika maeneo ambayo yamejificha. Lakini ofisi zikiwa kama Anautougrou pale au pale Lushoto sokoni pale kwamba hii ni ofisi yenu ambayo inapiga vita rushwa, watakwenda pale wataelimishwa rushwa ni nini. Hata kama kuna film zinaonyeshwa pale. Lakini kama kuna mtu ana taarifa ya kutoa, aende mahali faragha aende akashughulikiwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa nafasi uliyonipa na naunga mkono hoja asilimia mia moja. *(Makofi)*

**MHE. JOB Y. NDUGAI - MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kabla sijamkaribisha Mheshimiwa Dr. Harrison Mwakyembe, ambaye atafuatiwa na Mheshimiwa Dr. Chrisant Mzindakaya, kuna matangazo mawili ambayo ningependa kuyatoa katika hatua hii.

Tangazo la kwanza nitalisoma jinsi lilivyo ni tangazo la Spika. Mheshimiwa Spika, amepokea ufafanuzi kutoka Serikalini kuhusu idadi ndogo ya Waheshimiwa Mawaziri, waliokuwepo ukumbini saa za mchana baada ya kipindi cha maswali.

Ufafanuzi ni kwamba Mawaziri wawili walikuwemo ukumbini katika sehemu zisizo za Mawaziri. Mawaziri watatu wako nje ya nchi, Mawaziri wanne wana udhuru kuhusu misiba na wagonjwa, Mawaziri wengine watatu walikuwa wanahudhuria Kamati

za Bunge. Baadhi pia walikuwa na Mkutano muhimu na Mheshimiwa Waziri Mkuu, ambapo huko walipokuwa kuna vifaa vinavyofuatilia mijadala inayoendelea Bungeni.

Waheshimiwa Wabunge, maelezo haya yanatangazwa ili kufuta hisia kwamba Mawaziri walipungua bila kuwepo sababu maalum na zinazotoshelezwa. Mwisho wa tangazo la kwanza. *(Makofi)*

Tangazo la pili Waheshimiwa Wabunge, mnatangaziwa kwamba kesho tarehe 14 Aprili, 2007 watangazaji wa kipindi cha *Power Breakfast* kupitia Redio ya *Clouds FM* watafanya tafrija fupi kwa heshima ya Waheshimiwa Wabunge katika Uwanja wa tafrija wa Bunge kuanzia saa 1.00 jioni. Katika tafrija hiyo, kutakuwa na muziki wa dansi pamoja na sarakasi, chakula na vinywaji. Mnaombwa wote kuhudhuria hafla bila kukosa. *(Makofi)*

**MHE. DR. HARRISON G. MWAKYEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Na mimi nianze kama wenzangu walivyofanya kutoa rambirambi kwa familia ya Marehemu Dr. Aaron Chiduo. Naomba Mungu aiweke roho yake mahali pema peponi. *Amin!*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile naomba nimpongeze Mheshimiwa Philip Marmo, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utawala Bora, kwa kuwasilisha Muswada huu mgumu mbele yetu, lakini wenye uzito na maslahi makubwa ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge wenzangu wamechangia mambo mengi ya msingi ambayo naamini yakizingatiwa vizuri na mtoa hoja yanaweza yakaboresha vizuri sana Muswada na tukaishia baadaye tukawa na sheria nzuri sana pengine sheria ya mfano katika kuzuia na kupambana na rushwa katika ukanda huu wa Afrika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nafikiria katika mchango wangu huu niongee zaidi, nafikiri nitaongea zaidi kama Mwanasheria kuliko Mwanasiasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tafiti mbalimbali zinaonyesha kwamba nchi ambazo zimefanikiwa sana kupambana na rushwa zimefikia hapo siyo tu kwa kuwa na sheria nzuri sana ya kuzuia na kupambana na rushwa. Lakini vile vile ni kwamba nchi hizo zina Mabunge yenye meno ya chuma. Maana yake siyo meno ya *plastic,* nafikiri mnanielewa. Maana yake ni nini. Mabunge hayo kwa niaba ya wananchi yanaisimamia Serikali katika utendaji wake kazi wa kila siku yaani *scrutiny and oversight function. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niwe muwazi sana. Bila kuwa na Bunge lenye meno ya chuma au bila kuboresha usimamizi wa Bunge kwa Serikali na vyombo vyake, kwa kweli sheria ya kuzuia na kupambana na rushwa hata iwe nzuri kiasi gani itashindwa kufanikiwa kwa sababu itakosa nguzo ya kuegemea na nguzo ya kuegemea ni Bunge. *(Makofi)*

Nimefurahishwa sana na kiongozi wangu wa Chama hapa amenukuu Ilani ya Chama cha Mapinduzi na mimi utaniruhusu dakika moja tu kuelezea kwenye Ilani ya CCM, Ibara ya 110. Tunasema, Serikali katika hii miaka hii mitano mpaka mwaka 2010 itajenga mazingira mazuri zaidi yatakayowapa wananchi uwezo, ari na ujasiri zaidi katika kupambana na rushwa, wizi na ubadhirifu wa mali ya umma.

Katika kipengele cha (d) cha ibara hiyo hiyo ya 110, Serikali itaendeleza kuziba mianya ya rushwa katika utendaji wa Serikali. Hivyo basi, mimi naamini katika kuisoma Ilani, uimarishaji wa Bunge ni moja ya hatua za kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika miaka ya 1960 baadhi ya Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania walipoteza viti vyao baada ya kufukuzwa na Chama Tawala kwa wao kuhoji ndani ya Bunge uhalali wa Chama kushika hatamu *(Party Supremacy)* badala ya Bunge kushika hatamu *(Parliamentary supremacy). (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini mimi huo mjadala siingii huko kwa sababu kwanza dhana zote hizi mbili *Party Supremacy* na *Parliamentary Supremacy* zimepitwa na wakati. Sasa hivi tunaongelea *Constitutional Supremacy* (Katiba kushika hatamu). Nilitaka nijiulize swali moja tu hiyo *Constitutional Supremacy* imekuja kujaje? Dhana ya demokrasia ya uwakilishi inasema; "chimbuko la madaraka yote katika dola yoyote ile, katika nchi yoyote ile, ni wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Katiba zote duniani za kidemokrasia zinakubali na zinakiri na zinatambua ukweli huo. Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, inakiri vile vile ukweli huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naamini hii Katiba ni Katiba nzuri. Sikubaliani na rafiki zangu wanaokimbilia *shortcut* ya Katiba Mpya. Katiba Mpya kabla hujaielewa hata hii? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nifungue ibara ya 8 (1)(a) ili twende kwa pamoja. Inasema wananchi ndiyo msingi wa mamlaka yote na inaongezea na Serikali itapata madaraka na mamlaka yake yote kutoka kwa wananchi kwa mujibu wa Katiba hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, huo ndiyo msingi wa *Constitutional Supremacy*. Wananchi ambao ndiyo chimbuko la madaraka yote, nguvu yao yote iko wapi? Sasa wananchi watahakikishaje kuwa madaraka hayo yanatumiwa vizuri. Katiba hii ibara ya 63(2), nitaomba nisome ili nifike mahali tukubaliane, inasema; "Bunge litakuwa ndicho chombo kikuu cha Jamhuri ya Muungano, ambacho kitakuwa na madaraka kwa niaba ya wananchi kuisimamia/kuishauri Serikali na siyo Serikali tu na vyombo vyake vyote katika utekelezaji wa majukumu yake." *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema yote haya kwamba tunaweza kuwa na Muswada mzuri, lakini bila kuimarisha Bunge hili, tunatwanga maji kwenye kinu. Kwa

niaba ya wananchi, Bunge hili linategemewa chini ya Ibara ya 63 (c) kuidhinisha hata mipango ya Serikali. Tutafanya hili kwenye semina tarehe 23, lakini ilitakiwa iwe ndani ya Bunge. Kwa niaba ya wananchi Bunge hili linategemewa kuwa nguzo kuu ya vita dhidi ya rushwa. Lakini *what is the practice? (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati zinadai kwa niaba ya wananchi ripoti za mikataba ambayo kwa wananchi ina wasiwasi, Serikali inakuja inasema hapana ni siri, yaani una siri dhidi ya watu ambao ndio chimbuko la madaraka hayo? Kinachoniumiza zaidi nataka nikiweke wazi kwa sababu nchi hii ni yetu wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati zinadai ripoti, hazipewi. Lakini jana nilisoma Gazeti la Rai, Gazeti ndiyo linapewa ripoti. Barua ya siri ya Serikali inachapishwa kwenye gazeti. Kwa hiyo, gazeti lina maana zaidi kupita hata Kamati za Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi imenisikitisha kwa sababu barua zilizomo mle ndani ni *current,* za juzi tu kutoka Ofisi ya Waziri wa Mkuu. Halafu mpaka mimi najiuliza, hivi Serikali hii haina hata taratibu za usiri wa *documents,* kwa sababu sijaona ikilalamika. Lakini kwa Kamati ya Bunge kudai karatasi hiyo hiyo, ni matatizo makubwa. *There is something seriously wrong* na utendaji wetu wa kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Rais wetu alisema hapa hapa Bungeni katika hotuba yake ya kihistoria ambayo tunakumbuka wote tarehe 30 Desemba 2005. Alisema; "Tanzania yenye neema tele inawezekana. Alisema maisha bora kwa kila Mtanzania yanawezekana. Akamalizia kwamba kila mmoja wetu atimize wajibu wake." *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, chini ya sakafu ya moyo wangu naamini Rais wetu yuko *so committed.* Nauliza tu je, Bunge tunatimiza wajibu wetu ili tuhakikishe maisha bora kwa kila Mtanzania?

Sasa ni kutokana na hotuba hiyo ya Mheshimiwa Rais, mimi naamini Spika wetu akaunda Kamati ndogo kupitia Kanuni za Bunge letu ili Bunge letu liweze kutekeleza mahitaji na matumaini ya wananchi na tufikie mahali ambapo kila mtu ana neema kwenye nchi hii. Ulikuwa uamuzi mzuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwepo kwenye hiyo Kamati. Tumefanyakazi nzuri, tumetumia fedha ya walipakodi, tumezunguka, tumekwenda India na sehemu zingine duniani. Tumeleta kazi za aina tatu. Nasema hili kwa sababu tunaongelea vita ya rushwa. Hatutaiweza tukiwa na *double standards*. *Volume* ya kwanza tumetengeneza marekebisho ya Kanuni zetu ili Bunge letu liwe zuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni *prerogative* ya Bunge, hamna anayeingilia. Lakini nasikia hilo limeingiliwa kati. Na nani? Nani yuko *above the Constitution?* Yaani kitu ambacho kiko *within the prerogative* ya Bunge, hata kubadilisha Kanuni tu, *it is a problem*. Sasa hili Bunge lina meno ya chuma au ya *plastic? (Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumetengeneza *juzuu* ya pili, ambayo tuliainisha sheria ambazo zikirekebishwa, zitasaidia Bunge. Na *juzuu* ya tatu, ni tofauti kabisa inapendekeza kuhusu mabadiliko ya Katiba. Tulikuwemo mle wote…

*(Hapa microphone ilizimika)*

**MHE. JOB Y. NDUGAI - MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, atafidiwa dakika zake. Kama chombo hicho hakifanyakazi Mheshimiwa Mbunge anaruhusiwa kutumia chombo kilicho jirani.*(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Hujuma hiyo.

**MHE. JOB Y. NDUGAI - MWENYEKITI:** Mashine zetu zinaonyesha Mheshimiwa Lembeli, Mheshimiwa Ameir, Mheshimiwa Kwaangw' na Mheshimiwa Abdallah, wamewasha. Tuliowasha wote tuzime ndiyo inasababisha huu mgongano unaoleta matatizo. Unaweza kwa hatua hiyo Mheshimiwa Dr. Mwakyembe kumalizia hotuba yako. *(Makofi)*

**MHE. DR. HARRISON G. MWAKYEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Pengine nimalizie tu kusema Ibara ya 89 ya Katiba inasema; "bila kuathiri masharti ya Katiba hii Bunge laweza kutunga Kanuni za kudumu kwa ajili ya kuweka utaratibu wa kutekeleza shughuli zake." Mimi nilikuwa nataka nitoe ombi kwako limfikie Mheshimiwa Spika, kwamba tunaomba marekebisho ya Kanuni zetu yatekelezwe kwa sababu hii ni *prerogative* ya Bunge. Mambo ya Sheria na Katiba yasubiri mpaka yaletwe kwenye hili Bunge. Sisi wote tunakubaliana kama Watanzania kwamba tuheshimu Katiba, *Constitutional Supremacy. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimalizie kwa kusema tu kwamba uzoefu duniani kote unaonyesha na umedhihirisha kwamba bila kuwa na Bunge lenye meno ya chuma vita dhidi ya rushwa ni ndoto. Ahsante sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.*(Makofi)*

**MHE. DR. CHRISANT M. MZINDAKAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze na mimi kutoa maoni yangu kuhusu Muswada huu. Kwanza kabisa awali ya yote naunga mkono. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ningependa kutumia nafasi hii kumpongeza Waziri kwa niaba ya Serikali, kwa kuleta Muswada huu. Najua amefanya juhudi kubwa kushirikisha watu wa aina mbalimbali ili waweze kutoa maoni yao. Labda kabla sijaendelea ili nisije nikasahau nilitaka niseme kidogo kuhusu maneno ya busara aliyokuwa anayazungumza Mbunge mwenzangu Mheshimiwa Dr. Harrison Mwakyembe sasa hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi wakati tulipopewa nafasi ya kufanya mabadiliko kwenye Katiba na wananchi wakatakiwa watoe maoni na nitakapoendelea kuwa hai

nitaendelea kusema hivyo hivyo kwamba maadam Mawaziri wanatokana na Wabunge wa Majimbo, Bunge hata siku moja haliwezi kuwa na meno makali, haiwezekani. Kwa sababu humu humu ndani tukitoka mlangoni tunaoneana haya kwa sababu sisi wote ni Wabunge na wengine mkitoka mlangoni ana maneno mazuri ya kusema, lakini analala anaoto ndoto siku moja nitakuwa Waziri, hataki kusema, kwa kweli tunadanganyana hapa, huo ndiyo ukweli humu ndani. Kwa hiyo, hawasemi. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi mtu mmoja, namna gani mzee mimi nilikuwa kijana nilisema na wewe kijana sema, mimi mzee sasa. Kwa hiyo, nataka tuambizane ukweli hapa. Mawaziri watokane na raia ambao Rais ataona kwa uadilifu wake wanafaa kumsaidia kuongoza nchi hii. Wote tuwe nyuma ya *bench*. Pia vipo vingine ambavyo Mawaziri kwa mfano mimi natoka Mkoa wa Rukwa, kama Waziri wa kwetu akifanya ovyo siwezi kusema humu Bungeni kwa sababu itaonekana kama namsakama. Akitoka anasema yule ananionea wivu kwa sababu hakupata, ndiyo yapo mambo yanafanyika ovyo mengine hatutaki kusema humu. *(Makofi/Kicheko)*

**MBUNGE FULANI:** Rukwa.

**MHE. DR. CHRISANT M. MZINDAKAYA:** Ahaa, siyo Rukwa mimi sina tatizo Rukwa, mimi na wenzangu tunaheshimiana vizuri tena wananiita Mzee, kwa hiyo, sina tatizo. Hii nasema kwa uzoefu kwa sababu Waziri mmoja alishapata kumuita Mbunge mwenzake akasema bwana mbona wewe unaniandama na alisema humu humu Bungeni. Kwa maneno anayosema Mheshimiwa Dr. Harrison Mwakyembe, hayawezekani mpaka Wabunge wote tuwe *back benchers* wa kuchaguliwa ndiyo inawezekana. Lakini hivyo hivyo hapana. Shabaha tulizokuja nazo humu zimetofautiana humu ndani. Huo ndiyo ukweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo ningependa sasa niseme yafuatayo, la kwanza, naungana na Mheshimiwa Hezekia Shellukindo na Mheshimiwa Aggrey Mwanri kwamba katika jambo hili jambo la kuzingatia hapa ni dhamira ndiyo jambo kubwa. Dhamira ya Serikali hii imetokana na Chama chake cha CCM, ndiyo imezaa Muswada huu. Kwa hiyo, mimi ningependa tupongezane sana Wabunge wote wa CCM na Wabunge wote wa vyama vyote tuunge mkono Muswada huu upite maana una maslahi kwa nchi kuweka heshima ya nchi. Lakini vile vile mambo haya tunaposema haifai pia tukasema kama sisi ndiyo wachafu kupindukia kama vile hatujatembea na kuona. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi sisi tulikuwa Uingereza na Mwenyekiti wetu Mheshimiwa John Cheyo. Tulifurahi kweli tuliona jinsi wakubwa wa Wizara fulani wanavyogalagazwa kwenye Kamati pale. Wamefanya mambo ovyo, wamewekwa kiti moto vibaya sana pale. Inavyotumika kule ni kwamba wale Kamati ya *PAC,* inawaweka kiti moto na nchi nzima inaona na redio zinatangazwa. Mambo haya ni ya kusogeza kidogo kidogo tu, mnaanza na mambo ambayo mtu akiyafanya ataona aibu hao ni wakubwa. Hilo moja. La pili ambalo ningependa kushauri Serikali ni kuwa kazi ya chombo na mafanikio ya chombo haitatokana na Sheria itatokana na kukijenga chombo. Watalaamu wake wapelekwe nje, wasome, watafutwe vijana wasomeshwe vizuri, wawe

na uwezo wa kuendesha kazi zao vizuri,walipwe vizuri ili wenyewe isiwe chanzo cha kupokea rushwa ili wafiche kesi. Hiyo itasaidia kweli kweli.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wazo hili la *DPP* mimi nafikiri Serikali baadaye mtazame kama tukijenga uwezo wa chombo hiki na vijana wenyewe mna uwezo wa kupeleleza wale watakaopeleleza kesi ndiyo waende Mahakamani ku-*present* kesi. Kwanza haiwezekani hawa wakapeleleza kesi halafu wanampa mtu mwingine kwenda kuidhinisha kama iende au isiende, maana hata haujui aliyepeleleza ndani ya chombo chao mle mle kuwe na wale wanaoridhika kwamba hii inashitakika. Lakini asiwe tena mtu mwingine, haya mambo lazima tuwe na mahali pa kuanzia. Lakini nadhani baadaye tunaweza tukatazama jambo hili. Kwa hiyo, ningeshauri jambo hili Serikali itazame.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Hezekia Shellukindo alivyosema ni kweli zile *criteria* aliyezitumia ni sawa kabisa kwamba yale ndiyo mambo makubwa wanayosema. Lakini pia mimi nataka niseme hapa mimi nina kofia ya pili ya Mjumbe wa Halmashauri ya Taifa hapa ndani, mimi ningependa pia kupongeza Serikali yetu kwamba ukipanga orodha za Serikali za waswahili angalau na sisi tunakubalika kubalika kukopeshwa kwa sababu tuna sifa zinazosemwa mle. Maana kama huna sifa hukopeshwi, unanuka na tunawajua kuna watu wananuka. Sasa mimi ningependa kuipongeza Serikali kwamba mmeleta Muswada ambao ukisimamia vizuri utaongeza sifa ya Serikali yetu. *(Makofi)*

Sasa jambo kubwa, labda mimi sijakwenda hapo naomba uongozi wa Serikali mnisamehe na Waheshimiwa Wabunge mnisamehe pia ni hivi ni kweli kuna suala la kuamini uongozi lakini vile vile kuna suala la kuwa na mashaka kesho kutatokea nini. Mambo yote haya huwezi kuyaweka pembeni. Lakini nasema kwa upande tunaoanza sasa mnapoanza jambo, mnalianza ili baadaye muone mnakwendaje na hamwezi kufanya mabadiliko kabla hamjaanza. Unapoanza safari ndipo utajua mwendo utakuwaje, utasimama wapi na utakwenda vipi. Kwa hiyo, mimi nilikuwa nataka kusema kama alivyosema Mheshimiwa Dr. Harrison Mwakyembe, kwamba kwa sasa hivi baada ya Serikali ya Awamu ya Tatu na hata Serikali ya awamu ya nne tuseme tangu tumeanza bado tumeendelea kuheshimiwa katika Jumuiya za Kimataifa. Hata sasa Rais wetu ametembea tembea, habari watu tunaotembea duniani kukutana na watu bado sifa yetu ni nzuri sana. Nini, uadilifu? *(Makofi)*

Mimi siku moja nilikuwa nazungumza na Mheshimiwa Rais, naomba radhi kutumia jina la mkubwa, mimi nilimuuliza swali nikasema Mheshimiwa Rais, naona unasema kwa nguvu sana habari hii ya kuzuia rushwa, mimi ningependa nijue hasa wewe mwenyewe unavyofikiria tutakavyopambana na rushwa katika uongozi wako. Akasema bwana Mzindakaya, nataka kwanza nikuthibitishie mimi mwenyewe nitakuwa mfano wa kwanza. Akasema na sababu ya kwanza ni moja tu kubwa dhamira yangu kwa nchi yangu nataka iongozwe kwa uadilifu. Ya pili, akasema ni Rais gani mjinga wa ajabu atakayekuwa na tamaa ya utajiri, anasema bwana Mzindakaya, mimi ni raia Mtanzania ambaye nimekwishajaliwa tayari na Watanzania, baada ya miaka mitano hata kama siendi mingine mitano kuwa kumi mimi nitakula na watoto wangu mpaka kufa. Sasa

nataka hela za nini za utajiri? Haya maneno kanitamkia mwenyewe na mimi nasikitika kwamba nimefanya labda makosa kuyasema lakini nasema kwa nia njema. Kwa hiyo, mimi nasema imani ya Watanzania iko kwa Serikali yao na nadhani twende kwa kuanzia sheria hii ambayo inapitishwa. Sasa baada ya hapo mimi nilikuwa na wazo kwamba Serikali tukubaliane kwamba ama tufanye mambo yote mawili, yale yanayotangazwa hadharani kwamba yamekutikana yote kwa hesabu hiyo hiyo vile matokeo yatangazwe kwa sababu tuhuma zinazotangazwa ni nyingi kuliko matokeo. Kwa mfano, *anticorruption* au hata polisi wanapokamata kesi za aina yoyote wanatangaza. Lakini hakuna matangazo ya kutoa matokeo. Sasa watu wanakuwa na mashaka, haya mambo yote haya yanakwenda wapi, umwamini nani? Msululu wa matangazo tumetangaza kesi hii, tumekamata rushwa hii, lakini matokeo hayajulikani. Kwa hiyo, ningependa jambo hili nalo tuwe waangalifu.

Vile vile rushwa tunaijua sisi hapa kwa mfano sisi tulikwenda Botswana, Botswana wanasifiwa sana kwa kupunguza rushwa. Wao walichofanya mishahara mizuri kwa watendaji wa Serikali, *Principal Secretary* analipwa mshahara mkubwa kuliko Waziri wake lakini haruhusiwi kuendesha biashara. Anatakiwa afanye kazi ya kufanya maamuzi ya kuendesha shughuli za Serikali, mshahara mzuri sana lakini haruhusiwi kufanya biashara. Askari polisi na wengine wote huyu akila rushwa wenzako watajua. Kwa hiyo, wale watu wadogo wadogo ambao wanahusika na huduma kwa wananchi ndiyo wanaotunzwa vizuri, wanalipwa vizuri. Sasa sisi mpaka sasa kesi nyingi ambazo tunazijua hata wananchi wanazijua ni za manesi na ma-*traffic* na hizi za kushikisha watu unga. Hizo kesi zimepitwa na wakati, hiyo siyo rushwa, ni ndogo mno na haiwezekani sisi Wabunge, tukaja kutoka jasho hapa kwa ajili ya kesi za shilingi 20,000, shilingi 30,000 kushikisha watu ni za zamani hizo hazina tija kwa nchi, hizo ni unyonge za umaskini tu. Tunataka sasa twende hatua ya pili ya kushughulika na rushwa kubwa za Mikataba, za mtu aliyepata cheo leo, baada ya miaka mitano ana nyumba kumi nzuri. Kwa hiyo, hapo mimi nadhani ndiyo tutakuwa tumeanza kazi yenyewe. Huko ni *very scientific* siyo hii ya unga mnatembea na noti mnamvizia mtu, mnapaka unga halafu mnamshikisha, ni mambo ya zamani hayo. Kote huko tunakwenda hakuna. Siyo wadogo tu sasa, mbona wakubwa wa shilingi milioni 100 hatujawaona, kwani hawapo? Ila wa unga tu 30,000/=, 20,000/=, 50,000/=, 60,000/= ndiyo wapo? Kwa hiyo, mimi nataka tuanze kwenda mbele katika mambo makubwa yenye maana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo ningependa kumalizia kwa kusema kwamba suala la rushwa tusilifanyie mchezo. Lakini pia lazima tukubaliane kwamba lazima tulichangamkie wote. Tusionyeshe kidole kwa Serikali na Serikali mtukubali baadhi tukitoa tundu tuna uwezo wa kujua habari na kuzileta kwenu na tukizileta mchukue hatua, msipochukua hatua tunaleta Bungeni, maana mimi kwa mfano kuna Waziri mimi nilishampa habari sasa ni miezi minne hajachukua hatua. Siku nikizileta humu Bungeni asilalamike. *(Makofi)*

Maana zina ushahidi. Sasa mimi nangoja, wala hata kuniandikia bwana na-*acknowledge* niliipata, amenyamaza! Sasa siku ile nikija kufumua mambo, huyu asianze kusema oh, tunawatafuta watu! Ah! Aha! ndiyo kazi mmetupa leo kwa Sheria hii! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. *(Kicheko/Makofi)*

**MHE. DR. ZAINAB A. GAMA:** Ahsante Mheshimiwa Mwenyekiti. Kwa bahati mbaya kabisa, kama walivyosema asubuhi, nilijiweka tayari kwa Jumatatu. Lakini kwa sababu mimi sio mgeni wa masuala haya, nitazungumza. Mtanisamehe sitakuwa na uchambuzi ule wa kipengele kwa kipengele. Lakini nitazungumza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa naomba kutoa pole na rambirambi kwa familia ya Dr. Chiduo, Mwenyezi Mungu aiweke roho ya Marehemu Dr. Chiduo mahali pema Peponi. Ni Mwalimu wangu, aliyenifikisha hapa.

Napenda kumpongeza kaka yangu Abdallah Mtutura kwa kushinda ushindi wa kishindo. Lakini naomba niishukuru Serikali kwa kuunga mkono kukisaidia na kukipa moyo Chama cha Wabunge cha Kupambana na Rushwa. Wangekosa wao kutupa moyo, sisi tusingefanya ule Mkutano uliowahamasisha wadau wengi na Wabunge wengi na matokeo mnayaona, watu wengi wanachangia. Mimi naomba niwapongeze sana. *(Makofi)*

Lakini naomba pia niwapongeze *International Donor Partners* waliotusaidia kipesa mpaka Mkutano huu ukafanyika. Ushauri wangu kwa Wabunge isiwe tu Sheria hii, naomba sisi wenyewe tukishaona zile sheria zilizosomwa mara ya kwanza hazijaendelea mara ya pili na ya tatu tukaenda nazo nyumbani, tutafute wataalamu ili tuweze kuja ndani ya Bunge hili tuchangie vizuri. Huo ndio ushauri wangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutunga Sheria ni jambo moja, hiyo ni pamoja na kuweka chombo, ambalo ni jambo moja la kusaidia rushwa, lakini jambo la pili, inachosemwa ni *systemic approach.* Mnaweza kuwa na rushwa, mnaweza kuwa na chombo, lakini mipango yenu ya kushughulikia mambo ikiwa siyo mizuri, rushwa itaendelea. Nami nawaomba Wabunge, sheria zote zinazokuja Bungeni tutazame na tumwombe Spika atusaidie kuichanganua na kuondoa *loop holes* zote za rushwa ndani yake. Mimi hilo ninawaomba sana.

Lakini leo nimesimama kuzungumza kama mmoja wa Wabunge wa *African Parliamentary Network Against Corruption (APNAC).* Kwa hiyo, yaliyozungumzwa na *opposition* na Waheshimiwa Wabunge wenzangu ni sisi ndio tuliokaa tukayachambua, kwa hiyo, ni maoni ya Waheshimiwa Wabunge pamoja na wadau mbalimbali ambao wengi walichangia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kama inawezekana, nia na madhumuni ya Serikali ni kusikiliza wadau, wananchi yale wanayoona limeshikiliwa bango kubwa wananchi wanalitaka, naomba basi itekeleze, isipotekeleza Serikali inawekewa *querry.* Nimesikitika sana wakati kaka yangu Hamad na habati amesoma yeye, nilitaka niisome mimi. Alipoisoma ile ripoti ya mwaka 2004, ilionesha Wizara mbalimbali ambazo zinahusika katika masuala ya rushwa katika Wizara, ya pili ni ya Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri Mkuu ndiye Msimamizi wa Shughuli za Bunge Bungeni. Mimi namwomba asikilize kilio cha wananchi, vile vipengele vichache ambavyo vimeonekana kwa nguvu nyingi kabisa, wananchi wameomba na Bunge limeomba, basi fikiria, ama sio wataweka neno *question mark* kwa sababu ripoti imeonesha ni Wizara ya pili. Ombi langu hilo kwake sina nia mbaya, tumsaidie kaka yetu Kikwete, sisi watu wa Mkoa wa Pwani tunamfahamu Kikwete. Amepata Uwaziri wa kila aina, lakini ukienda kutazama mali aliyokuwa nayo inasikitisha. *(Makofi)*

Watu wa Serikali walipokwenda kwenye nyumba yake ile ya zamani ambayo ndiyo alikuwa anakaa, wakakuta anapikia mkaa, wakasema hii, hata huyu Waziri wa Mambo ya Nchi za Nje anapikia mkaa badala ya kupikia umeme na gesi kuonyesha ni mtu wa aina gani. *(Makofi)*

Nia yake ni kweli kupambana na rushwa, lakini kumbukeni ni mtu mmoja. Viongozi aliowateua msaidieni! Bunge bila aibu tumsaidie, ana nia njema kwa Watanzania! Baada ya kusema hivyo, naomba sasa niende pole pole. Tumesema hivi, *DPP* asiingilie shughuli za *PCB.* Sheria hii ambayo kwa bahati mbaya imewekwa katika Katiba ni moja ya *loop holes* ya rushwa. *PCB* wana wataalamu wengi Wanasheria, wana ma-*prosecutor* wengi kuliko *DPP*, wana-*investigate* kwa pesa nyingi za Serikali. Lakini mwisho wa siku wanasema *no,* huyu mtu huyu, hii Idara moja ndiyo itakudhibiti! Hapana!

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaiweka sura ya nchi hii pabaya. Tumesaini mkataba wa kupambana na rushwa wa *UN,* kuna kipengele kinasema hivi: "Chombo hiki kiwe *independent",* tukifanye kiwe kina-*compromise* kazi zake. Mimi naomba kiwe *independent.* Hii mimi nashauri kabisa kweli kumweka *DPP* haiipi sura nzuri Serikali na inaonekana mnamdanganya Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete. *(Makofi)*

Ushauri wangu ni kwamba, kwa sababu mmeweka kwenye Katiba nikizungumza *against* sitaeleweka. Sasa naomba kushauri kwamba katika sheria hii tuweke kipengele kinachosema *DPP* asipotoa sababu katika siku 30 kwa nini *PCB* imefanya *investigation* kwa hela nyingi ya Serikali, asipotoa sababu kwa siku 30 *PCB* ichukulie amekubali na aendelee ku-*prosecute.* La sivyo na *PCB* kama haikuridhika na ina ushahidi wa kutosha iende Mahakamani ikapinge amri hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nazungumza kwa uchungu sana. *APNAC* tumeishauri Serikali tangu mwaka 2001 katika *resolutions* mtakuta tunasema, hapana! Mnasema oh!! Kuna wanaoweza wakasingiziwa, watu wakaonewa kama hamuamini *PCB*, mnaiaminije *DPP?* Tuambie mmeweka kitu gani ili *DPP* aonekane ana imani. Yeye ni binadamu na tuna wasiwasi na huu ni wasiwasi wangu na wananchi. Inawezekana imewekwa kipengele hiki kuwalinda wakubwa na ni *corruption* kubwa inakotokea. *(Makofi)*

Kwa hiyo, mimi nilikuwa nashauri, ikiwezekana tuweke siku 30 huyu mtu aieleze *PCB* na alieleze Bunge ikiwezekana kwa maana ya Kamati Maalumu ya Bunge. Kwa nini amesema kwenye suala hili? Tunaomba ripoti ya *PCB* iwekewe Kamati Maalumu ya Bunge tufahamu kuna siri gani kuona hawa watu wanaotunyanyasa, wanaokula hela,

kuna siri gani? Kama inamhusu Dr. Gama awekwe pale. Tusizungumze kwenye Bunge, tunaweza ku-*victimize,* lakini Kamati Maalumu iwe siri, kama inamhusu Waziri Mkuu tuweke pale. Ndiyo! Tuombe hiyo! Samahani Mheshimiwa Waziri Mkuu, natoa mfano tu. Sina maana mbaya na ndiyo maana nimejiweka mimi, nikakuweka na wewe. Waziri Mkuu ni mdogo wangu, hamna tatizo. *(Kicheko/Makofi)*

Kwa hiyo, hiyo ni moja. Lakini la pili ni suala la ajira ya huyu *Director General* na *Senior Officers.* Kwanza uajiri wao uwe *transparent,* itangazwe, tuweke *qualifications.* Ikishatangazwa, wale ambao wanamshauri Rais watatazama, katika matangazo haya huyu ndiye ana-*qualify* lakini mara ngapi tumekuta watu wamemshauri Rais lakini mwisho wa siku Rais akateua mtu mbovu. Sasa mimi nilikuwa naomba, hata Bunge lihusike kwa sababu katika *APNAC* tumesema katika *appointment* za *Senior Officers* na tukatoa mifano iletwe Bungeni kama Bunge la Uganda kama linavyofanya. Kwa nini tunakataa? Nina wasiwasi kuondolewa madarakani.

Huyu mtu jamani anafanya kazi nzito, anamwona Dr. Gama kala rushwa,. Dr. Gama, huyu Mbunge nikiinuka hapa naweza nikampigia maneno hapa na akaambiwa na Rais simama, tumwekee kipengele cha kumlinda. Huyu *DG* pamoja na *other Senior Officers* tuwalinde jamani kipengele kiseme kabisa kama kilivyo katika kipengele cha Majaji, bajeti yao, ikiletwa Bungeni ikapitishwam tufanye kitu kimoja, tusiidokoe dokoe vi-*allocation,* isiwepo. *(Makofi)*

Tunachokitaka, kama kunatokea kuna matatizo ya nchi, hela inabidi ipunguzwe, basi ipunguzwe *evenly.* Lakini kama kuna matatizo hayo, pesa yao isidokolewe na wapewe basi nafasi kupitia huko huko Serikalini waombewe msaada mahali. Kwenye mkakati wa kupambana na rushwa umesema, Bunge mnatakiwa msimamie mikataba yote inayohusu mambo yenye mapesa makubwa lakini kwa sababu ya *loop hole* hiyo hiyo, unakuta unaambiwa aha *ACT* mkataba wake hauruhusiwi! Siri! Hili Bunge kweli lina meno hili? *(Makofi)*

Kwa bahati mbaya, sisi Wabunge, mimi nitakuwa wa mwanzo yale mapendekezo yaliyotolewa pale, *unless* tuambiwe na Spika kwa nini yasiletwe. Labda Spika wenyewe ana matatizo yake. Mimi naomba nisimtuhumu mtu mwingine, nitamtuhumu Spika kwa sababu tumetumia pesa zetu nyingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu adhabu, mimi nasema tuondoe, tumwachie Jaji atoe kiwango cha juu kulingana na kosa. Lakini ukiniuliza mimi, nasema adhabu ya pesa iondolewe kabisa! Iwe kifungo moja kwa moja! Maana yake ukimfunga mtu hata miezi sita, umemvunjia heshima yake yote. Tuondoe adhabu ya pesa. Hilo ni ushauri wangu mie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *procurement* inaniuma. Masuala ya mikataba na tenda inaniuma! Naomba nikupe mfano na nitaisema *live,* hata nikiambiwa nina mdomo nisiyokuwa na *break.* Nakupa mfano wangu mwenyewe, naomba niseme *I am interested on this.* Mimi nimempelekea Waziri mhusika wa *TAMISEMI,* kuna hela Shilingi milioni 300 ya kununua gari la Zimamoto bila ya amri ya Halmashauri imepelekwa kwenye

*CRDB* na Mkoa wa Pwani hatuna *CRDB,* maana yake imekwenda Dar es Salaam gari mpaka leo halipo. Waziri nimemwambia, nimeuliza kule kwenye Halmashauri, *Full Council* sikujibiwa, nijibu wewe Waziri. Akasema nitaifanyia kazi. Mpaka leo sijapata majibu. Sasa kwa nini? Kama binadamu, nasema inawezekana kuna *chain* ya Hazina, TAMISEMI na *DED* wangu. Haya mambo, hata ile sheria ya tenda ndugu zangu ina *loop hole* ya rushwa, kuwalinda baadhi, unamwachia Mwenyekiti asiyekuwa katika Bodi unamwambia asaini. Anasaini nini kitu asichokijua?! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa bahati mbaya kabisa sikupewa nafasi, nilijiandaa Jumatatu na mimi nasema kuhusu suala la *DPP* nimeshaanza, nimeweka marekebisho. Baada ya kusema hilo. Ahsanteni. *(Makofi)*

**MHE. LUCY F. OWENYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia katika Muswada huu. Hata mimi mwenyewe nilikuwa nafikiri nitachangia Jumatatu. Kwa sababu mwanzo Mheshimiwa Spika alikuwa amewataja wachangiaji wanne tu. Kwa hiyo, sikujua kwamba nitachangia leo, lakini nitaendelea.

Awali ya yote, napenda nimpongeze Mheshimiwa Marmo kwa kuuleta Muswada huu pamoja na *PCB* na wafanyakazi wote wa Wizara yake kwa kuuandaa Muswada huu ambao umekuja kwa wakati muafaka kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la rushwa siyo geni katika nchi hii ya Tanzania. Miaka mingi iliyopita zaidi ya 40 tumekuwa tukizungumzia adui watatu ambao ni maradhi, ugonjwa na umaskini. Kwa busara za Mwalimu Nyerere akaongeza hiki kiadui kingine ambacho ni rushwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, rushwa inazungumzwa na Taasisi nyingi, hata Taasisi za Dini, vitabu vitakatifu, vinazungumzia kwamba rushwa ni adui wa haki. Anayepokea na kutoa rushwa ni dhambi. Naomba niwarudishe nyuma kidogo, wakati wa Azimio la Arusha lilipotengenezwa lilisisitiza maadili ya viongozi wa nchi pamoja na uendeshaji wa uchumi katika nchi yetu na ilisisitiza siasa ya ujamaa na kujitegemea. *(Makofi)*

Baada ya hapo, likaja Azimio la Zanzibar ambalo *document* yake sijawahi kuipata na kama ipo ningependa kuiona. Azimio la Zanzibar nafikiri lilikuwa linazungumzia zaidi ubepari kama sikosei. Sasa Wajumbe wengi waliotangulia wamekuwa wanalalamika kuhusu mikataba mibovu ya madini.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa kuhusu utaratibu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa kaa chini Mheshimiwa Owenya, kuna taarifa ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu Na. 50 kinasema kwamba: "Ni marufuku kabisa kwa Mbunge kusema uongo na

kwamba ni lazima Mbunge atawajibika kuwa na uhakika wa maelezo anayoyatoa ni sahihi na siyo mambo ya kubuni, au ya kubahatisha.” *(Makofi)*

Sasa kama Mheshimiwa Mbunge anasema kwamba Azimio la Zanzibar ni kuhusu ubepari, tena anasema nadhani, naomba afute usemi wake au athibitishe kitu anachokisema. *(Makofi)*

**MHE. LUCY F. OWENYA:** *Okay!* Nafuta usemi wangu, lakini naomba nipatiwe Azimio la Zanzibar. *(Kicheko/Makofi)*

Naweza kuendelea?

**MWENYEKITI:** Endelea.

**MHE. LUCY F. OWENYA:** Nashukuru. Kwa sababu ya mikataba mibovu ambayo kila mchangiaji amekuwa akilalamika kama mikataba ya Madini, mikataba ya umeme, pamoja na uuzaji wa nyumba za Serikali, tumeona kwamba nyumba za Serikali zimeuzwa *within three months,* unakuta nyumba imeshakuwa kubwa. Tunashangaa hawa wafanyakazi wa Serikali wamepata wapi hizo za kubadilisha hizo nyumba. Hii inaonyesha kwamba kuna mianya ya rushwa ndani yake. Kwangu mimi naona hizi ni rushwa kubwa ambazo Serikali inabidi ichunguze na iangalie watu hawa walipataje fedha hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile tunabidi tutofautishe hizi rushwa kubwa na rushwa na ndogo. Kuna hizi rushwa ndogo ambazo ni za wananchi wa kawaida ambazo hazimsaidii mwananchi wa kawaida. Unakuta mtu anakwenda kwenye huduma za kijamii, tumeona hata kwenye *television* wanaonyesha kwamba watu wanaulizwa rushwa kama mahospitalini, Mahakamani, inabidi mtu alipe kitu kidogo ili aweze kupata huduma hiyo ambayo kwa hakika hii ni haki yake kimsingi kupewa huduma ile, lakini unakuta unaulizwa rushwa.

Kitu kingine ambacho Muswada huu umezungumzia ni kuhusu ule uteuzi wa Bodi. Ule uteuzi wa Bodi umefutwa, lakini mimi sioni kama hii ni *solution* ya kufanya Tume iwe Huru na Haki. Mimi nilikuwepo katika mjadala wa kuzungumzia kuhusu Muswada huu wa rushwa. Wadau wengi walikuwa wanasema wale Wajumbe wa Bodi wawe huru, watoke kwenye vyombo vya dini, kijamii kwenye *private sector* lakini wasiwe ni watumishi wa Serikali. Hii ndiyo itawasaidia waweze kufanya kazi kwa uhuru zaidi. Lakini pakiwa hakuna Bodi kabisa, mimi nafiriki *PCB* haiwezi kuwa huru na *PCB* ikipeleka malalamiko yake kwenye hii Bodi na hii Bodi ilete malalamiko yake Bungeni na Bunge lijadili na sisi tuweze kupeleka kwa Rais, nafikiri hii itakuwa ni Tume Huru na Mkurugenzi wa *PCB* atakuwa na uhuru zaidi wa kufanya kazi zake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la *DPP*, mimi nafikiri *DPP* asihusishwe kwenye kushtaki au kuangalia kama muhusika kweli amefanya kosa la rushwa. *PCB* ipeleke malalamishi yake *direct* kule Mahakamani. *(Makofi)*

Vile vile kuhusu kutozwa faini za wale ambao wanafanya makosa. Unaweza kukuta mtu mwingine ni tajiri sana na amekula rushwa, faini ya shilingi milioni 20, milioni 15 siyo faini kubwa sana. Mimi nam-*support* kabisa Mheshimiwa Gama, mtu ambaye anafanya kosa la rushwa, afungwe na asitoe faini kwa sababu faini shilingi milioni 20, shilingi milioni 15 ni kitu kidogo sana kwa wafanyabiashara wa sasa hivi.

Vile vile ili kuweza kufanikisha huu Muswada wa Rushwa, mimi naomba Serikai iweke wazi ile Ripoti ya Tume ya Warioba, itasaidia sana *PCB* kufanya kazi yake kwa ufanisi zaidi. Vile vile jamii iweze kuelimishwa na ihusishwe, waelewe kwamba rushwa siyo kitu kizuri. Rushwa ni kitu kibaya. Elimu iwepo, jamii ijumlishwe pamoja, wananchi wanaweza kuelimishwa kwa kupitia Makanisani, elimu za awali, mitaala ya elimu pia kuwe na elimu ya rushwa, Madrasa na *Sunday School.* Watu wote hawa watawafundisha maadili mazuri na watoto watakuwa wakielewa kwamba rushwa ni adui wa haki. Kwa sasa hivi unakuta mtu mzima, ameshazoea rushwa. Kumkunja samaki aliyekauka siyo rahisi, lakini hawa wadogo wadogo, tukianza nao watakuwa na maadili kwamba wanaelewa rushwa ni adui wa haki. *(Makofi)*

Vile vile ningeshauri hii taasisi ianzishwe Kikatiba, kama Tume ya Haki za Binadamu ilivyo kwenye Katiba na fedha za matumizi, fedha za *PCB* ziletwe Bungeni tuzipitishe na zisiwe na masharti yoyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naomba kuwasilisha. Nilikuwa sijajiandaa vizuri. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Tunakushukuru Mheshimiwa Lucy Owenya.

Waheshimiwa Wabunge, katika orodha yangu, wasemaji wengi waliokuwa wameomba kwa leo ni wanaume. Kwa hiyo, nilijitahidi kujaribu kupandisha kidogo baadhi ya majina ya akina mama waliokuwa wameomba. Mheshimiwa Richard Nyaulawa, atafuatiwa na Mheshimiwa Mnyaa, atakayefuatiwa na Mheshimiwa Juma Njwayo na Mheshimiwa Binilith Mahenge.

Kuna akina mama walioomba ambao ningependa kujua waniandikie endapo wako tayari au wanataka kuongea Jumatatu, Stella Manyanya na Mheshimiwa Beatrice Matumbo Shellukindo.

**MHE. RICHARD S. NYAULAWA:** Ahsante Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia katika Muswada huu. Kabla ya kuchangia, kwanza nilitaka nitoe salamu za rambi rambi kwa kifo cha Mheshimiwa Chiduo. Nawapa pole sana familia yake.

Lakini pili, natoa pongezi sana kwa Mheshimiwa Mtutura kwa kupita kwa kishindo katika Jimbo la Tunduru. Nina imani kwamba wananchi wamempa kazi kubwa ya kuweza kushiriki katika shughuli zao za maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo ningetaka kuipongeza sana Serikali kwa kuleta Muswada huu ambao nina imani kwamba umekuja katika muda muafaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, rushwa ni adui wa haki na rushwa ni aghali sana kwa kuwa watu hudhulumiwa. Kwa kuwa watu wengi ambao wamefungwa, wamefungwa kwa makosa lakini ni kwa sababu kumekuwa na matatizo ya rushwa na inasemekana kwamba zaidi ya asilimia 40 ya watu waliofungwa sio wahalifu, lakini ni watu ambao wako humo ndani kwa sababu ya rushwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, rushwa hupunguza sana kazi za maendeleo. Lakini vile vile inafanya rasimali zetu ziende mahali ambako hakustahili. Imefika mahali ambapo rushwa katika nchi yetu imekuwa ni kama utamaduni. Kwa maana ya kwamba watu ambao wanapata rushwa na kisha wakatajirika haraka haraka huwa wanaitwa wajanja. Wale ambao wanafanya kazi yao bila kupokea rushwa, huwa wanaitwa wajinga.

Sasa natumaini hii ni hali ambayo inasikitisha sana katika nchi yetu kwa maana ya kwamba, tabia na utamaduni wa nchi umefika mahali ambapo rushwa tumeona ni kama njia sahihi ya kuweza kujipatia utajiri wa haraka haraka. Sasa kama hilo limeanza kujitokeza, hivyo basi matatizo yetu ni makubwa.

Lakini nina imani kwamba kutokana na matatizo yote haya ambayo ni makubwa, Serikali imeleta muswada huu ili tuweze kuufanyia kazi na kuweza kuupitisha. Katika muswada, kazi za Taasisi zimeainishwa. Kazi mojawapo katika kifungu cha saba kinaeleza kwamba kazi za taasisi itakuwa ni kushauri na kuchunguza taasisi za umma na mashirika ya umma pamoja na makampuni binafsi kuhusu mwenendo na tabia zao katika shughuli za rushwa. Lakini katika kipengele hiki, hawaelezei kuhusu watu binafsi, kwa sababu nafikiri watu binafsi vile vile wanaweza kuwa wanahusika kwa kiwango kikubwa sana katika masuala ya rushwa na wao wasipochunguzwa inawezekana kukawa na matatizo ya aina moja au nyingine. Kwa hiyo, kuwe na Taasisi, lakini vile vile na watu binafsi waweze kuchunguzwa vile vile.

Katika kipengele Na. 7 chini ya kazi za Taasisi, kuna maelezo kuhusu kazi za Taasisi kwamba ni kuchunguza na kufungua mashtaka baada ya kupata ushauri kutoka kwa *DPP*. Natumaini wenzangu wengi wamelizungumzia suala hili na natumaini wengi tunachoshauri hapa ni kwamba *DPP* asiingie katika masuala ya rushwa. *(Makofi)*

Cha msingi ambacho kinastahili kufanyika na wote tunajua kwamba kwa muda mrefu kumekuwa na kesi nyingi sana ambazo zinaendeshwa na *DPP*. Wana kesi inavyoelekea ambazo ziko nje ya uwezo wao. Kwa hiyo, kwa kupewa majukumu mengine ni kuwaongezea mzigo. Lakini wote tunaelewa kwamba kuna kesi nyingi ambazo zinachukua muda mrefu kuliko inavyostahili. Huwa wanasema kama haki isipofanyika katika muda muafaka, basi haki hiyo inakuwa haitolewi. Mimi nilikuwa nafikiria kwamba itakuwa ni vizuri kwamba Taasisi ya Rushwa iwe na majukumu ya kuweza kuchukua kesi hizo Mahakamani moja kwa moja na kama wakipewa *DPP* maana yake ni kwamba hiyo kazi inarudiwa mara ya pili.

Kwa sababu watu wa rushwa wameshafanya uchunguzi, wamekusanya habari zote, lakini baada ya kukusanya habari hizo wanampelekea mtu wa *DPP* na huyo naye anaanza kufanya kazi upya. Kwa hiyo, kwa kazi hiyo hiyo inarudiwa mara mbili na kwa upande wa Serikali natumaini inakuwa ni gharama mara mbili.

Kwa hiyo, ili kupunguza gharama hizo ingekuwa ni vizuri na tungeshauri kwamba Taasisi ya Rushwa ipewe meno, kwani kwa sasa hivi haina meno na wakati mwingine hata wafanyakazi wanaohusika na rushwa wanakuwa *frustrated,* wanapata matatizo kwa sababu wanaona kazi yote ambao wameifanya haichukuliwi hatua wala hazifikii mwishoni. Kwa hiyo, kunakuwa na *frustrastration* ndani ya Taasisi na wakati mwingine inaweza kupunguza hata kasi zao za kuweza kufanya kazi vizuri.

Kwa hiyo, ili kuweza kukamilisha kazi sawasawa na kuwapa uwezo ni kuwapa meno ya kuweza kuwa na uwezo wa kushtaki watu ambao wanatuhumiwa kwamba wamekula rushwa. Lakini ili kuweza kufanya hivyo, nafikiri itakuwa ni vizuri kama tukiweza kujenga vizuri uwezo wa taasisi hiyo, kwa maana ya mafunzo ili waweza kuwa na uwezo mkubwa wa kuweza kuzishughulikia kesi hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu ambao wanahusika zaidi wangekuwa na uwezo zaidi wa kutoa taarifa ni watu wa kawaida tu ambao wanafanya kazi katika Serikali, katika Mashirika ya Umma, Mashirika ya watu binafsi ambako kuna matendo mbalimbali ambayo yanahusiana na rushwa. Lakini ili watu hawa waweze kutoa taarifa mbalimbali zinazohusiana na rushwa wanastahili kujengewa mazingira ambayo yanaweza kuwafanya watoe taarifa hizo, lakini vilevile wawe na usalama.

Kwa hiyo, tunaweza kupata taarifa nyingi za kujua kuhusu rushwa zinazofanyika katika mashirika yetu pale ambapo tunaweza kujenga mazingira mazuri, kuhusu rushwa zinazofanyika katika mashirika yetu, lakini vilevile tukawawezesha wale watu ambao wanatoa taarifa. Hawa watu ni muhimu katika jamii kwa sababu inawezekana kwamba taasisi kama taasisi

peke yake haiwezi kufanya kazi bila kushirikiana na hawa watu wanaoweza kutoa taarifa mbalimbali, huwa wanaitwa *whistle blowers.* Kwa hiyo, ingekuwa ni vizuri tungeweza kuwajengea mazingira kwa kuweza kufanya kazi hiyo vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa rushwa zipo za aina mbalimbali. Kuna rushwa ndogo ambayo madhara yake ni makubwa, lakini vilevile kuna rushwa kubwa, *grand corruption*, madhara yake ni makubwa zaidi. Kwa hiyo, hivi viwango vya adhabu ambavyo vimetolewa vinastahili kuangaliwa zaidi na ninatumaini faini ya shilingi milioni tano au milioni 10 au hata milioni 15 ingeweza kuwa ni faini nzuri kwa wala rushwa wadogo wadogo. Kwa sababu nia hapa ni kutaka kuzuia rushwa isifanyike, sasa kama faini itakuwa katika uwezo wa kulipa bila matatizo ya aina yoyote, basi inawezekana wala rushwa wataendelea kuwepo. Tutakuwa hatujajenga mazingira mazuri ya kuzuia rushwa.

Lakini inapokuja kwenye *grand corruption,* mimi nafikiri kiwango kingekuwa kikubwa sana. Tukichukua suala la mikataba, mikataba mikubwa ya mabilioni, ambapo mtu anaweza kupata labda tukasema asilimia 10 kwamba ndiyo rushwa, malipo hayo yanaweza kuwa ni milioni 400 au milioni 500, wewe unampa faini ya shilingi milioni 15. Huyu ataendelea kwenda kwenye mikataba ya rushwa au ataacha? Maana yake katika shilingi milioni 500 akienda kulipa faini ya shilingi milioni 15 haimpi matatizo ya aina yoyote yale, huyu ni mtu ambaye ataendelea kula rushwa siku hadi siku kwa sababu ana uwezo wa kuweza kuilipia faini kwa kutumia fedha hizo za rushwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mara nyingi labda kiwango cha rushwa kinakuwa hakijulikani. Kwa hiyo, hata pale tunaposema Serikali inaweza kuchukua au kurejesha kiasi cha rushwa kilichopatikana, inawezekana isiwe rahisi. Kwa hiyo, kwa ushauri wangu, nilikuwa nafikiria ili kuweza kuzuia rushwa kabisa, adhabu zinazostahili kutolewa, zinastahili kuwa kubwa kuliko hizi ambazo zimeonyeshwa.

Nilikuwa nafikiria labda badala ya kusema *not exceeding* bila shaka ilistahili kuwa *not less than,* kwa neno *'exceeding'* liwe *'not less'.* Hapo tutakuwa tumeanza kufanya kazi ya kuweza kupigana na rushwa, lakini hivi inawezekana kwamba kwenye kipengele kinachohusiana na mambo ya adhabu, inawezekana kwamba ndiyo mahali ambapo tunaweza kuwa tuna-*encourage* rushwa kuongezeka au kupungua. Kama tukitaka kufanya kazi sawa sawa lazima adhabu ziwe zinaonekana kwamba zinamzuia mtu kufanya shughuli za rushwa. Rushwa isionekane kama ni sehemu ya biashara, lakini pale anapofanya biashara ya rushwa akapata faida na akalipa faini ndogo, huyu mtu ataendelea kufanya kazi ya rushwa mara kwa mara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ningeomba katika hilo, basi labda Muswada huu uliangalie kwa undani zaidi. Baada ya mchango huo na mimi naunga mkono Muswada huu na ningependa kumalizia hapo, ahsante.

**MHE. MOHAMMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia nafasi hii na mimi ingawa nilikuwa katika kundi la kujiandaa Jumatatu, lakini nitajitahidi sitokosa la kusema.

Kwanza na mimi ni vyema niungane na Wabunge wenzangu kutoa rambirambi za Marehemu Aaron Chiduo, Mungu ailaze roho yake mahali pema peponi.

Pili, nachukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Phares Kabuye kwa kuchaguliwa kuwa Makamu Mwenyekiti wa Chama cha *TLP*. Baada ya hayo ningependa kuanza mchango wangu, kwanza kwa kuzitambua au kwa kuutambua mchango wa Kambi ya Upinzani na mchango wa Kambi ya Upinzani mna masuala muhimu mazito katika Muswada huu naomba yapewe *priority* kuzingatiwa.

Baada ya hapo, ningejaribu kutaka kuchangia sehemu ya kwanza ambayo nasikitika wachangiaji wote waliotangulia hakuna aliyechangia kipengele hicho. Sasa sijui kwa sababu gani! Lakini inawezekana wengine watakaofuata watachangia. Katika

Muswada, Ibara ya 2(1) inazungumza sheria hii au Muswada huu utatumika Tanzania Bara tu.

Mimi kidogo nina wasiwasi na sikubaliani na hilo na vyema jambo zuri kama hili la kuzuia rushwa ni kwanini litumike Tanzania Bara tu lisitumike Tanzania Visiwani pia? Ikiwa wenzetu huku wa upande mmoja wa Jamhuri wanapenda mambo mazuri kama haya ya kuzuia rushwa, kwanini basi yasizuiwe kule kwetu pia? Kwanini tusitumie nafasi hii kwamba itumike sheria hii mpaka Tanzania Visiwani? *(Makofi)*

Kuna sababu nyingi zaidi ya hiyo. Kwanza tuliporidhia *United Nation Resolution* kuhusu mambo haya ya kupambana na rushwa, tulisaini kama *United Republic,* hatukusaini kama Tanzania Bara. Kwa maana hiyo, moja katika sababu ambapo tunahitajika tupambane sote kwa pamoja kama *United Republic including* Zanzibar ni kwa sababu hiyo moja. Lakini ziko sababu nyingine. Nani anafanya rushwa? Ng'ombe hafanyi rushwa, mbuzi hafanyi rushwa, ni binadamu anayefanya rushwa au Serikali ndiyo zinazofanya rushwa. *(Makofi)*

Sasa ikiwa utasema Muswada huu utumike Tanzania Bara tu na sisi Tanzania Bara hakuna raia wa Tanzania Bara, tuna raia wa Tanzania vipi una-*exclude* Zanzibar katika suala hili? Zanzibar kama ni watu au ni Wizara za Muungano ziliyopo na hata zisizo za Muungano, Jamhuri yetu sasa hivi huwezi kutofautisha *movement* ya watu na hawa watu ndiyo wanaotenda hizi rushwa.

Ibara hii ya 2(1) inapingana na Ibara 2(2) inayozungumzia kwamba sheria hii inaweza kutumika kwa mtu yeyote nje ya Tanzania. Sasa hapa ni mchanganyiko mkubwa, ni balaa kwamba iweze kutumika, mtu amefanya kosa yuko nje ya nchi, lakini isitumike Zanzibar, ni jambo ambalo linaonyesha la ajabu hapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ningeomba suala hili litazamwe upya na Muswada huu tuupitishe kwa kuwa ime-*include* Zanzibar, kweli iwe *included*.

Sababu nyingine hapo hapo ya kutaka Muswada huu utumike mpaka Zanzibar, tuna Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje na Ushirikiano wa Kimataifa. Ni masuala mengi tu ambayo Zanzibar haiwezi kwenda kule ku-*negotiate a loan*, ni mambo machache sana Zanzibar yanayoweza ku-*negotiate a loan*. Wanaokerwa na rushwa sio Watanzania tu na hao wafadhili wanayotupa hiyo misaada wanakerwa na rushwa na Tanzania ikienda ku-*negotiate* hiyo asilimia 4.5 inamegwa inapelekwa Zanzibar, nayo ni pesa ya Wafadhili. Wafadhili hao hao wanaokerwa na rushwa utasemaje sasa Muswada huu utumike Tanzania Bara tu usitumike Zanzibar? Mbona na sisi tunazipata japo hicho kidogo cha asilimia kinachotokana na wafadhili, halafu tusitumie Muswada huu utumike Tanzania Bara tu!

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeomba Waziri anayehusika Mheshimiwa Marmo, suala hili alizingatie kwa makini sana. Nashangaa upande mmoja katika taasisi mbalimbali zilizochangia Muswada huu, suala hili waliliona na wakatoa sababu pamoja na kwamba ni tofauti na sababu nilizozitoa mimi, lakini walitoa sababu. Kwa maana

hiyo, suala hili litizamwe na linakuja sawasawa na tulivyopigia kelele Tume ya Haki za Binadamu ambapo hapo mwanzo ilikuwa haifanyi kazi Zanzibar. Mantiki ile ile au sababu zilezile ndiyo zitumike pamoja na hizi sababu nilizozitoa kwamba chombo hiki au Muswada huu au Taasisi hii ifanye kazi mpaka Tanzania Visiwani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 5(2) inazungumzia taasisi hii kuwa huru. Huu uhuru unaozungumziwa hapa ukilinganisha na namna anavyopatikana Mkurugenzi Mkuu na hayo mambo mengi unatia wasiwasi. Ni vyema uhuru huu uelezwe bayana: Je, ni chombo ambacho kina uwezo wa kushitaki na kushitakiwa? Je, ni chombo ambacho kifedha kitajitegemea kifedha, au kitakuwa kinapata ruzuku kutoka Serikalini? Kikiwa kinapata ruzuku Serikalini: Je, uhuru utakuwa wa namna gani? Utakuwa uhuru kamili au utakuwa uhuru kama mengine ambayo tunayaona?

Kipengele hiki ni vyema kifafanuliwe na isitoshe tu suala la uteuzi wa Wajumbe wa taasisi hii ni vyema ingefikiria pia kutoa viongozi kutoka vyama vya upinzani, ndiyo tutasimamia vizuri. Lakini ikiwa hakutakuwa na ile *playing* kwa kuchagua upande mmoja tu kama tunavyoona hizo *board* nyingine na mambo mengine hatuwezi kusema uhuru huu utakamilika. Katika nchi ambayo ina siasa ya vyama vingi nieleze waziwazi kwamba katika madaraka fulani lazima upinzani uhusishwe. Kwa sababu, ikiwa na wapinzani watahusishwa au upinzani utahusishwa, kidogo kama huo uhuru tutaona na hatuwezi kuunyamazia kimya, tutawaeleza sisi patakapokuwa na matatizo. Kwa hiyo, ibara hii ifanyiwe marekebisho ihusishwe na bidhaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu nyingine, Mheshimiwa Mwanri alitoa sababu za kuwa Mheshimiwa Waziri kashindwa ku-*define* rushwa ni nini? Nami nataka niungane naye kwamba rushwa ni suala pana sana, kwa hiyo, yapo mambo ambayo hayajazungumziwa katika Muswada huu, lakini nayo ni aina ya rushwa.

Ni vyema Mheshimiwa Waziri ayaelezee na namna gani hatua zitachukuliwa, kuna rushwa mbali zile za ngono, kuna rushwa za kazi mtu yupo katika Idara fulani ya kazi anaweza akakaa hapo, mtu ambaye namfuatilia kuja akapanda vyeo mara chungu mzima, huyu mwenzake anamwona na wana *same level of education, just* kwa sababu ya kufahamiana au huyu ni mwenzangu, ni mtoto wa nani, mbona haijazungumzia suala hilo? Tunaona na tunashuhudia katika vikosi vya Polisi watu wanapata nafasi kwa matabaka. Kule Zanzibar kuna nafasi zinazotolewa kwenda huko Kigoma na Ngara. Basi kupata nafasi ya Ngara ni kikwazo kwa sababu askari wote kila mmoja anataka hiyo nafasi ya kwenda huko Ngara. Lakini sijui kuna nini? Lakini kuipata hiyo nafasi, basi ni balaa. Ni watu wa tabaka fulani ndio wanaweza kupata nafasi ya kwenda huko. *(Makofi)*

Kwa maana hiyo, hii rushwa ni pana sana itizamwe na sehemu za kazi: Je, haki inatendeka? Je, kuna upendeleo gani unafanyika na kuna mambo mengi sana yanafanyika huko Hazina, hasa katika hizi sehemu za vikosi, kuna rushwa ya aina yake ambayo huwezi kuieleza. Kuna rushwa kubwa sana ya aina yake na zinapelekea nyingine unaweza kusema hata dhuluma. Kwa sababu ikiwa mmeingia kazini siku moja, mna elimu moja lakini mwenzako anapanda vyeo mara kumi zaidi kuliko wewe, unasaga pale

pale tu kwa sababu ya aidha ulikozaliwa, ulikotoka au namna gani. Hiyo nayo ni rushwa ya dhuluma. *(Makofi)*

Ningeomba Waziri anayehusika na suala hili lizingatiwa katika muswada huu. Kwa vile sikujitayarisha leo, kwa hayo tu niliyozungumza nafikiri mchango wangu utasaidia. Kwa hayo, machache na naomba niishie hapa, ahsante. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Tunakushukuru sana Mheshimiwa Mohammed Mnyaa.

Niwakumbushe tu Waheshimiwa Wabunge, kwa wale ambao hawajajiandaa vizuri kuongea leo, kwa sababu *list* yetu ni ndefu, basi waniandikie ili wawe katika *list* ya Jumatatu. Lakini vilevile kwa Mheshimiwa Sophia Simba - Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na watoto na Naibu Spika - Mheshimiwa Anne Makinda Mwenyekiti wa *TWPG* katika *list* niliyonayo ambayo iko tayari kuongea leo ni wanaume watupu. Kwa hiyo, isije ikahesabika kwamba jicho la Mwenyekiti lina makengeza.

**MHE. JUMA H. KILLIMBAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kupata nafasi hii ili nami niweze kuchangia mjadala huu muhimu unaohusu suala la mapambano dhidi ya rushwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, nishukuru waandaaji, hasa Mheshimiwa Waziri, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, anayeshughulika na masuala ya Utawala Bora - Mheshimiwa Marmo. Niwashukuru watendaji wa *PCB* kwa pamoja wakiongozwa na Mkurugenzi wao Mheshimiwa Hosea, kwa mpango mzuri na utaratibu mzuri walioweza kuandaa Muswada huu ambao tunauhitaji kwa wakati huu muhimu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama walivyozungumza wazungumzaji waliopita, rushwa ni donda ndugu na rushwa ni mdudu mbaya sana na hasa anayeweza akaangamiza jamii iliyomaskini na ikaendelea kuwa maskini kwa muda wote. Kwa hiyo, kwa kweli Watanzania kwa hali tuliyonayo, hali ya rushwa inachangiwa sana na kukosekana uaminifu kwa maeneo mbalimbali hasa kwa watu waliopewa dhamana ya kuweza kuongoza nchi, au kuweza kuwa katika nafasi mbalimbali ambazo zinatoa huduma kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naamini Muswada huu utasaidia sana na kuweka sawa *discpline* ya Watendaji wetu na hasa tuweze kufikia malengo yote kwa pamoja hasa yale ya utawala bora na ambayo yanaweza kutufanya tuweze kuondokana na umaskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nizungumzie muswada wenyewe kama ulivyo, nikianza na pale panaposema *"Establish the Board",* hasa *Board* yenyewe baada ya kuzungumza *part three* kipengele cha 15 kifungu 2(b). Hapo tumetaja Wajumbe wa Bodi na katika kuwataja, pale panaposema *"Civil Society"*, nilikuwa naomba paonyeshwe waziwazi kwamba hizi *Civil Society*, ni *Civil Society* zipi? Ni lazima ziwe ni zile zinazopambana na masuala ya rushwa. Kwa sababu tunazo *Civil Society* za aina nyingi, tunazo zinazojikita na masuala ya wakulima tu, zipo nyingine ambazo zimekijikita

kwenye masuala ya UKIMWI, lakini ningeomba katika sehemu hii pale kwenye *Civil Society* paeleze waziwazi kwamba kama itakuwa ni Mjumbe Bodi basi kama kwenye *Civil Society* awe ni yule anayepambana na mapambano dhidi ya rushwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kadhalika, nilikuwa naomba katika kipengele hicho hicho kinachozungumzia kuhusiana na Bodi, nilikuwa napenda *religions group* ziwepo. Kwa sababu ni watu muhimu sana! *Religions* ndiyo wana watu na wanaweza wakahamasisha jamii kwa njia moja ama nyingine na watu wakaachana na masuala ya rushwa.

Kadhalika katika hii Bodi nilikuwa naomba suala la *media* lisitupwe, lisiachwe pembeni, ni watu muhimu sana na ni watu ambao naamini hata wakiingia mahali wanaweza wakaisadia Bodi ikafanya kazi vizuri na ikatoa mwongozo na kuweza kusimamia masuala mazima ya kupambana na rushwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipengele cha 16 kimezungumzia juu ya Bodi itakavyofanya kazi zake. Lakini hapa ningeomba vilevile eneo hili liongezwe...

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, niwakumbushe tu kwamba eneo la Bodi, Bodi imefutwa. Kwa hiyo, katika uchangiaji wenu kama ulikuwa umejiandaa kuchangia kwenye eneo la Bodi labda kama una jambo maalum kabisa, lakini eneo hilo halimo. Nilikuwa natoa taarifa tu, Mheshimiwa Killimbah unaweza kuendelea.

**MHE. JUMA H. KILIMBAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na pengine nilikuwa natumia ule Muswada wa mwanzo kabisa, lakini ule wa pili ambao sijaupata nasema, naomba niweze kuendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuendeleza masuala ya pambano dhidi ya rushwa, suala la uwazi kuna kipengele kinachozungumzia mikataba ambayo tumesema kwamba kutakuwa na uwezo wa kudhibiti hii mikataba ambayo ina rushwa dhidi ya mikataba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipengele hiki nilikuwa naomba sana, kwa sababu katika utawala bora tuna masuala matatu ambayo tunazungumzia uwazi, uwajibikaji, pamoja na ushirikishwaji. Hili katika suala la *transparent* ndipo rushwa inapokuwepo.

Sasa kwenye suala la mikataba, ili tuweze kudhibiti vizuri hii mikataba, nilikuwa napenda katika kipengele hiki na pia pengine tuwe wa wazi kama vile tunavyofanya kwa maeneo kama *MEM* ambayo yalifanyika, mbao za matangazo mashuleni zikawa zinaonyesha pesa zile zilizotumika na wananchi wakaweza kuhoji na wakatoa maoni kwa masuala mbalimbali kuhusiana na zile pesa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, katika suala hili, nilikuwa naomba kwamba lazima sasa suala la mikataba kama tunakwenda tunasema kwamba hili tunaweza kudhibiti rushwa katika mikataba na mikataba iwe ya bayana ili kuondoa mang'ununiko na pengine kwa wananchi pale wanapotaka kuhoji kama wanahisi kuna rushwa katika

mikataba wawe na uhakika na mikataba hiyo, ni pesa ngapi ambazo zimeingiwa mkataba na waweze kutoa maoni yao na waweze kutoa taarifa kwa chombo husika kama wanaona kuna dalili zozote za rushwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kadhalika ningezungumzia suala la adhabu ambazo nimezisoma, zinaonyesha kwamba adhabu wanaweza kupewa na hii imetajwa katika hii sehemu ya mkataba kwa mfano wanasema mtu akikamatwa na kosa moja na hilo kosa anaweza kuhumiwa kwa faini ya shilingi milioni moja hadi milioni tatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pesa hizi za adhabu ni ndogo sana kulingana na makosa yenyewe. Mtu amekula rushwa kupitia mkataba, mkataba unaweza ukawa wa Shilingi bilioni mbili, halafu akaja akapatikana na kosa la rushwa, maana yake rushwa katika Shilingi bilioni mbili pengine wao wala rushwa wana mipango yao na wana njia wanachukua kwa kupitia kitu kinaitwa labda *percent*. Sasa ukija kuangali rushwa kama ya Shilingi bilioni mbili, *ten percent* yake ni pesa ambazo zinakaribia Shilingi milioni 200.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kama huyu mtu atakuwa kweli kadhihilika, kweli na Mahakama ikamtia hatiani, akaenda akaambiwa alipe milioni moja, bado itakuwa haisaidii kabisa. Kwa hiyo, tunachoomba katika hii adhabu, mimi nilikuwa napendekeza kwamba adhabu ya mla rushwa iwe kali kama tunavyofanya adhabu nyingine ambazo tumewahi kutoa.

Bunge hili Tukufu limewahi kutoa maamuzi kwa adhabu mbalimbali kama za wabakaji ambao wanafungwa kifungo cha maisha. Kwa hiyo, ninaamini, mla rushwa yeyote ambaye atapatikana na kosa katika maeneo kama haya na hasa ya mikataba, ambayo mikataba tunaamini kabisa ndiyo inayoendeleza masuala muhimu ya nchi yetu na kufanya nchi yetu ipige hatua za kimaendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naamini adhabu ya kifungo sio chini ya miaka 20 hadi 30, huyo mtu anayepatikana na adhabu hiyo atumikie na si adhabu hiyo peke yake! Kadhalika achapwe viboko. Mwalimu aliwahi kutoa mfano mmoja, akasema aliwahi kutokea Waziri aliwahi kula rushwa, akasema achapwe viboko 12 akiingia na wakati anatoka akishamliza adhabu anachapwa viboko vingine 12. Yaani anaingia na viboko 12 na akitoka anapata vingine 12 akamwonyeshe mke wake, kama ni mwanaume akamwonyeshe mkewe na adhabu akiwa ametumikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la rushwa linamgusa kila mtu na hatuwezi kuondoa umaskini tulionao kama hatutatoa adhabu kali juu ya wala rushwa ili wakaogope zile adhabu. Kwa hiyo, wakijua kabisa kwamba tukipatikana na kosa la rushwa, basi tutatiwa hatiani na tutatumikia adhabu kali ya vifungo na ambavyo pengine vinaweza vikatupoteza kabisa na tukatenganishwa na familia zetu.

Kwa hiyo, naamini heshima itapatikana na nchi itarejea katika heshima kuliko hali ya sasa hivi ambayo tunazungumza rushwa, lakini tunapozungumza rushwa, watu wenyewe wanabadilisha tu namna ya kuchukua rushwa. Ukizungumzia sheria

inavyowekwa namna hii, kesho anakuja na utaratibu mwingine na njia nyingine ambazo anaamini atajihalalishia ili aweze kuchukua rushwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru tena kwa kunipa nafasi hii. Naunga mkono hoja hii, ipite kwa asilimia mia moja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. JUMA A. NJWAYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ingawaje natambua kwamba kibidamu ilirukwa kidogo maana ulikuwa umenitangaza kabla ya mwenzangu aliyekuwa ameketi punde. Niungane na Wabunge wenzangu kwanza kuwapongeza Mheshimiwa Florence Kyandesa na Mheshimiwa Mtutura A. Mtutura kwa kujiunga na Wabunge kuwawakilisha Watanzania wenzetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nichukue nafasi hii kutoa pole kwa familia ya Dr. Aaron Chiduo na kwamba tunamtakia kila la kheri kwa Mwenyezi Mungu, Mungu asimtupe amlipe thawabu, maana amechangia maendeleo ya nchi hii kwa kiwango kikubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lililopo mbele yetu ni kuhusu Muswada wa Rushwa na kwa kweli naamini kwamba umeletwa ili kuziba mianya iliyokuwepo kwa sheria zilizopo na hasa kwa sura Na.329 mimi kwa kweli sina mengi sana, lakini nataka kutoa ushauri kwa Serikali. Ushauri wangu wa kwanza ni kwamba suala la rushwa ni pamoja na utawala bora.

Katika hali ya sasa wananchi wanakosa imani ya Serikali yao kwa sababu ya mambo madogo madogo yaliyopo ikiwa ni pamoja na rushwa. Kwa hiyo, ombi langu kwa Serikali ni kwamba Serikali isiogope kutumia gharama, kama kuna nchi ina-*base practise* zilizofanikiwa sisi tukachukue kule tuzitumie hapa bila sababu ya kuwa na wasiwasi, suala ni kujenga mafanikio ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili ni suala la adhabu. nimejaribu kuangalia hapa, adhabu nyingi zipo, nyingine zipo ndogo na nyingine zipo kubwa, lakini mimi nataka kupendekeza adhabu moja na ambayo ningependekeza kwenye Muswada huu iwekwe, kwamba ukiwa *found guilt* wewe adhabu yako kwa maisha iwe kwamba hauruhusiwi kupewa nafasi yoyote ya kugombea kwenye Chama cha kisiasa au nafasi yoyote ya umma, kwa sababu nia hapa ni ku-*discourage existence* ya rushwa nchi hii. Lakini tukiendelea na hali iliyopo hivi sasa ya kuwapa nafasi, wewe umekutwa umetumia rushwa na Mahakama imekupa adhabu ya rushwa bado kesho na kesho kutwa una nafasi ya kugombea au kushika nafasi yoyote ya umma, kwa kweli inakuwa ni kama kutwanga maji kwenye kinu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni kwamba wengi wape. Waheshimiwa Wabunge wengi walionitangulia hapa wamesema sana na kwa uchungu juu ya suala la *power* ya *DPP* katika suala la rushwa. Mimi nina mawazo kwamba kama Serikali inaona ni lazima *DPP* awe na nafasi, basi katika sheria hii nategemea kuna *regulation* zitakuwepo, basi tu-*set standard* au *roles* ambazo *decision* zozote anazofanya *DPP* aweze kueleza *the reason for the decision.* Hali hii itambana kidogo na kumweka katika

mazingira ambayo kwa sababu kuna mahali anabanwa, aeleze uamuzi huo alifikia kwa misingi gani, basi itapunguza suala la rushwa kwa sababu tunaweza tukawa na *DPP* hapa.

Mkurugenzi wa mashtaka ambaye ni mla rushwa akawa na vitu vya ajabu sana, lakini tukiwa tumesha-*state* vitu vyetu inaweza ikapunguza sana yeye kuwa na mambo ya ajabu katika rushwa. Lakini pia katika kufanya huu uamuzi anaoufanya inapotokea madaraka yake yamekasimiwa na mtu mwingine, basi mtu huyo anayekasimishwa madaraka awe ni mtu ambaye ni Afisa Mwandamizi Serikalini, siyo tu aliyeanza kazi juzi, maana unajua kuanza kazi kuna matatizo yake. Unaweza ukawa unasema hapa ndio pa kuanzia maana nimepata bulungutu hili ukaepuka kufuata maadili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni suala la *Report* ya Jaji Warioba kuhusu rushwa. Imebainisha wazi kwamba Mahakama zetu na hasa Mahakama za Mwanzo zina tatizo kubwa la rushwa na mimi hapa nataka niishauri Serikali kwamba kwa mtazamo wangu, wale *Court Assessors*, Wazee wa Mahakama wale kwa namna moja au nyingine wamekuwa wakichangia sana tatizo la rushwa pale Mahakamani na wale watu wana matatizo makubwa kwa sababu hata posho zao huwa zinachelewa kutolewa kwa wakati. Posho iliyoko ni ndogo na mambo ya namna kama hiyo ni mengi tu.

Ombi langu ni kwamba, Serikali ijitahidi kadri inavyoweza kutengeneza mazingira mazuri kwa wale *court assessors* maana wale ndio wanasimama wanakuwa katikati ya Mahakama na Washtaki au Washtakiwa maana kwao inakuwa ni rahisi kukutana na washtakiwa maana si ndio wanaoishi nao katika jamii tofauti na Hakimu, maana hakimu anaogopwa lakini yule ni rahisi tu wewe ukampata ukaongea naye, basi akawa kama daraja la kumfikia Hakimu. Hilo lilikuwa ni ombi langu lingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni suala la vitendea kazi kwa ujumla. Matatizo mengi tunayokumbana nayo ni vitendea kazi vya wadau mbalimbali wa masuala ya rushwa. Watendaji wa kule TAKURU wana matatizo, unakuta kuna jambo la haraka, lakini wana gari moja na mambo ya haraka yapo mengi inabidi wanyang'anyane hilo hilo, haiwezekani! Mishahara na hata nyumba ni matatizo! Hivi unakaaje nyumba ya kupanga na mwananchi wa kawaida ambaye kesho akiwa na tatizo inabidi umnyenyekee? Maana huwezi kuwa msumeno wa kukata nyuma na mbele wakati unakaa kwake! Akikuhamisha kesho na kesho kutwa unafanyaje?

Polisi hivyo hivyo, tumewaacha, nyumba wanazokaa ndio hizo tena, *full suit* na mambo ya namna hii. Mimi nadhani Serikali kama nilivyotangulia kusema, kwa sababu haya mambo ya utawala bora yana gharama, tusiepuke gharama, tufanye *investment* ya kutosha kwenye suala hili, vinginevyo tutaendelea kulalamika rushwa haiishi kwa kupuuza vitu vidogo vidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ingawaje nimelalamika kwamba ulimtaja mwenzangu badala ya mimi uliyekuwa umenitaja mwanzo, lakini nikasema mimi ni mwakilishi wa umma na sina sababu ya kuchelewa kufanya *presentation* au kutoa mawazo yangu leo

japo nilijiandaa kufanya Jumatatu. Kwa kifupi mawazo yangu ni haya na asanteni sana. *(Makofi)*

**MHE. DR. BINILITH S. MAHENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipatia nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia Muswada huu ambao ni nyeti sana. Lakini kabla sijaanza kuchangia, ningependa kuchukua fursa hii kwa niaba ya wananchi wa Makete kuungana na wananchi wote wa Tanzania kutoa rambirambi zetu kwa kada ambaye amefanya kazi Serikalini kwa muda mrefu katika nyadhifa mbalimbali kama Waziri, familia ya Marehemu Dr. Aaron Chiduo kuwapa pole sana katika wakati huu mgumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile nichukue nafasi hii kwa niaba ya wananchi wangu kumpongeza ndugu Abdallah Mtutura kwa kuchaguliwa kuwa Mbunge wa Tunduru, nami ninamuahidi ushirikiano wa karibu kwa niaba ya wananchi wangu wa Makete. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwanza kwa kuipongeza Serikali kwa sababu nadhani suala la msingi limeshajionyesha kwamba hoja ni ile dhamira. Kwa hiyo, nachukua nafasi hii kumpongeza hasa Rais wa Awamu ya Nne na viongozi wake wote kwa kulileta hili wazo kwa sababu kama mnakumbuka tarehe 30 wakati Mheshimiwa Rais akizindua Bunge aliongelea dhamira yake ya kuzuia na kupambana na rushwa. Kwa hiyo, nadhani hili ni suala la msingi sana kwamba limeshaletwa kwenye meza yetu, nadhani kazi yetu kubwa ni kuhakikisha tunasaidia kwa kutoa mawazo mazuri na kuuweka Muswada uweze kufanya kazi yake vizuri bila kuogopa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani kila mtu anafahamu madhara ya rushwa. Rushwa inakandamiza demokrasia, inakandamiza haki za binadamu, inaathiri amani na usalama na kwa vyovyote vile inaathiri ujenzi wa uchumi wa nchi yoyote ile. Ningependa labda niangalie hali ya rushwa kidunia. Nilikuwa naangalia katika dunia, kuna shirika linaitwa *Transparent International* ambao wao wanajaribu kuangalia nchi zote Duniani hali ya *corruption* ikoje na kwa miaka mbalimbali nimeweza kuchukua mwaka huu wa 2006 ambao una maoni ya nchi 163. Haya maoni yameonesha ni nchi zipi zinaongoza kwa *corruption* na nchi zipi ambazo zenyewe hali yake ni nzuri. Labda nizitaje ili tujue sisi tuko sehemu gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ninukuu nchi ambazo hali yake ni nzuri kati ya zile 163. Mojawapo ni Finland, New Zealand, Denmark na Sweden. Hizi zimechukua namba moja kati ya nchi 163. Lakini nikaangalia vile vile hali ya rushwa katika nchi kama ya Marekani, U.K nikagundua kwamba Marekani wao wamechukua nafasi 20 kati ya nchi 163 wakati Uingereza wamechukua nafasi ya 11 kati ya nchi 163. Sasa nikaja nikaangalia nchi zetu Tanzania tumekuwa nci ya nchi ya 93 kati ya 163 tukiwa na *corruption index* ya 2.9 kwa maana ya kwamba *index* ikiwa 10 maana yake rushwa ni kidogo inapozidi chini maana yake rushwa ni hatari zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nikaangalia wenzetu wa Kenya ambao ni jirani zetu, wao wamekuwa ni nchi ya 142 kati ya nchi 163. Kwa hiyo, nadhani kule hali siyo nzuri zaidi na Uganda vile vile nafasi ya 105 kati ya nchi 163. Sasa hii inadhihirisha

wazi kwamba kwanza sisi tumekuwa tukijitahidi sana kutokana na rushwa kwa kuangalia hizi takwimu, lakini vile vile inadhihirisha wazi kwamba hata wawekezaji wanapokuja katika nchi zetu pamoja na kwamba sisi tuna juhudi za kuweka mazingira mazuri ya uwekezaji, lakini hivi vitu vinaangaliwa kuona kwamba je, hali ya rushwa katika nchi hizi ukiwekeza ikoje? Kwa hiyo, nadhani ni hoja ya msingi ni kwamba, sasa imekuja na ina haki ya kujadiliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu ya pili inakwenda kwenye Muswada wenyewe na hii ni sehemu ya pili. Mimi nadhani kwamba kama tukiangalia hii sehemu ya pili *part 5(1)* inasema kwamba: *"The Bureau shall be an independent public body".*

Nadhani ugomvi mkubwa uko hapa kwa sababu hatujaweza kutoa tafsiri sahihi nini maana ya *independent public body* na nilikuwa naiomba Serikali, basi ingeweza hili neno kuliweka kwenye sehemu ya kwanza ya *interpretation* ili watu waweze kujua *limitations* za hiki chombo itakuwa ni zipi, kinaweza kufanya kazi yake katika mipaka ipi na ndio hii kingeweza kutuambia kwamba kwa mipaka hii hiki chombo kinaweza kubaki Serikalini au kinaweza kusimama na kitu gani na ninadhani kama tunge-*define* vizuri, hapa hatuna haja ya kubishana kwa sababu tukishaonesha mipaka yake, kazi yake inaeleweka na taratibu, kwa hiyo, tatizo la kuvutia huku wala kule halikuwepo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, pendekezo langu ni kuomba kwamba hili neno *an independent public body* liweze kuingizwa kwenye *interpretation,* itafsiriwe ionyeshwe *limitation* zake zikoje, likitokea hilo nadhani ugomvi wote hautakuwepo.

Lakini vile vile pamoja na kuipongeza Serikali, baada ya kusikia maoni ya wadau na kuondoa sehemu ya tatu ambayo ilikuwa inaelezewa kuundwa kwa Bodi, mimi natoa ushauri kwamba bado kitengo hiki cha TAKUKURU kiwe na Kamati yake ambayo itawajibika kwenye Kamati ya Bunge kama vile *ALAT*. Nadhani ni kazi yetu na tunapodhani kwamba kiende sehemu fulani, hatuna maana kwamba wenzetu hawafanyi kazi, nadhani tunatekeleza yale ambayo ameyasema Mheshimiwa Dr. Harrison Mwakyembe kwenye katiba ya nchi kwamba tungependa kuwawakilisha wananchi kama ipasavyo, lakini vile vile tungependa kumsaidia Mheshimiwa Rais wetu katika ile dhamira ambayo ameshaionesha. Kwa hiyo, mapendekezo yangu hapa ni kwamba ili kuwe na *transparency,* chombo hiki kiwe na Kamati yake, lakini vile vile hii Kamati itoe mambo yake kwenye Kamati ya Bunge ambao Wabunge ni wawakilishi wa Wananchi hawana *interest* yoyote ile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu yangu ya tatu ni sehemu ya rushwa katika mikataba, hapa ndipo ninaposononeka zaidi, kwa sababu unapoongelea rushwa katika mikataba, mara nyingi watu wanaona kwamba ni wakati *tender* inapotolewa au wakati *certificate* inaandaliwa ya mtu kutoa malipo au wakati wa kuomba kazi yoyote ile.

Lakini ipo *corruption* ambayo ipo kwenye akili ya mtu, yule anayeandaa ile *tender* anaweza akaandaa ile *tender* akimlenga mtu wa kampuni fulani na hiyo *corruption* ya akili ya mtu siyo rahisi kuikamata kwamba uliandika, ulikuwa unafikiria hivi, kwa hiyo, wewe labda unastahili kupelekwa Mahakamani.

Hii imenipeleka hapa kwa sababu ya hali halisi ya mikataba ya barabara. Barabara mwaka huu ziliharibika sana nchi nzima na ni fedha nyingi za Serikali zimekuwa zikiwekwa kila mwaka kwenye hizi barabara, lakini matokeo yake zikinyesha mvua barabara zinaoshwa zote na tunaambiwa mvua ni kubwa au tunaambiwa udongo ni mbaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilikuwa nadhani kwamba, ipo haja sasa hivi ya hawa wenzetu wa kitengo hiki, kwa kuwa wakati mwingine hatuwezi kukamata akili ya mtu alikuwa anawaza nini anaposaini, basi tuanzie kwenye ubora wa kazi, twende kwenye ile barabara ambayo imejengwa, tuwaruhusu hawa *PCB* ku-*investigate* kwamba kwa nini hii barabara imeharibika na fedha kadhaa zimetumika, basi ahojiwe mkandarasi atoe ushahidi wake na hivyo hivyo tutarudi kwa msimamizi wa Serikali upande wa *TANROAD* na hivyo hivyo kwa viongozi ambao walikuwa wametoa hiyo *tender* nadhani tunaweza tukapata ukweli wa hali halisi, kwa sababu haiwezekani kwani katika vitu ambavyo vinatumeza kiuchumi kukwamisha ni hili suala la barabara. Kila mwaka tunatenga mabilioni, lakini ikifika masika, zote zinaoshwa. Sasa nani wawajibike? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani tuwawezeshe wenzetu wawe na wataalam katika hii sekta ambao wanaweza waka-*asses* ubora wa kazi kulingana na hasara ambazo zimetumika na wakam-*task* mtu aeleze kwa nini barabara hii badala ya kuharibika baada ya miaka mitatu imeharibika baada ya miezi miwili? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo langu lingine ni kwamba, kweli faini ni kidogo, inabidi ziongezwe na vile vile hizi faini zingekuwa *classified* kulingana na aina ya makosa. Vile vile naungana na wenzangu kuhusu suala la kutokuwepo kwa *DPP* katika kushiriki ku-*process* haya mashtaka kwa sababu kimsingi wangeweza kumwachia yale masuala ambayo yana *interest* ya usalama wa kitaifa, lakini yale madogo ambayo yanaeleweka, nadhani kitengo hiki kingeruhusiwa kuyapeleke moja kwa moja Mahakamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo nilitaka kuchangia ni kwamba nadhani ni vizuri na nilitegemea kwamba katika Muswada huu kwa kuwa Mheshimiwa Rais katika hotuba yake ya tarehe 30 Desemba, 2005 alieleza dhamira ya kuona mienendo ya fedha katika vyama. Nakubaliana na wenzangu kwamba suala la uchaguzi linaweza kuwa linahitaji muda, lakini suala la kujua mienendo ya fedha katika vyama, *NGO's*, mashirika mbalimbali ya dini nadhani lingehusishwa kwenye Muswada huu ili tuweze kujua. Kwa sababu kuna *research* iliyofanywa na *World Bank* mwaka 1999 ya kuona vyama vinapata pesa namna gani na nikagundua kwamba vilivyo vingi vinakuwa vinafadhiliwa na makampuni makubwa na hivyo kuathiri baadhi ya maamuzi ya vyama hivyo. Kwa hiyo, nilidhani hilo ni la msingi, tukaanza kuliona kwa sababu tuna nia njema ya kuhakikisha kwamba tunaua rushwa moja kwa moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho nilitaka kusema kwamba kimsingi, kama kweli sisi tumedhamiria kuondoa hii rushwa, ni lazima mimi, wewe na mtu mwingine na hasa

wananchi na ile hali ya wananchi kuona kwamba rushwa inapungua au inapotea kabisa, lazima iendane na kila mmoja wetu kuchapa kazi kwa sababu matatizo mengine ni ya kiuchumi ndio maana watu wanaanza kuwa na tabia ya kutata rushwa. Kwa hiyo, naamini kwamba kama kila mtu atachapa kazi kwa uaminifu, kwa bidii na maarifa uchumi wetu utapanda na tutapata mishahara mizuri na hivyo hakutakuwa na vishawishi vya kuwa na rushwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi hii na ninaiunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. VEDASTUSI M. MANYINYI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi angalau ya mwisho katika siku hii ya Ijumaa ili na mimi niweze kuchangia katika Muswada huu ambao uko mbele yetu.

Awali ya yote, kwa niaba ya wananchi wa Musoma nami naungana nao kutoa pole kwa familia ya Marehemu Dr. Aaron Chiduo ambaye amekuwa kiongozi wake kwa muda mrefu na ninaamini sisi wote tunatambua mchango wetu katika nchi hii.

Lakini vile vile naungana na wenzangu kumpongeza ndugu yetu Mtutura A. Mtutura kwa kukipa Chama cha Mapinduzi heshima ya kushinda na kuwa Mbunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo ya utangulizi, naomba basi nimshukuru Mheshimiwa Waziri Philip Marmo kwa namna alivyoweza kuwasilisha Muswada huu ambao kwa kweli ni Muswada ambao ninaamini watu wengi tumekuwa tukiusubiri sana kwa hamu, maana suala lililopo mbele yetu kwa kweli ni tatizo kubwa ambalo linarudisha maendeleo ya nchi yetu nyuma. Lakini vile vile napenda kuishukuru Serikali kwa juhudi za makusudi ambazo inazifanya na kuzichukua zinazohusu kupambana na tatizo la rushwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la rushwa kwa kweli kama ni ugonjwa basi ni ugonjwa ambao ni mkubwa kuliko ugonjwa wowote ule na rushwa hii inatuumiza sisi sote, maana wakati ule unachukua rushwa unadhani wewe unafaidika, lakini ni kwamba tunajikuta ni rushwa ambayo inaendelea kutuumiza na inasababisha tuendelee kubaki pale pale tulivyo na ikiwezekana kurudi nyuma zaidi. Lakini vile vile tunaendelea kutambua kwamba kwa kweli rushwa ni adui wa haki na vile vile ni sumu ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unapozungumza suala la rushwa, kwa kweli sisi kama binadamu ni kawaida yetu kunyooshea vidole, maadam haujawahi kudhihirika, basi ni rahisi kusema fulani anakula rushwa. Ukiwa mwanasiasa ukienda kule hospitali, kutokana na zile huduma za kule hata mgonjwa kupewa asprini anaombwa rushwa, ukienda kule Polisi kama una tatizo na kwenyewe unakumbana na hali kama hiyo, halikadhalika ukienda ardhi matatizo yapo. Kwa hiyo, wote tunakuwa ni watu wa kuonyeshana vidole hata wanasiasa wakati ule wa mchakato tunayafahamu mambo haya. Kwa hiyo, kusema kweli leo tukisimama na tukaanza kuonyeshana vidole, mfano huu naufananisha na mfano wa kwenye biblia. Kwa wale Wakristo wanaosoma Biblia, kuna wale Mafarisayo ambao kule kwao dhambi kubwa ilikuwa ni dhambi ya kufanya uzinzi.

Sasa baada ya kuwa wamemkamata mwanamke mmoja akifanya uzinzi, walimpeleka kwa Yesu na adhabu ya wakati ule ilikuwa ni apigwe mawe hadi afe. Lakini Yesu kwa kutambua udhaifu wa binadamu, aliinamisha kichwa na akasema, hebu ambaye hana dhambi na awe wa kwanza kurusha jiwe juu ya mama huyu. Alikosekana hata mmoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwa nini nasema hivyo? Leo suala la rushwa tunasema linatuumiza kwa sababu kwa asilimia kubwa kila mmoja wetu kwa namna moja au nyingine amejikuta katika mazingira tofauti na suala hili limemhusu. Kwa hiyo, ndio maana tunasema tunapoleta Muswada huu katika kuuzungumza, lazima tudhamirie kwamba kwa kweli tuangalie kwa kila jinsi tutakavyoweza tuhakikishe kwamba hili suala la rushwa tunaondokana nalo. Zipo rushwa za aina nyingi kwa kadri ambavyo tumeambiwa, ukienda kule kwenye manunuzi, rushwa imejaa, ukienda huko kwenye ajira rushwa imejaa, ukienda huko unapohitaji huduma, habari ya mikataba rushwa kila mahali.

Kwa hiyo ndio maana tunasema kwa kweli ni suala ambalo tunahitaji tuliangalie kwa macho mawili, tudhamirie kweli kweli kuhakikisha kwamba suala la rushwa kuendelea ni sawa na jinsi ambavyo mtu unakata mti wakati ukiwa unasimama juu yake. Maana yake ni kwamba, hata kesho na wewe itakurudia. Hizi rushwa zipo za aina mbili. Ziko zile rushwa ambazo ni ndogo lakini zipo rushwa kubwa, lakini bado tunakubaliana kwamba rushwa ni rushwa, maana hata hiyo rushwa ambayo unadhani ni ndogo nayo ina madhara makubwa. Mfano unapokwenda hospitali, mgonjwa akaombwa Sh. 500/= ni rushwa ndogo sana, lakini yule mwenye mgonjwa anashindwa kutoa Sh. 500/=, matokeo yake mwanaye au anafariki mgonjwa wake anafariki. Kwa hiyo, tayari tunaona kwamba kumbe pamoja na kwamba tunadhani ni rushwa ndogo lakini madhara yake ni makubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali kadhalika zile rushwa kubwa kubwa kama tunavyozisikia rushwa za mikataba kwa kweli hizo ndizo zinazodidimiza uchumi wa nchi. Katika hali hiyo, sasa ni lazima tujaribu kutafuta viini kwamba hivi hasa hizi rushwa ndogo ndogo zinasababishwa na nini? Lakini hata na zile kubwa zinasababishwa na nini? Pamoja na kwamba rushwa ni tabia, lakini wakati mwingine mazingira nayo yanasababisha rushwa iendelee kuwepo.

Mfano, leo unapozungumza mtumishi katika nchi hii analipwa mshahara wa Sh. 60,000/= au analipwa mshahara wa Sh.70,000/= hiyo fedha hata kama ungeibajeti kwa namna gani, fedha hiyo haitoshi! Haitoshi kununua mboga, haitoshi kumsomesha mtoto na pia haitoshi ukafanya matumizi mengine ya kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kutokana na mazingira hayo, sasa pamoja na kelele ambazo tunapiga na dhamira tunazozichukua bado katika mazingira ya namna moja au nyingine yanamsababisha mtu ashawishike kuchukua rushwa na ndio maana leo hata kule unapokwenda kwenye *Council* wale Waheshimiwa Madiwani ambao wanapata posho ya Sh. 10,000/= wakati huo wana majukumu ya kupitisha mamilioni ya fedha leo tukizungumza tunasema *council* rushwa zimejaa.

Lakini pili, ili haya matatizo mengine yapungue, maana wakati mwingine Serikali inashindwa kulipa watu vizuri kwa sababu watu wanashindwa kuwajibika, leo unakuta Watanzania wengi katika masaa nane ambayo Mtanzania anapaswa kufanya kazi ukitafuta wastani aliofanya kazi sio zaidi ya masaa mawili. Kwa hiyo, upande wa kwanza Serikali haiwezi kumlipa, lakini upande wa pili vilevile hakuzalisha. Kwa hiyo, ni vizuri vilevile tungeangalia ni kwa kiasi gani watu wataweza kuwajibika.

Vilevile, hawa ndugu zetu wa *PCB* ni vizuri wakaeleweka, yaani tuwafahamu ili tuweze kuwapa *information* na ikiwezekana wajitahidi zaidi kutembelea katika yale maeneo ambayo zaidi yanakithiri katika hivi vitendo vya rushwa.

Hata katika hili suala la adhabu ambalo tumelizungumza hapa, ziko adhabu za aina mbili, yaani faini na kifungo. Lakini mimi nasema, suala la kumpa mtu adhabu kubwa au adhabu ndogo wala haisaidii, maana kwa kweli kama mtu ameiba Shilingi milioni mia tano, ukasema alipe Shilingi milioni ishirini, bado hujafanya kitu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata angefungwa mwezi mmoja, hiyo kwake ni adhabu kubwa maana leo hii ukiwaambia watu wengi kwamba afungwe hata mwezi mmoja na kulipa Shilingi milioni ishirini kama anazo milioni ishirini anasema bora alipe. Kwa hiyo, katika hiki kipengele cha adhabu kama hayo ndiyo yangekuwa maoni yangu ni kwamba, kifungo zaidi kingeangaliwa kuliko adhabu ya faini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuna kila aina ya sababu ya kuhakikisha kwamba elimu zaidi inatolewa kwa wananchi, wananchi waendelee kutambua kwamba kwa kweli rushwa ni adui wa haki na ni haki yao kupata huduma wanayopaswa kuipata pasipo kutoa chochote na tunadhani kwa kufanya hivyo sasa na wananchi wakiendelea kupata elimu zaidi itapunguza hii mianya mikubwa inayotokana na rushwa.

Lakini leo tumesema chombo kinachoshughulika na rushwa ni *PCB*, lakini kama ingewezekana katika zile ngazi zote, kunakuwepo na Kamati labda katika ngazi ya Wilaya kunakuwepo na Kamati ambayo inazungumza na kushughulikia masuala ya rushwa ambao wanasaidia kutoa *information* kamili, maana leo unapozungumza labda katika *Council* rushwa jinsi inavyotembea pale kama kuna chombo cha *Council* ambacho kinayazungumzia hayo ni rahisi kikawaelekeza zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwa sababu ya muda na mimi naomba kuunga mkono hoja na kusema kwamba naupitisha Muswada huo kwa asilimia mia moja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Tunakushukuru sana Mheshimiwa Vedastus Manyinyi, kwa mchango wako.

Waheshimiwa Wabunge, dakika zilizobaki hazitoshi hata kwa msemaji mmoja. Ningependa kuwakumbusha Waheshimiwa Wabunge kuhusiana na suala la semina ya kesho ambapo tutatakiwa tuwe katika Ukumbi wa Msekwa kuanzia saa tatu asubuhi.

Waheshimiwa Wabunge, katika Muswada huu, bado tuna maombi mengi tu ya Wabunge ambao wangependa kuchangia siku ya Jumatatu na ili kuwafanya wajiandae, ningeliomba niwataje kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Godfrey Weston Zambi, Mheshimiwa Chacha Zakayo Wangwe, Mheshimiwa Manju Salum Omar Msambya, Mheshimiwa Dr. Raphael Masunga Chegeni, Mheshimiwa Ruth B. Msafiri, Mheshimiwa Charles Muguta Kajege, Mheshimiwa Eng. Stella Martin Manyanya, Mheshimiwa Beatrice Matumbo Shellukindo, Mheshimiwa Vita Rashid Kawawa, Mheshimiwa Lucy Thomas Mayenga, Mheshimiwa John Magale Shibuda, Mheshimiwa Susan Anselm Jerome Lyimo, Mheshimiwa George Boniface Simbachawene, Mheshimiwa Benito William Malangalila, Mheshimiwa Ezekiel Magolyo Maige, Mheshimiwa Michael Lekule Laizer na Mheshimiwa Dr. Mary Michael Nagu kabla ya Mheshimiwa Waziri.

Kwa hiyo, utaratibu utapangwa Jumatatu na utaelezwa hapa na Mheshimiwa Spika, lakini ningeliwaomba basi Wabunge wahusika waendelee kujiandaa kwa sehemu zote mbili za Muswada huu maana Muswada huu unahusisha suala la kuzuia rushwa na suala la kupambana na rushwa *(Prevention and Combating Corruption)*

Waheshimiwa Wabunge, tarehe 26/02/2007 – 03/03/2007 Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Bunge letu walitembelea Bunge la Denmark na katika msafara huo nilipata bahati ya kuwa kiongozi wa safari hiyo ya Wenyeviti wa Bunge. Tulitembelea Bunge lao na wao watakuja kututembelea wiki ijayo Wabunge kutoka Denmark kwa nia ya kuhuisha uhusiano wa Mabunge ya nchi hizi mbili.

Tulipokuwa kule tulitembelea Bunge lao, lakini pia tulipata fursa ya kutembelea Wizara ya Kodi. Wanayo kabisa *Ministry of Taxation*. Tulipokuwa katika Wizara hiyo, tuliuliza suala la rushwa katika nchi ile kwamba vipi wenzetu hapa? Walichosema ni kwamba rushwa haiko katika utamaduni wao. Ni *minute* kiasi kwamba ni sawasawa na haipo.

Nimesema haya kuwakumbusha tu kwamba, iko haja ya kubadili utamaduni wetu kama Watanzania, kuona ni jambo la kawaida kutoa rushwa na kupokea rushwa. Kwa hiyo, pamoja na michango tuliyoizungumza lipo jambo *cultural aspect,* sheria peke yake bado itatusaidia sana, lakini vilevile lipo jambo la kujenga Taifa kwa kuanzia na vijana ambao wanachukia kabisa rushwa, yaani hawapokei wala hawatoi rushwa.

Waheshimiwa Wabunge, kama nilivyosema, muda wa Bunge umekaribiria na kazi zilizopangwa kwa siku ya leo zimemalizika. Kwa kufikia hapo, naomba niahirishe shughuli za Bunge hadi Jumatatu, tarehe 16 Aprili, 2007 Saa Tatu asubuhi.

*(Saa 01.25 Bunge liliahirishwa Mpaka Siku ya Jumatatu,
Tarehe 16 Aprili, 2007, Saa Tatu Asubuhi)*